ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri waMiundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge

10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani

36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Kwanza - Tarehe 9 Oktoba, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nimefurahi kukuoneni tena tukiwa katika shughuli zetu tukiwa wazima na namshukuru Mwenyezi Mungu kutukutanisha tena. Waheshimiwa Wajumbe karibuni sana katika shughuli zetu katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu.

Waheshimiwa Wajumbe Taarifa Spika, ya leo ni kama ifuatavyo:

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Baraza la Nane la Wawakilishi, uliofanyika kuanzia tarehe 3 Aprili, 2013 – 19 Aprili, 2013 Baraza lilipitisha Miswada Mitano ya Sheria kama ifuatavyo:

1) Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari na mambo yanayohusiana na hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu na Uwezo na mambo yanayohusiana na hayo

3) Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

4) Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

5) Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Biashara ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 12/6/ 2013 - 06/8/2013 Baraza lilitisha Mswada wa Sheria ufuatao:

Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi bilioni mia sita na hamsini na nane, mia tano na ishirini na sita milioni, mia tano na ishirini na nane elfu, kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30/6/2014 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90 (3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2012, naomba kutoa taarifa kwenu kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndiyo taarifa, kazi ya Mswada iliyofanyika katika Mkutano wa kumi na mbili wa Sheria ya Fedha. Huo ulitolewa taarifa mapema katika Baraza hili mara baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais kwa sababu ulikuwa unafanyiwa kazi mwanzo wa tarehe 01/07/2013. Kwa hiyo taarifa ya Mswada huo ilikwishatolewa mapema.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika Baraza lako hili Tukufu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba Kuwasilisha Mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 7 Agosti, 2013. Naomba kuwasilisha mezani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba Kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Vifungu mbali mbali vya Sheria ya Ardhi na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, nami naungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuweza kufika hapa leo na kuendeleza majukumu ambayo tumejipangia.

Baada ya hayo kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, katika Mswada wa Sheria.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 9
Kamati Teule za Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kabla sijauliza swali langu Nam. 9 kwanza naomba niseme machache. Nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Ali Mohammed Shein kwa mabadiliko madogo aliyoyafanya katika Baraza la Mawaziri na watendaji wake. Hii itawapelekea ufanyaji kazi mzuri kama inavyoelekeza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ili tupate ushindi mwaka 2015.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba swali langu (b) na (c) lijibiwe, swali (a) lisijibiwe kutokana na lile jengo linavyopendeza na tija itakayopatikana kwa serikali. Jengo hili limetoka wakati wa utawala wa Dokta Karume Rais ambaye ameleta maendeleo makubwa nchi hii ikiwe Serikali ya Ummoja ya Kitaifa, zikiwemo barabara Pemba pamoja na umeme na kumaliza majengo mengine ya Michenzani. Kwa maelezo hayo Mheshimiwa naomba swali (b) na (c) lijibiwe - Aliuliza:-

Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW) limekua likiunda Kamati za Uchunguzi za Baraza na kubaini ubadhirifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya madaraka.

(a) Kwa nini Serikali inashindwa kutekeleza maagizo ya Kamati kwa muda muafaka yakiwemo yale ya kutaka majengo ya Mambo Msiige kurudishwa Serikalini kutokana na kukodishwa kinyume cha sheria?

(b) Kwa kuwa Baraza kazi yake kubwa ni kusimamia Serikali, hatua ya Serikali kutozingatia maamuzi ya Baraza inaleta sura gani katika misingi ya Utawala Bora?

(c) Kuna sababu gani kwa Baraza la Wawakilishi kuendelea kuunda Kamati Teule za uchunguzi na kutumia fedha za walipa kodi wakati Serikali haifanyii kazi ripoti zake kwa manufaa ya nchi na wananchi wake?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 9 lenye vifungu (a) ambacho hataki kujibiwa, (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kuliarifu na kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba serikalli huwa inapokea ripoti zote zinazowasilishwa na Kamati za Baraza la Wawakilishi na ushauri unaotolewa na Kamati hizo huwa inafanyiwa kazi kikamilifu.

Aidha serikali inawajulisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatua ambazo serikali inachukua kwa mujibu wa taarifa zilizopelekewa kutokana na taratibu zilizopo.

Mhe. Spika, serikali hii ni sikivu na inatekeleza majukumu yake kwa kufuata misingi ya Utawala Bora, Sheria na Katiba. Aidha serikali kutumia vyombo vyake mbali mbali vya Dola katika kufuatilia kila tuhuma zilizoibuliwa na Baraza la Wawakilishi ili kutoa uamuzi wa haki na uliofanyiwa kazi kwa kina kwa kila muhusika.

Mhe. Spika, ni vyema ikaeleweka hatua mbali mbali zinachukuliwa na serikali zikiwemo za kiutawala, kisera na kisheria nia yake ni kujenga misingi ya utekelezaji ulio na tija, ufanisi na kujenga nidhamu na uadilifu ili kuondoa vitendo vyote viovu ikiwemo ubadhirifu ndani ya serikali, na haya yote yanafanyika kutokana na mchango mkubwa wa Baraza hili na Kamati zake zikiwemo Kamati Teule.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu kuna mihimili mitatu ya Dola, na kila muhimili una majukumu yake. Hivyo serikali inaamini kuwa kila muhimili utafanya kazi zake bila ya kuingilia mamlaka ya muhimili mwengine, na hivyo serikali itaendelea kufanyia kazi ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Baraza hili kwa kufuata sheria za nchi na taratibu zilizopo.

Mhe. Spika, kuhusu majengo ya serikali ambalo namuheshimu sana Mheshimiwa kutaka hili tulisilijibu lakini kwa kuwa majibu yake pia ni ya kuridhisha napenda niendelee. Serikali itahakikisha kuwa majengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yanayotolewa kwa uwekezaji yanafuata taratibu na yanaleta tija kwa nchi na watu wake yakiwemo majengo ya Mambo Msiige ambayo yanaendelezwa kwa mradi wa Hoteli ya kitalii ambayo itakuwa Hoteli ya aina yake katika mji wa Zanzibar. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya Mhe.Waziri kutofikia majibu ya swali la msingi naomba nimuulize swali moja dogo tu la nyongeza. Mbali na hatua zinazochukuliwa za kiutawala na za kisera, ni hatua gani za kijinai na za kuhujumu uchumi zilizochukuliwa kama zilivyopendekeza Kamati ya Baraza la Wawakilishi? Ni hilo tu Msheshimia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa sababu hatua ni nyingi, maana nilikuja nazo karatasi zote hapa kusudi nizieleze kinagaubaga hatua zilizochukuliwa na serikali katika kutekeleza mambo mbali mbali yaliyopendekezwa na Kamati Teule.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba basi nizitoe *copy*, ili Wajumbe wote wapate, kwa sababu nikisoma yote haya Mhe. Spika, naona itachukua muda mrefu. Hayo mambo ya jinai ni sehemu kwa sababu zipo kesi ambazo tayari zipo Mahakamani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi, mara baada ya tuhuma zinazotolewa na Baraza la Wawakilishi, serikali kwa kutumia vyombo vyake vya dola hufanya uchunguzi wa kina na hatimaye kuchukua hatua. Je, Mhe. Spika, katika hili Mhe. Waziri anatwambia kwamba maelezo yanayotolewa na Baraza la Wawakilishi kwa serikali huwa haiyaamini mpaka ikabidi aunde chombo chengine badala ya kuchukua maelezo haya na wahusika kuwapeleka moja kwa moja Mahakamani mpaka afanye uchunguzi kupitia serikalini, Ni kwa sababu haliamini Baraza au kwa nini akafanya hivi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba serikali inaheshimu, maelekezo na mapendekezo ya Baraza hili tukufu, lakini ikumbukwe Mhe. Spika, Baraza hili ndilo linaloweka sheria mbali mbali kwa nia ya kuongoza nchi, kwa nia ya kutenda haki, kwa nia ya kufuatilia mambo. Msingi wake ni kwamba yale maelekezo yanayotolewa na Baraza kwa asilimia 100, maelezo ya Baraza hili yameonekana yapo sahihi kwa serikali na napenda niwapongeze, lakini kwa sababu ya utaratibu ili kukamilisha hatua ambazo Baraza hili imeziweka ndio maana vyombo husika vya serikali kwa baadhi ya mambo yachunguzwe ili viweze kupelekwa Mahakamani.

Sasa hivi nimeulizwa swali hapa na Mhe. Jaku kwamba ni hatua gani huchukuliwa kwa mujibu wa yale makosa ya jinai. Huwezi kuchukua hatua bila ya kufuata mkondo wa sheria na taratibu zetu. Kwa hivyo Mheshimiwa sio kudharau hata kidogo. Sisi serikali tunaliheshimu Baraza hili na ndio maana tuko hapa sote tunafanya kazi kwa pamoja kwa nia ya kuwatumikia wananchi wetu, ahsante sana.

Nam. 40
Idadi ya Viwanda vya Serikali

Mhe. Abdi Mossi Kombo - Aliuliza:-

Hivi sasa nchi nyingi zinakwenda kwenye maendeleo ya mfumo wa viwanda ili kukuza biashara na kupunguza matatizo mbali mbali ikiwemo ya ajira kwa wananchi wake na kukuza uchumi wa nchi.

1) Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoendeshwa kwa mfumo wa Umoja wa Kitaifa ina viwanda vingapi?

2) Kama serikali inavyo viwanda hivyo vina wafanyakazi wangapi?

3) Ni bidhaa gani zinazozalishwa katika viwanda hivyo na zinasafirishwa nchi zipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 40 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba nianze na utangulizi ufuatao: Kwa mujibu wa utaratibu wa kiuendeshaji ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, masuala ya sensa ya viwanda huwa inafanywa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Takwimu inayotumika hadi hivi sasa Mhe. Spika, kuhusiana na viwanda ni ile iliyofanywa kwa mara ya mwisho mwaka 2008 na ingawa takwimu hizo ndizo bado tunaendelea kuzitumia.

(a) na (b) Mhe. Spika, jibu (a) na (b) naomba nilijibu kwa pamoja.

Kwa wakati huo Mhe.Spika, viwanda 150 vilikuwa vimeajiri watu kumi au zaidi ya 10 kwa kila kiwanda. Viwanda 2050 vilivyobakia vilikuwa vimeajiri watu wasiozidi 9 kwa kila kiwanda. Hivyo Mhe. Spika, kwa ujumla wake viwanda hivyo 150 wakati huo vilikuwa vina wafanyakazi 9,930.

(c) Bidhaa zinazozalishwa ni pamoja na bidhaa za vyakula,ushoni,bidhaa za nguo na ngozi, maji na juice, bidhaa za thamani, vyakula vya mifugo, *cassette* za sauti na *cassette* za picha, bidhaa za uchapishaji pamoja na bidhaa za ujenzi na usarifu wa bidhaa za viungo (*spices*). Miongoni mwa bidhaa zinazosafirishwa nchi za nje Mhe. Spika, ni pamoja na ngozi, mafuta ya karafuu, karafuu zenyewe, mafuta ya makonyo, mafuta ya nazi, viungo, mafuta ya viungo, vyakula vikavu ambapo hapa zaidi ni vyakula vya matunda na bidhaa, bidhaa zinazotokana na vyuma chakavu, mbao,

bidhaa zinazotokana na mbao *(furniture)*, bidhaa za vitambaa zikiwemo nguo, sabuni za viungo vinavyosarifiwa, bidhaa za vifaa vya umeme, bidhaa za madini na bidhaa za kazi za mikono.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2012, usafirishaji wa bidhaa umeongezeka kutoka 30, 189.21 kwa 2008 hadi kufikia milioni 67,390.5 kwa mwaka 2012. Bidhaa hizo zinapelekwa katika nchi zifuatazo:

1. Australia
2. Comoro
3. China
4. Denmark
5. Finland
6. Germany
7. Hong Kong
8. Indonesia
9. India
10. Italy
11. Japan
12. Kenya
13. Malawi
14. Liberia
15. Malaysia
16. Nertherland
17. Oman
18. Switzerland

19. Singapore

20. Swaziland

21. Afrika ya Kusini

22. Thailand,

23. Uganda,

24. Jamhuri ya Watu wa Kiarabu,

25. UK

26. USA na

27. Zambia.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante kwa majibu yako Mhe. Naibu Waziri. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa vile nchi yetu ya Zanzibar inasemekana kwamba ni nchi ya mwisho kiuchumi. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuimarisha viwanda zaidi ili nchi yetu nayo ipate kuendelea au kukuza uchumi wa nchi hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, tumekuwa tukijibu sana ndani ya Baraza lako hili tukufu kuhusu utaratibu ambao sasa Wizara imeanzisha. Wizara ina utaratibu tumekuwa tukisema kwamba unaandaa sera mpya ya viwanda. Tumekuwa tukisema kwamba sera hiyo iko katika hatua za kukamilika ili tuweze kwenda na wakati kufuatana na uchumi wa ulimwengu unavyokwenda, lakini pia katika suala zima la kuondosha tatizo la ajira kwa vijana. Sasa namuomba Mhe. Abdi Mossi atustahamilie wakati huu ambapo Sera hii ya Viwanda inaandaliwa halafu hatimaye itawasilishwa rasmi na yeye bila ya shaka ataipata.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake ametaja kwamba kuna bidhaa mbali mbali ambazo viwanda vyetu vimekuwa vikizalisha hapa Zanzibar. Je, ni bidhaa gani ambazo zinazalishwa hapa Zanzibar na zinasafirishwa nje ya nchi na ni kiasi gani cha fedha au kina thamani gani zinazoingiza serikali yetu katika kuleta maendeleo hapa Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ukiacha bidhaa ya karafuu na mafuta ya karafuu na makonyo, bidhaa nyengine zote nilizozitaja zinafanywa katika sekta binafsi. Kwa upande wa karafuu kama ndio hicho anachohitaji labda nimwambie Mhe. Nassor Salim kwamba mpaka sasa hivi tumeshasafirisha tani 140 za karafuu kwa msimu huu zenye thamani ya dola milioni moja, mia moja na arubaini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali langu dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri alivyokuwa akijibu alisema kwamba kuna viwanda 150, anaweza kutwambia viko wapi na vinazalisha nini na bidhaa gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, napenda nimuombe sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub,wakati majibu haya tunajibu hapa awe anasikiliza. Mhe. Spika, nimesema kwamba suala la sensa ya viwanda linafanywa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Nimesema hapa kwamba takwimu hiyo kwa kipindi hiki bado zinaendelea zipo katika hatua ya mwisho. Nikaendelea kusema kwamba takwimu zinazotumika ni takwimu zilizofanywa kwa mara ya mwisho mwaka 2008. Nimesema bidhaa ambazo zinazalishwa katika viwanda hivyo 150, na nikasema bidhaa ambazo zinasafirishwa, nikazitaja nchi ambazo bidhaa hizo zinakwenda. Sasa kama Mhe. Jaku Hashim anataka kwa orodha badala ya kurudia tena hapa nimtolee kopi hii nakala ili aweze kuwa nayo au afuatilie kwenye *hansard* Mhe. Spika.

Nam. 71

Faida Inayopatikana kwenye Mifuko ya Maendeleo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wake Dk. Ali Mohamed Shein, dhamira yake kuu ni kupunguza umasikini sambamba na kuongeza kipato kwa wananchi wake kupitia mifuko mbali mbali kama vile AK, JK pamoja na zile fedha zinazotolewa katika miradi inayofadhiliwa na TASAF.

(a) Ni kwa kiasi gani mifuko hiyo imefikia katika dhamira inayokusudiwa?

(b) Kwa kuwa mifuko hiyo sio ruzuku bali ni yenye mfumo wa Mkopo ambapo hutolewa na baadaye kurejeshwa kwa ajili ya kupatiwa wengine (*Rotating funds*) Je, utaratibu huo unafanyika?

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 71 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Idara ya Mikopo ambayo ipo chini ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa sasa inaendesha Mifuko miwili tu, mifuko hiyo ni kama hii ifuatayo:-

i) Mfuko wa Kujitegemea na
ii) Mfuko wa JK/AK

Mhe. Spika, dhamira ya Mifuko hiyo ni kuwapatia ajira wananchi kupitia shughuli mbali mbali za kiuchumi baada ya kupatiwa Mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa na mifuko hiyo.Lengo kuu likiwa ni kupunguza umaskini sambamba na kuongeza kipato kwa wananchi hao.

Dhamira hiyo imefikiwa kwa kiasi kikubwa kwani katika kipindi cha miaka kumi kuanzia Juni, 2003 hadi Juni 2013 jumla ya mikopo Elfu sita mia moja na hamsini na tisa (6159) yenye thamani ya Shilingi milioni mia nane na ishirini na tatu na laki tisa (823,900,000/=) imetolewa kupitia Mfuko wa Kujitegemea.

Mifuko hiyo imetoa ajira za moja kwa moja kwa watu elfu sita mia moja na hamsini na tisa (6159) wakiwemo wanawake elfu tatu mia mbili na saba (3,207) na wanaume elfu mbili mia tisa na hamsini mbili. (2952) Aidha mfuko wa JK na AK umetoa jumla ya mikopo 755 yenye thamani ya Shilingi Bilioni moja, milioni mia tano na hamsini na tatu milioni, laki nne na elfu thamanini na nne, mia nane thalathini na mbili (1,553,484,832/=) katika Mikoa Mitano ya Zanzibar.

Kupitia mikopo hiyo, wananchi wameweza kujipatia ajira, kuongeza vipato, kuzalisha bidhaa mbali mbali na kutoa huduma, na kuajiri wananchi wengine kupitia miradi waliyoianzisha.

(b) Mhe. Spika, utaratibu wa utoaji mikopo katika Mifuko hii ni ya mzunguko ambapo fedha zinazotolewa inabidi zirudishwe kusudi zitumike kuwapatia mikopo wengine.

Utaratibu huo ndio unaotumika hadi sasa na utaendelea kutumika ili fedha za Mifuko hiyo ziendelee kuwasaidia wananchi wengi na kwa kipindi kirefu zaidi.

Mathalan katika kipindi cha miaka kumi, kati ya Shilingi milioni mia nane na ishirini na tatu na laki tisa (823,9000,000/=) zilitolewa, Shilingi mia saba thalathini na tatu milioni hamsini na nne elfu, mia moja tisini na nne (733,054,194/=) zimesharejeshwa.

Aidha kipindi cha uhai wa Mfuko wa JK/AK, kati ya Shilingi bilioni moja, milioni mia tano na hamsini na tatu, laki nne na elfu thamanini na nne, mia nane thalathini na mbili (1,553,484,832/=) zilitolewa, jumla ya Shilingi mia nane arubaini na sita milioni, laki tisa kumi na saba elfu, mia tisa hamsini na sita (846,917,956/=) zimesharejeshwa na zinaendelea kuwafaa wananchi wengine.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, amekiri Mhe. Waziri kwamba yeye ana-*deal* na mfuko wa AK na JK na Mfuko wa Kujitegemea. Na kwa mujibu wa takwimu alizotoa ni kwamba hii ni *rotating fund* inazunguka, akasema milioni mia nane zimetoka katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita lakini milioni mia saba na kidogo zimerejeshwa. Kuna karibu milioni mia moja ambayo bado iko mikononi mwa wajasiri amali ambazo bado hazijarejeshwa. Kwa bahati mimi nimewahi kuitumikia hii Kamati yako Mhe. Spika, ya Baraza la Wawakilishi ya Wanawake na Watoto kwa utumishi uliotukuka mno. Tulipokwenda vijijini walisema turudishe vipi pesa hizi na katuletea Mzee Kikwete wanatwambia hawawezi kuzirejesha. Je yeye Mhe. Waziri katika hili ni utaratibu gani atatumia ili kuona zile milioni mia moja ambazo bado zinakwama kwa watu ambao wanaona mfuko huu ni wa Mzee Amani na Mzee Kikwete acha tuzile zimerudi serikalini ili wengine wapewe, atatumia utaratibu gani Mheshimiwa?

Pili Mhe. Spika, huu mfuko wa TASAF mara hii TASAF inataka kugusa mpaka katika *level* ya familia, kama walivyotupa semina juzi wanakwenda kwenye familia zenye mazingira magumu. Sasa jee hii mifuko yako Mhe. Waziri utaandaa utaratibu gani ili uweze kufika katika familia masikini kama walivyofanya wenzetu wa TASAF katika hii TASAF *three* inayokuja hivi karibuni. Nyinyi mtafika lini katika *level* ya familia?

Mhe. Waziri wa Nchi Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nataka nimwambie kwamba mikopo sasa

hivi tumeitungia kanuni maalum sio tunakwenda kienyeji enyeji tu, kwa hivyo tunahakikisha kwamba anayekopa anarejesha na tunamfuatilia mtu kabla hajakopa kuona miradi yake na shughuli zake na hasa tunakwenda huko vijijini waliko maskini za mungu maana ndio waliokusudiwa nao waweze kujinyanyua kiuchumi. Sasa kwa huko baadae sisi tutafanyaje, tutaendelea kufuatilia ili watu waweze kupata mikopo bila ya upendeleo wowote. Namuomba Mheshimiwa mwenzangu pale anataka aongezee kidogo Maalim Haroun.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa majibu mazuri. Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Saleh kwa ufuatiliaji wake makini wa kutetea wananchi wanyonge na hiyo ndio azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutetea wananchi wake wanyonge.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwa faida ya Wajumbe wote kwamba mfuko huu au mifuko hii yote ya AK, JK pamoja na Mfuko huu wa Kujitegemea pamoja na ule wa tatu ambao hajautaja Mhe. Waziri wa Uwezeshaji yote tuna lengo la kuikusanya pamoja na kuwa na mfuko mmoja, lakini pia mifuko hii yote sasa itaandaliwa utaratibu chini ya mfuko wa uwezeshaji na sheria zake na kanuni zake namna ya utoaji wa mifuko na namna ya ulipaji wa mikopo hiyo.

Ni kweli tumekuwa na matatizo makubwa na wenzetu wa PBZ ndio maana yake walishindwa kusema kweli kufuatilia, kwenda kufatilia mikopo ile kwa wananchi kutokana na gharama za ufuatiliaji ni kubwa zaidi kuliko kile ambacho kinapatikana. Na ndio maana serikali imepitisha maamuzi na nadhani siku si nyingi kwamba PBZ watakabidhi rasmi mfuko ule kwenye Wizara inayohusika ili usimamiwe na Wizara. Kwa hivyo kanuni zimeandaliwa, muongozo umeandaliwa na nina hakika muongozo huu utasaidia sana kurejesha pesa zile ambazo nyingi bado ziko mikononi mwa wananchi.

Taaluma ilikosekana ya kutosha wakati wa kutoa mifuko ile, lakini tunashukuru katika kipindi cha miaka miwili na nusu taaluma ya kutosha imetolewa na wananchi wameelewa. Lakini pia na utaratibu wa utoaji wa mikopo wenyewe ilikuwa na urasimu mkubwa sana, upitie kwa Sheha, Wilaya, sasa hivi tunataka mwananchi mwenyewe ana tatizo anataka kuchukua mkopo basi moja kwa moja anakuja Wizarani pale anapewa utaratibu na anajaza fomu na kupewa moja kwa moja bila ya kupata usumbufu wowote. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, ninashukuru kupata nafasi hii, Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika maelezo Mheshimiwa alipokuwa akijibu amesema kwamba kuna vijana karibu 7000 wamenufaika na ajira moja kwa moja, lakini nataka nimueleze Mhe. Waziri kwa kuwa Wizara yake haina uadilifu katika utendaji wa kazi zake, nasema hivi baada ya kujiridhisha baada ya Kamati kupita kupata taarifa za maelezo ya kazi au sera za serikali pasipo na ukweli nataka kumuuliza anaweza akatuthibitishia vipi hawa watu walionufaika katika maeneo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, mimi sikubaliani na Mheshimiwa kwamba Wizara yangu haina uadilifu, sikubali kabisa suala hilo.

Taarifa

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, Mhe. Waziri tunapozungumza ndani ya Baraza tunazungumza kwa mujibu wa taratibu na kanuni zinatutaka tuzungumze masuala ya ukweli. Sasa anaposema hakubaliani Kamati ambayo mimi ni Mjumbe; ya Wanawake na Watoto na Uwezeshaji ambapo yeye kama Waziri katika kikao alikuwa hayupo, imetudanganya kwa kutupa taarifa za uongo na tukataka lazima tukalione eneo *physically* la kilimo cha mboga mboga Tunguu. Baada ya kufika taarifa tulizopewa katika maandiko ziko tofauti na taarifa tulizozikuta. Sasa anaposema hakubaliani nalo anithibitishie hakubaliani kwa msingi gani.

Mhe. Spika: Sasa ni tafauti ya taarifa na uadilifu hivi ni kitu kimoja, mimi nadhani kuhusiana na hizi tafauti ya taarifa isioneshe kuwa hakuna uadilifu isipokuwa ni suala sasa ku-*cross check* kati ya taarifa mliyopata nyinyi na taarifa ya Wizara, lakini sio kwamba suala hili linaonesha hakuna uadilifu, uadilifu ni kitu kingine. Nadhani tuishie hapo najua hili suala linagusa watu sana, lakini limechukua muda mrefu kidogo ninafikiri tuendelee.

Nam. 3

Kutoweka kwa Vikundi mbali mbali vya Sanaa Pemba

Mhe. Bikame Yussuf Hamad – Aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya karibuni katika Kisiwa cha Pemba vikundi mbali mbali vya sanaa katika Tasnia ya muziki wa taarab vilishamiri na kuweza kutoa burudani ya uhakika kwa wananchi wa kisiwa hicho. Na kwa kuwa vikundi hivyo viliibuka na hatimaye kuyeyuka ghafla kama uyoga.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kushindwa kuimarishwa vikundi hivyo na hatimaye kutoweka ghafla namna hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mwakilishi wa Viti Maalum vya Wanawake swali lake Nam. 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu zilizopelekea vikundi vya tasnia ya muziki wa taarab Pemba kuyayuka ghafla kama uyoga ni nyingi; zikiwemo ukosefu wa fedha za kuendeleza vikundi hivyo, wasanii kutoona tija ya jasho lao, na imani ya dini inayoelekeza kuwa kupiga na kucheza ngoma ni dhambi.

Mhe. Spika, suala hili limepelekea hadi kujitokeza watu au vikundi vya watu ambavyo vinafanya juhudi kubwa ya kuzuia jaribio lolote lile la kuendeleza sanaa ya taarab au sanaa nyengine za maonesho.

Mhe. Spika, kukatika kwa msaada wa kiufundi na wataalamu kutoka vikundi vya Culture Musical Club kwenda katika vikundi vya Pemba ni moja ya sababu iliyochangia.

Mhe. Spika, pamoja na sababu zote hizo; ukosefu wa fedha umechangia sana kufa kwa vikundi vingi vya ngoma Pemba na sio taarab pekee. Kwa wastani ili kikundi kiweze kujimudu kuendesha shughuli za taarab kunahitajika kuwepo si chini ya shilingi milioni 10 kwa mwaka.

Mhe. Spika, fedha hizo ni kwa ajili ya kununulia vifaa vidogo vidogo tu vinapoharibika kwa bahati mbaya, vikundi vya taarab vya Pemba licha ya kuwa na vipaji vikubwa vya kutunga mashairi, utiaji wa muziki na kupiga muziki lakini havina mahala mwa kuonesha sanaa yao hiyo katika mpango wa kuingiza fedha kwa ajili ya kuendeleza vikundi hivyo.

Mhe. Spika, hiyo ni kutokana na wananchi wengi kuwa na kipato kidogo na hivyo kupelekea vikundi hivyo kufa kwa kukosa kuvidhamini na kusaidiwa kifedha.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema kuwa kuna ukosefu wa fedha katika vikundi hivyo, na kwa kuwa Mhe. Spika, tunashuhudia vikundi vingi vya uzalishaji, kupatiwa mikopo na vifaa mbali

mbali katika kuendeleza shughuli zao hizo za uzalishaji, na kwa kuwa Michezo pia ni miongoni mwa ajira. Jee ni sababu gani ya vikundi hivi kuwa havipati kusaidiwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwenye swali mama nimeeleza kuhusiana na swali lake alivyouliza ni kuwa vikundi hivi vimekufa na havionekani kwenye kisiwa cha Pemba nimejibu vizuri kwa ufafanuzi mzuri zaidi. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi wa Viti Maalum Wilaya ya Micheweni, najua kwamba amegusia sana kutokana na vikundi kuyayuka kama uyoga, ni kweli Mheshimiwa nimejibu na nimeeleza kwa kina lakini ninakuomba Mheshimiwa Mwakilishi ukiwa ni Mwakilishi ambaye unatokana na Mkoa wa Kaskazini Pemba na nguvu yako kubwa umeielekeza kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba, kufa kwa vikundi hivi nakuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane mimi na wewe ili kuviendeleza vikundi hivi ambavyo vimekufa na tuvifufue pamoja mimi na wewe ikiwa ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na unatoka Jimbo ambalo kimetoka kikundi hiki ambacho kimekufa kama uyoga.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika hapa leo katika mambo yetu mbali mbali ya kiserikali. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Spika, Zanzibar ni maarufu sana kwa taarab, na ni taarab ambayo huko nyuma ilikuwa ukichoka nyumbani kwako unakwenda kwenye taarab kupumzika kujistarehesha. Na kwa kuwa serikali ina mipango yake, je atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba sasa hivi kumeingia watu maalum wa kupiga vita vikundi vya kustarehesha katika Mikoa, Wilaya je atachukua hatua gani kwa sababu hizi ni taratibu ambazo tumezipanga na sheria zetu katika nchi yetu? Kumeingia wimbi hilo Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Asha Bakari swali lake la nyongeza kwamba jukumu la serikali kupitia Wizara yangu ni kuweka mazingira mazuri ambapo wananchi wanaweza kuanzisha vikundi mbali mbali iwe vya taarab au vya ngoma nyengine na kuwepo kwa mazingira ya usalama ili kuendeleza shughuli zao. Sasa serikali inafanya jukumu hilo. Vikundi mbali mbali katika mikoa yetu tumevipa usajili kuanzisha shughuli zao na hali ya utulivu na usalama wa nchi upo wa kutosha wananchi wanapotaka kufanya shughuli zao wanafanya shughuli zao.

Sasa kama kuna watu wanajaribu kuwashawishi sasa ni jukumu wanaoshawishiwa kuona kwamba shughuli wanayoifanya wanaifanya vizuri. Sisi tutahakikisha kwamba bado tunawapa nafasi wale ambao wanataka kufanya kazi hiyo tukiona tu kwamba hali ya utulivu wa nchi yetu imezingatiwa. Kwa hivyo tunachoweza kusema kama Wizara wale ambao wanataka kupiga shughuli za burudani basi wafuate sheria sisi hatuna matatizo, serikali haina matatizo na kwamba kuna watu wanawashawishi wasikubali kushawishiwa. Na kama kuna watu wana mtazamo wa kidini ni kweli kuna watu wana mtazamo wa kidini kwamba kupiga ngoma ni dhambi, sasa kila mmoja na itikadi yake ya kidini na uwezo wake wa kufahamu hilo. Wale ambao wanakubali bila shaka wamekubali hivyo, lakini la msingi sisi serikali ina mazingira ya kutosha ya kwamba wale ambao wanataka kusajili vikundi hivyo vya muziki au vyengine ruhusa ipo Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, nimefuatilia kwa uangalifu kabisa jibu la Mheshimiwa Waziri wangu mpendwa lakini nilikuwa nataka kumuuliza swali dogo sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri hivi karibuni katika ukanda wa kuanzia Jambiani, Bwejuu na halkadhalika na sehemu nyengine, kwa taarifa tulizozipata kuna vijana au wenye mahoteli wamefungiwa ili wasipige mziki. Mheshimiwa ni sababu zipi ambazo zilizopelekea hata wakafungiwa vijana hao?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, na naomba nimjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Mwakilishi wa Jimbo la Kitope. Ni kweli Mhe. Spika, kwamba hivi karibuni kuna watu ambao wanamiliki mabaa katika maeneo ya Paje, Jambiani na Bwejuu ambao wamekuwa wakipiga *disco* lenye kuudhi kwa wananchi. Wananchi wameilalamikia serikali kwamba hawalali usingizi, wagonjwa wana udhia mkubwa, wanafunzi hawapati fursa ya kudurusu, kwa sababu watu wana mabaa na wanapiga mziki kuanzia saa kumi na moja za jioni mpaka saa moja za asubuhi. Kwanza hiyo ni kinyume cha sheria, serikali hii ina sheria zake za upigaji wa mziki na taratibu zilizowekwa.

Kwa hivyo malalamiko ya wananchi tumeyasikiliza ni ya msingi, na kama serikali Wizara inayohusika imechukua hatua ya kuona kwamba wananchi wapate utulivu katika maeneo yao ya kuishi. Na tumezuia upigaji wa *disco* wenye kuudhi kwa wananchi wetu. Kwa hivyo ni kweli Mheshimiwa tumechukua hatua hiyo kwa makusudi na pahali popote pale ambapo wananchi watalalamikia kwamba upigaji wa muziki umekuwa ukiwaudhi na kuwaletea bughdha basi serikali itafuata sheria yake ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata utulivu katika maisha yao ya kawaida.

Nam. 39

Mchakato wa Mapitio na Marekebisho ya Sheria

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria inayo taasisi inayojulikana kwa jina la 'Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar' ambayo ina jukumu la kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake.

(a) Katika kutekeleza majukumu yake ni kwa namna gani Sheria inayofanyiwa marekebisho huingizwa katika mchakato mpaka ikafanyiwa marekebisho.

(b) Kwa nini hadi hii leo sheria mbali mbali ambazo zina utata hadi hii leo zimebakia kama zilivyo bila kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Salim Abdalla hamad Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe swali lake nambari 39 kama ifuatavyo:-

Katika kutekeleza majukumu yake Tume inafuata muongozo wa kuwashirikisha wananchi kwa pamoja ambayo inapitia katika hatua zifuatazo:

1. Kuna matayarisho ya mwanzo ya awali kuhusiana na sheria inayopendekezwa kufanyiwa mapitio.
2. Majadiliano ya mawazo ya awali kuhusu sheria husika.
3. Utafiti wa wazi.
4. Majadiliano ya Utafiti.
5. Mazingatio ya Wadau.
6. Ripoti ya mapendekezo ya ya matokeo ya utafiti.

Mhe. Spika, sheria zote za zamani kuanzia Mapinduzi matukufu ya 1964 huwa zinafanyiwa mapitio isipokuwa kwamba nyingi hazikufuata utaratibu wa sasa wa mapitio. Vile vile sheria ya *interpretation of laws and general provision act* namba 7 ya 1984 ni miongoni mwa mapitio yayofanyiwa na kuleta mageuzi makubwa. Kuanzishwa na kuimarishwa kwa Tume sasa sheria nyingi zinafanyiwa utaratibu na mapitio ya kisasa kama ilivyoainisha hapo awali. Hivyo Tume inaopitia sheria hizo kwa kuzingatia kipaumbele cha jamii na matakwa ya sheria pamoja na mapendekezo ya Wizara husika.

Ni kweli sheria nyingi bado zinahitaji kupitiwa upya na kazi hii ni ya taasisi yangu pamoja na wizara husika kutupendekezea ili tuzifanyie kazi ipasavyo, kwa mujibu wa mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Ninachopenda kusema Mhe. Spika, ni kuwa Wizara husika nazo zina mchango mkubwa katika kurekebisha sheria kwa wao kupendekeza kasoro zilizopo katika sheria inayohusika inahusu sekta zao, baada ya mapendekezo hayo ndio Wizara yangu kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wataendelea na suala hilo kwa mujibu wa utaratibu ulivyowekwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu yake mazuri ambayo naamini yametusaidia sote. Lakini Mhe. Spika, pamoja na maelezo yake mazuri ambazo sheria hizi kwa vile zinalinda haki, demokrasia ya wananchi, kubakia tu kutofanyiwa masahihisho mpaka leo ni sheria ambazo sisemi moja kwa moja lakini kwa upande mwengine huwa hasa zinasababisha migogoro.

Kwa mfano, kwa ruhusa yako Mhe. Spika, tukiangalia sheria hii ya uandikishaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi sheria nambari 7 ya mwaka 2005 kifungu nambari 6 naomba kukisoma kama kilivyo na lugha iliyoandikiwa ili kifahamike kimesema hivi. Kwanza kuna maneno yale madogo yanasema hivi:-

"Duties of the Director of Registration"

Halafu kinasema hivi:

"Subject to the provisions of this Act and directives of the Minister, the Director shall-

(i) Register every Zanzibari resident in Zanzibar who has attained the age of eighteen years and above;

(ii) Issue identity cards to every registered Zanzibar resident in Zanzibar;

(iii) Maintain a record of all Zanzibaris resident in Zanzibar to whom this Act applies.

Sasa hapa kuna hii *'and the directive of the Minister'*, yaani na maelekezo ya Waziri. Sasa Mhe. Spika, hii ni sheria na ikiwa sheria haitekelezeki na maelekezo ya waziri ambayo ni ya mdomo ndio utaona siku zote katika mambo haya ya vitambulisho kuna matatizo, na matatizo haya yanaendelea haki haitendeki, tumefuatilia na tumeona, kwa maana hiyo kubakia kama ilivyo inakuwa siku zote inapoteza haki.

La pili Mhe. Spika, tukija sheria Nambari 33 ya Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 23,

Kifungu 33(7) kinasema kwamba:

> "Iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa rais kwa mujibu wa kifungu hiki, basi hakuna Mahkama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuhusu kuchaguliwa kwake".

Mhe. Spika, wanaotangaza ni binadamu, kama katika mazingira wamekosea wasiulizwe tena ni kifungu cha pili kinabakia ambacho mpaka sasa hivi kinasababisha matatizo.

Mwisho mfano wa tatu, kwa sababu mifano ni mingi tukiangalia ukurasa wa 83 kuhusu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Kifungu 119 (12) kinasema hivi:

"Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya chama cha siasa".

Mhe. Spika, yaani ifanye inavyotaka yenyewe tu na ndivyo ilivyowekwa na katiba. Tukiangalia kifungu chengine kidogo,

Kifungu cha119(13) kinasema hivi:

> "Hakuna Mahkama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya katiba hii".

Kifungu 119 (14) kinasema hivi:-

> "Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano".

Mhe. Spika, hiyo Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi vizuri mara kumi kuliko ya Zanzibar katika kutenda haki. Je, Mhe. Spika, kuacha vifungu kama hivi kuendelea hivi hatuoni kuwa vitaendelea kuleta matatizo siku zote?

Mhe. Spika: Unajua hili swali ni swali la nyongeza linalofuatana kwa mujibu wa swali mama kwenye (b), nadhani ndio inahusiana na hapo. Lakini haya

mambo utakuta ni mapana mno na ni makubwa ambayo ingefaa wizara tuipatie nafasi ya kuzingatia kwa makini kutoa majibu mazuri, sina hakika kama Mhe. Waziri anaweza kuyajibu bila kufanya *reference* vizuri, maana umetaja mambo mengi ya sheria mbali mbali ambazo bado zimebakia vile vile kama inavyoonekana kwenye swali (b). Sasa nimsikilize Mhe. Waziri lakini inaelekea sheria za aina kama hii zingejitokeza moja kwa moja kwenye swali mama ili wizara na watendaji wakafuatilia kwa makini tukapata majibu ya usahihi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, mimi nafikiri jibu lipo na ni dogo tu, kwa hivyo naomba nimjibu Mhe. Mjumbe maswali yake hayo.
Kama nilivyosema katika majibu yangu kuwa wizara yangu haihusiki kabisa na utungaji wa sheria, wizara yangu inahusiana na utungaji wa sheria baada ya kupendekezewa na wizara husika. Sasa mimi siwezi nikasema tu kwamba sheria hii tuifanyie mabadiliko na hii tuifanyie mabadiliko aa, wizara inayohusika kwa mfano amesema mambo ya vitambulisho, sheria ya uchaguzi na kadhalika, waziri anayehusika na suala hili kama kuna matatizo katika sheria yake ndio yeye anapendekeza kwa wizara yangu.

Ukiacha hilo Mhe. Spika, mbali na waziri anayehusika Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kupitia Kanuni za Baraza la Wawakilishi anaweza kupeleka mswada binafsi kama yeye atahisi kwamba kuna matatizo. Kwa hivyo, sisi tukishapata ama kwa Waziri anayehusika au kwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio hapo sisi tunaendeleza marekebisho ya sheria kwa kupitia zile ngazi ambazo nilizitaja.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mjumbe kama kuna matatizo hayo awasiliane na Waziri anayehusika na Waziri hapa alipotajwa waziri sio Waziri wa Katiba na Sheria ni waziri anayehusika na sheria ile. Kwa mfano, suala la Tume ya Uchaguzi ni waziri anayehusika na Tume ya Uchaguzi ambaye atakuwa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi naomba awasiliane na wizara zinazohusika baada ya hapo tukishakubaliana kwamba kunahitaji marekebisho halafu wao watakubaliana tena sisi kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tutaendeleza katika kurekebisha ile sheria ambayo inahusika. Huu ndio utaratibu unaofuatwa kila siku. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya nyongeza juu ya swali la nyongeza la Mhe. Salim Abdalla Hamad hasa lile lililotaja sheria ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Katika suala lake alionesha kwamba sheria hii ni miongoni mwa sheria ambazo pengine zinahitaji kufanyiwa

marekebisho na akagusia vile vile kama kwamba hii sheria haitendi haki kutokana na ile sheria yenyewe ilivyo. Nataka kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba sheria hii ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi si muda mrefu Baraza hili hili la Wawakilishi la wananchi wa Zanzibar limeifanyia marekebisho, sikumbuki kikao gani lakini katika kikao cha mwezi wa Aprili au Januari itakuwa imefanyiwa marekebisho.

Sasa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na wakati ule sheria hii ilipofanyiwa marekebisho sote tulikuwepo, sasa sheria inaweza ikafanyiwa marekebisho hata kama imetungwa jana kama alivyosema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kama tunahisi sheria hii tuifanyie marekebisho wizara tupo tutaangalia hayo ambayo yanaonekana kama ni mapungufu ili tuweze kuifanyia marekebisho.

Lakini inaonekana sheria hii haifanyi haki, mimi nataka nitofautiane kidogo na Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, sheria hii inaeleza vizuri sana ni kwa vipi Mzanzibari Mkaazi anastahiki kupata kitambulisho cha Mzanzibari na ikumbukwe tu kwamba sheria hii tokea imetungwa imeshafanyiwa marekebisho zaidi ya mara tatu.

Sheria hii yenye kipengele cha masharti ni vipi Mzanzibari anaweza akapata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi hapo zamani ilikuwa zaidi ya miezi 36, nafikiri ilikuwa miaka mitano zamani, hivi sasa imepungua ule umri, na tulifanya hivyo serikali baada ya kuona kuna mapungufu ndio tukaweza kufanya hivyo. Sasa nataka nihakikishe kwamba sheria hii sasa hivi inatekelezwa kwa mujibu wa sheria na haimnyimi Mzanzibari haki yake ya kuweza kupata kitambulisho cha Mzanzibari ilimradi tu amefuata masharti ya sheria inavyosema hivi sasa. Ahsante sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, Mwakilishi anapozungumza jambo hapa huwa anazungumza yuko makini na anajua analolizungumza. Mhe. Spika, katika kikao kilichopita hivi juzi ilikuja hoja hii ya vitambulisho na Mhe. Omar Ali Shehe katika kuchangia alizungumza hivi na mimi katika kuchangia nikatilia mkazo mpaka Mheshimiwa mmoja aliyekuwa Waziri wa Wizara hii kwa wakati ule, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora tukakubaliana kwenda katika Mkoa wa Kaskazini na tukaonana na Mkuu wa Wilaya tukawaita wanaohusika na wengi walikuwa na haki ya kupiga kura lakini walizuiliwa, na tulipokwenda nashukuru kwa busara zake watu wale wakapatiwa haki yao ya kwenda kupewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, lakini mwanzo ilikuwa wameshakoseshwa. Kwa hivyo, tukisema kitu tunasema kwa uhakika wake na tunarudia pale pale kwamba hii sheria

haitendi haki kutokana na neno moja tu, '*the directives of the minister'*, kutokana na maelezo au pamoja na maelezo ya waziri ni hilo tu kama sheria ingekuwa haikutoa hivyo, basi naamini Mkurugenzi anayehusika angelifanya haki yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka sawa hoja aliyoizungumza Mhe. Salim Abdalla Hamad. Mhe. Omar Ali Shehe alileta hoja kwamba wananchi wa Jimbo la Nungwi hasa Kidoti na Fukuchani walinyimwa haki hiyo, nikamwambia twende, tukaenda mimi na yeye nikamkabidhi Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' wakahakikiwa hao watu 300 waliosema. Mhe. Spika, waliopata haki hawazidi watu 10 na mwenyewe huyo hapo au hayupo, hawazidi watu 10 na mwenyewe kakiri na akawagomba wale watu kwamba kwa nini nyinyi mnanisemesha uongo kwamba mnanyimwa, mnaonewa na kweli hamna haki, tumekwenda mguu kwa mguu mpaka kwa Mkuu wa Wilaya. Sasa Mhe. Salim Abdalla naomba haya maneno anapozungumza awe na uhakika, Wazungu wanasema, *"beat around the bush"*, azungumze moja kwa moja na uhakika. Ahsante Mhe, Spika.

Mhe. Spika: Inaonekana kwamba kuna tofauti ya taarifa hizi, hiki ni kipindi cha maswali tusijadili taarifa tofauti, kama kuna taarifa tofauti basi kila mmoja aangalie ili tuone kwamba tunapata taarifa zilizo sahihi, majadiliano ya hapa hayatatufikisha pahala kupata taarifa zilizo sahihi kwa hapa. Mhe. Salim Abdalla na Mhe. Waziri hebu kaeni muone kwamba mnapata taarifa zilizo sahihi. Tunaendelea.

Nam. 90

Mikataba ya Kazi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu nambari 90 nataka nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mpya wa wizara hii aliyekuwa makini Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, na isije ikaonekana kwa kuwa ni jamaa yangu hivyo nampendelea. Hii inatokana na utendaji wake makini na mahiri na tutegemee mambo makubwa katika wizara hii, na hii ni kutokana na kuacha jina zuri huko anakotoka. Baada ya maelezo hayo na sifa hizo naomba sasa swali langu nambari 90 lipate jawabu.

Mhe. Spika, Wafanyakazi katika Sekta ya Utalii kwa muda mrefu wamekuwa na kilio cha kufungishwa mikataba ya muda mfupi na kushindwa kunufaika na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) Zanzibar.

(a) Je, serikali imechukua hatua gani dhidi ya wawekezaji wenye tabia hiyo.
(b) Kwa nini wawekezaji katika sekta hiyo wamekuwa wakiwanyima wafanyakazi haki ya kutibiwa na fedha za likizo wakati ni haki yao kwa mujibu wa sheria.
(c) Je, ni waajiri wangapi wamechukuliwa hatua kwa kutozingatia sheria za kazi kutokana na sekta hiyo kuwa na malalamiko mengi ya uvunjwaji wa sheria.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma – Alijibu:-

Mhe. Spika, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi ya leo kuamka nikiwa na afya njema. Lakini pia kujibu swali langu la kwanza nikiwa na wizara hii mpya Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. *Inshaallah* namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tulete ule ufanisi tuliyoukusudia na kuwasaidia wananchi wetu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake nambari 90 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kifungu cha 44 cha Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005 kinatambua kuwepo kwa aina nne za mikataba ya kazi ambayo waajiri na waajiriwa kwa ridhaa yao wanaweza kukubaliana na kuingia kisheria katika moja ya mikataba hiyo. Aina ya mikataba hiyo ni pamoja na mikataba ya kudumu, mikataba ya muda maalum, mikataba ya masaa maalum na mkataba wa siku yaani *daily paid contract*. Hivyo mikataba ya muda maalum inatoa fursa muajiriwa kwa kunufaika na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuwakumbusha waajiri na waajiriwa juu ya haja za kutimiza wajibu wao na kufuata Sheria zetu za Kazi ikiwemo suala la kuwachangia wafanyakazi wao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Aidha, wapo pia waajiri wanaolalamika juu ya tabia ya baadhi ya wafanyakazi ya kutokubali kukatwa sehemu ya mshahara wao (5%) kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

Mhe. Spika, katika kutekeleza hilo, wizara imekua ikishirikiana kwa karibu sana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwa na Mikataba ya kazi na wanapata fursa za kuchangiwa na waajiri wao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Tumekuwa tukibadilishana taarifa za kiutendaji pale tunapobaini kwamba wapo waajiri wasiochangia wafanyakazi hao kwa lengo la kukomesha tabia hiyo kwani suala la hifadhi ya jamii ni miongoni mwa misingi ya kazi za staha *(Decent work*).

Aidha,Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar (*ZATUC*) na Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (*ZANEMA*) imepitisha Kanuni inayohusu mikataba ya kazi ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria za Kazi. Kanuni hiyo ilitangazwa katika tangazo la Kisheria (*Legal Notice Nam. 31* la mwaka 2013 na tayari imeanza kutumika. Kuwepo kwa kanuni hiyo, kutarahisisha sana utekelezaji wa sheria za kazi katika suala zima la Mikataba ya Kazi.

b) Mhe. Spika, nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba suala la mfanyakazi kutibiwa na muajiri wake kwa maradhi aliyoyapata akiwa kazini na malipo ya likizo ni haki na sio fursa, ili kuhakikisha kwamba haki hiyo ya wafanyakazi haipotei, serikali kupitia wizara yangu imeunda chombo cha kisheria kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa haki hiyo iwapo muajiri na muajiriwa walishindwa kuafikiana katika eneo la kazi. Chombo hichi cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro na mambo ya Kazi kipo na kinafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa sana sasa hivi.

Kwa tarifa ya Waheshimiwa Wajumbe katika kipindi cha mwaka 2012/2013 jumla ya Migogoro 179 ilipokelewa katika kitengo hicho. Kati ya migogoro hiyo, Migogoro 136 sawa na asilimia 76 ya Migogoro yote ilisuluhishwa na walalamikaji kupata haki zao. Migogoro iliyobakia inaendelea katika ngazi ya uamuzi. Aidha, migogoro 40 sawa na asilimia 22 ya migogoro yote ilisuluhishwa ndani ya kipindi kisichozidi wiki tatu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha wafanyakazi kwamba iwapo wameshindwa kupata haki zao za kutibiwa, likizo na haki nyengine kutokana na waajiri wao basi wawasilishe malalamiko yao katika kitengo cha usuluhishi na uamuzi wa migogoro na mambo ya kazi kwa hatua za kisheria. Kamwe hatutokubali mfanyakazi kunyanyaswa kwa sababu

nyengine yoyote ile huku wakikumbuka kwamba kila kwenye haki basi kuna wajibu.

c) Mhe. Spika, hatua mbali mbali zimechukuliwa katika jibu langu la (c) na kwa waajiri wanaoonekana kukiuka sheria za kazi ikiwemo, kuonywa na hata kufikishwa Mahkamani kwa wale walioonekana sugu. Jumla ya waajiri kumi(10) walipewa barua za kutekeleza amri (*Compliance orders*) kwa ajili ya kufanya marekebisho juu ya mambo mbali mbali yaliyobainika ikiwemo ukiukwaji wa sheria za kazi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013. Wapo pia waajiri wawili ambao walifunguliwa mashtaka katika Mahkama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe kutokana na madai ya kukiuka sheria za kazi na kutotii amri waliyopewa na kufanya marekebisho ya kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi wa kazi. Hatua hizo zimesaidia sana na kuwakumbusha waajiri hao juu ya haja ya kushirikiana katika kutii Sheria za Kazi kwa lengo la kuimarisha mahusiano mema kazini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri naomba kumuuliza Mhe. Waziri ni wafanyakazi wangapi wamenufaika na likizo na fedha hizo tangu kupitishwa kanuni hii ya mikataba ya kazi. Hilo moja.

Kwa kuwa mikataba ya kazi ni ya muda mfupi na muda mrefu, kero za wafanyakazi katika Sekta ya Utalii zimekuwa kubwa na wanakuwa hawapati pesa zao kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF)* mpaka wanapokuwa wazee. Je, wanatoa kauli gani kuhusu suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, swali hili la kumpatia idadi ya wafanyakazi hao litahitaji kwenda kulifanyia kazi zaidi, kwa sababu siwezi kubuni tu nikatoa takwimu ambayo si sahihi. Lakini kero za wafanyakazi ndio zile ambazo nimesema zilizowasilishwa ni 176, 136 tumezipatia ufumbuzi nyengine zinaendelea. Sasa kama wako wafanyakazi nimetoa wito kwenye jibu langu hili kwamba waje pale ofisini kwetu katika kitengo kinachohusika na usuluhishi wa migogoro ili tufuatilie kujua kwamba haki zao zote wanazostahiki kupatiwa wapatiwe.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya wawekezaji wanapowanyima haki wafanyakazi huwaambia kwamba wanaweza kufanya lolote kwa sababu wamewadhibiti maofisa wa Idara ya Kazi. Je, Mhe. Waziri anayo taarifa hiyo. Ikiwa ni kweli ni vipi maofisa wa

Idara ya kazi wakawaachia wawekezaji kuwadhalilisha wafanyakazi wa Zanzibar kwenye nchi yao?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, kauli hii imekuwa ikitolewa sana ndani ya Baraza hili ya wawekezaji kuwadhibiti wafanyakazi wa Wizara ya Kazi, hizi ni kauli nzito zinazotolewa kwenye kikao hiki kikubwa na lazima kuwe na ushahidi. Sasa Mhe. Salma kama ana ushahidi wa hayo uniletee, niliwahi kusema hapa katika kikao kilichopita kwamba tusichukue maneno ambayo hayana uhakika na kama yana uhakika mahali pa kupelekwa ni pale wizarani panapohusika. Sasa kuja kuyazungumza hapa tu kila siku kwamba kuna wawekezaji wanasema wamewadhibiti wafanyakazi wa wizara hii mimi sijalithibitisha hilo na hakuna hata kiongozi mmoja au Mwakilishi hata mmoja katika Baraza hili ambaye ameniletea ushahidi kuwa mfanyakazi huyu kapewa hiki, kafanya hiki, kafanya kile. Ninachoomba Mhe. Salma Mohamed kwa vile amelitamka hapa Barazani basi anitafutie ushahidi wake na napenda nikuhakikishie kama kuna mfanyakazi yeyote yuko kwenye madaraka yangu basi nitamuondosha na kumchukulia hatua za kufaa.

Mhe. Spika, kama yuko kwenye madaraka ya uteuzi wa Mhe. Rais nitapendekeza kwa Mhe. Rais ili achukue hatua za kufaa, na napenda nikuhakikishie kwamba hatutakuwa tayari hata mara moja wawekezaji wowote kuwadhalilisha, kuwanyanyasa wafanyakazi na wananchi wetu wa Zanzibar katika suala lolote lile la ajira katika sekta zao, ni wajibu wao kupata ajira, Wazanzibari wana haki ya kupata ajira lakini hawana haki ya kunyanyaswa.

Nam. 34

Ubovu wa Barabara

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman – Aliuliza:

Kwa kuwa serikali hutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuwaletea wananchi wake maendeleo kama vile barabara, lakini jambo la kusikitisha barabara hizo zinajengwa bila ya kuzingatia mitaro ya kupitisha maji, mfano barabara ya Kigope - Mtambile ambayo katika kipindi cha mvua za masika inakuwa haipitiki kwa kujaa maji.

Je, serikali inachukua hatua gani kuona inaiwekea njia ya kupita maji ili kuwanusuru wananchi na mali zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa maji ni adui mkubwa wa barabara, hivyo mitaro na madaraja ni moja ya suluhisho la kuzinusuru barabara hizo kutoharibiwa na maji. Mitaro hiyo huchimbwa pemebezoni mwa barabara kulingana na maumbile ya ardhi ilivyo pamoja na aina za udongo.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikizingatia mambo yote niliyoyataja hapo juu. Hata hivyo, maumbile ya maeneo mengi ya Kisiwani Pemba yakiwemo maeneo ya Kigope, Mtambile, Chanajamjawiri, Matuleni, Mgagadu, Kichunjuu na mwenginemo yana udongo ambao ukipata maji huporomoka (*slide*) hasa kwenye maeneo yaliyokatwa vilima na kujaa udongo kwenye mitaro ya maji hiyo, na hivyo kusababisha kutuama kwa maji barabrani na baadae kuharibu barabara pamoja na kuleta usumbufu kwa watumiaji.

Mhe. Spika, barabara ya Kigope – Mtambile baadhi ya maeneo ni miongoni mwa barabara zenye udongo unaoporomoka (*sliding soil*) baada ya kupata maji na kujaa kwenye mitaro. Wizara yangu tumeliona hilo na kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara tunaahidi kulifanyia kazi na kuimarisha mitaro katika maeneo yote tuliyoyataja.

Nam. 21

Wajawazito Kutojifungua Hospitali

Mhe. Farida Amour Mohamed – Aliuliza:-

Malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kupunguza na hatimae kuondosha kabisa vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua. Na kwa kuwa pamoja na juhudi zote zinazochukuliwa na serikali takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia 49 tu ya akinamama wajawazito wanaojifungulia hospitali pamoja na vituo vya afya.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea akinamama kuwa wazito kujifungulia katika hospitali pamoja na vituo vya afya vinavyokubalika.

(b) Kwa kuwa Wizara ya Afya hutoa huduma za kufika maeneo mbali (*outreach service)* katika mambo kama chanjo na kadhalika. Je, ni lini serikali itaanzisha huduma hii kwa upande wa uzazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa swali lake hili mambo yafuatayo ndio yanayowafanya akinamama wasiende hospitali.

(a) **1. Mila na Desturi**:

(a) Tuna mila na desturi potofu za jamii kuhusu kuzalia hospitali

(b) Ushiriki mdogo wa wanaume katika afya ya uzazi.

2. Elimu:

(a) Elimu duni ya mume na jamii anayoishi nayo mzazi mwenyewe juu ya umuhimu wa kujifungulia hospitali.

(b) Kudhani kwamba kuzaa kuna uzoefu kwa wale ambao wamezaa watoto wengi wa mwanzo salama

3. Maamuzi ya kwenda kujifungulia hospitali:

(a) Mzazi mwanagenzi, wazee na wakunga wa jadi kumuamulia azalie nyumbani.

(b) Lakini pia kinamama wenye umri mkubwa hawapendi kuzalishwa na wakunga wadogo wanaolingana na watoto au wajukuu wao.

4. Ni sababu ambazo ziko nje ya maamuzi ya mzazi mwenyewe

(a) Vijiji vya maweni ambavyo vigumu kufika usafiri

(b) Wakunga wa jadi kutowaruhusu wazazi kwenda hospitali kwa kujiamini au wengine kwao kuwa ni mradi, anapata chochote.

(b) Kwa upande wa uzazi tofauti na chanjo, maelekezo ya Shirika la Afya Duniani(*WHO*) ni kuhakikisha kwamba kila mzazi anazalia hospitali ili kupunguza vifo vya mama na mtoto. Kwa hivyo kufanya *outreach* kwa ajili ya kuzaa hilo halitowezekana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada ya Sheria ya Kurekebisha Sheria mbali mbali za Ardhi na Mambo Yanayohusiana Na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa **Ardhi**, Makaazi, Maji na Nishati. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba Mswada ya Sheria ya kubadilisha vifungu mbali mbali vya Sheria ya Ardhi na Mambo yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Spika, malengo ya mswada huu ni kueleza mapungufu yaliomo katika Sheria ya Ardhi ambayo yamekuwa yakiathiri katika utekelezaji wa shughuli zake za Idara ya Ardhi na Usajili pamoja na Ofisi ya Msajili wa Ardhi.

Aidha yapo baadhi ya marekebisho ambayo yamependekezwa kuzingatia hali ya Uchumi wa Zanzibar baada ya mtizamo wa kina baadhi ya vifungu vilionekana kwamba vinahitaji kufanyiwa marekebisho kuipunguzia Serikali mzigo wa fidia kwenye masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, mpango wa MKUZA II umeelekeza kuwa ifikapo mwaka 2015 asilimia 50% ya Ardhi ya Zanzibar iwe imesajiliwa. Aidha Serikali imetoa tamko kuwa majengo ya Taasisi ya Serikali na maeneo yote ya Serikali yasajiliwe na kupatiwa hati miliki. Katika utekelezaji wa zoezi hilo kwa kuanzia na maeneo ya Mji Mkongwe imeonekana kuwa Sheria ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1982 haitoi nafasi kwa taasisi kumiliki hati ya matumizi.

Kwa upande mwengine marekebisho haya pia yamekuja baada ya kuwa na wananchi ambao wanapewa Ardhi na Serikali kuidai Serikali ilipe fidia ya soko la Ardhi pale Serikali inapotakiwa kuchukua Ardhi hiyo.

Jambo hili limekuwa likiitia hasara Serikali ikizingatia kuwa wananchi wamepewa haki ya matumizi ya ardhi hiyo kwa kulipia fedha kidogo sana.

Mhe. Spika, dhamira ya Mswada huu ni kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika baadhi ya Sheria za Ardhi. Baadhi ya marekebisho hayo yataondoa mzigo mkubwa kwa Serikali kwa kulipa bei ya soko pale inapofuta hati ya matumizi ya ardhi kwa viwanja vilivyotolewa na Serikali.

Madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu vya Sheria ya Ardhi kama inavyoelezwa hapa chini.

(1) Marekebisho ya kifungu cha 8 cha Sheria ya namba 12 ya mwaka 1992. Kifungu kilivyo sasa kinatoa nafasi ya kumiliki haki ya matumizi ya ardhi kwa mtu binafsi tu na hakitoi nafasi hiyo kwa taasisi. Marekebisho yanayopendekezwa ili kuruhusu taasisi za Serikali kupata hati ya haki ya matumizi ya ardhi.

(2) Marekebisho ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Ardhi *land tenure Act* kifungu kilivyo sasa kinaeleza kuwa Serikali italazimika kumlipa bei ya soko mtu yeyote atayekatishwa haki ya matumizi ya ardhi. Kifungu hiki hakibagui yule ambaye amepata haki hii kutoka kwa Waziri au wale waliopata ardhi ile kwa kununua, kurithi au kupewa zawadi. Malengo ya marekebisho ya kifungu hiki ni kuweka tafauti ya fidia baina ya wale waliopata haki ya matumizi ya ardhi kwa kununua, kurithi au zawadi na wale ambao wamepata kutoka serikalini. Kwa wale ambao wamepewa hati hiyo na serikali kwa kulipia ada ndogo tu, pale ambapo serikali italihitaji eneo husika kwa matumizi mengineyo serikali iweze kulichukua eneo hilo na kumpa eneo jengine mbadala pamoja na kumlipa fidia ya maendeleo yaliyofanyika.

Mhe. Spika, wale ambao wamepata hati ya matumizi kwa njia nyenginezo iwapo serikali itakatisha hati zao za matumizi ya ardhi walipwe fidia ya maendeleo yaliyofanyika.

(3) Kuongeza kifungu kidogo katika kifungu cha 46 cha Sheria ya Ardhi. Malengo ya kuongeza kifungu hiki ni kuwatambua ndugu zetu walioko nje ya nchi ambao kwa sasa wana uraia wa nchi nyengine na ambao wana mali zao hapa Zanzibar au wanataka kujenga hapa Zanzibar. Kifungu hiki kinawapa nafasi watu hao kuitumia ardhi kwa ukodishwaji maalumu utakaokuwa na masharti mepesi yatakayowekwa katika kanuni ya sheria hii.

Mhe. Spika, maombi ya Kamati ya kifungu cha 47 yanayohusu kifungu cha 47 cha muda; hili naomba Baraza lako tukufu likubali tuje tulishughulikie wakati wa marekebisho ya mswada mzima wa sheria hii.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu Wajumbe wameupitia na kuutafakari vyema mswada huu na nategemea watatoa michango muafaka. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda, (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ahsante sana, Mswada umeungwa mkono sasa ujadiliwe.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebiso ya Sheria mbali mbali za Ardhi.

Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi kwa kuweza kutufikisha hapa katika chombo hichi muhimu kwa lengo la kutetea maslahi ya Wananchi wa Zanzibar, tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Spika, Shukurani za dhati pia nazileta kwako kwa kuniruhusu nitumie muda wako ili niweze kusema machache kuhusiana na kazi uliyotupa ya kupitia mswada wa Sheria uliyonituma mimi pamoja na Wajumbe wengine wa Kamati yangu kwa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.
Mhe. Spika, Kabla ya kuanza kutoa maoni, nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa nitakosa kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ambao kwa ushirikiano wao wa hali ya juu umeniwezesha mimi kusimama hapa leo, na kwa hivyo kwa ruhusa yako na kwa niaba yao naomba nitoe maoni kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Nina furaha ya dhati, kuipongeza Serikali kwa mawazo na fikra njema walizokuja nazo za kuifanyia Marekebisho Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992, kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi ambayo kwa sasa imekuwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, Kwa kuwa lengo kuu la marekebisho hayo, ni kuziwezesha taasisi za Serikali, kampuni na Jumuia za Kiraia, kupata haki ya matumizi ya ardhi, ambayo kwa Sheria ya sasa hazina haki hiyo. Naomba ieleweke kwamba kamati haina pingamizi na Taasisi za Serikali kupata haki hiyo, lakini wasiwasi upo kwa kampuni ambazo mara nyingi muelekeo wake huwa ni wa kibiashara zaidi, na hivyo kuzifanya ziangalie faida kuliko hasara, suali jee iwapo kampuni itaamua kuuza hisa zote kwa mtu asiyekuwa Mzanzibari

au kwa taasisi isiyo ya kiserikali, haki ya kumiliki ardhi ambayo itakuwa imetolewa tayari itarudishwa vipi bila ya kusababisha migogoro.

Mhe. Spika, Hoja ya kuzipatia Jumuiya za kiraia haki ya kumiliki ardhi, pia sio mbaya ingawa kwa miaka hii tuliyonayo ni vigumu kuweza kuzidhibiti jumuiya zenyewe hadi hapo tutakapokuwa na mipango bora na iliyo imara ya kuweza kuzidhibiti jumuiya hizo.

Mhe. Spika, Kamati imeitaka Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kulifikiria upya suala hili kabla ya kutoa mwanya wa kukaribisha migogoro zaidi ya ardhi nchini.

Mhe, Spika, Kamati pia imelifurahia wazo la Serikali kuwatafutia utaratibu wale waliokuwa na sifa ya Uzanzibari lakini wakapoteza sifa hiyo, ili waweze kupata ardhi katika nchi hii, hata hivyo Kamati inafikiria ni vyema watu hao wakapatiwa ardhi kwa njia ya kukodishwa kwa masharti mepesi tofauti na yale wanayopewa wageni ambao hawajawahi kuwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, Kamati inaamini kwamba kuwapatia ardhi kwa njia ile ile wanayopata wazanzibari halisi itakuwa sio sahihi, na pia inaweza kuleta migogoro zaidi kwa sababu ardhi hiyo itahitaji kurithiwa, na warithi wanaweza kuwa watoto ambao hawajawahi kuwa Wazanzibari. Hivyo, kwa kuepusha hili ni vyema utaratibu wa kukodisha ukatumika.

Mhe. Spika, jamii pia imekuwa ikishuhudia migogoro mingi inayozuka wakati Serikali inapotaka kuitumia ardhi ya mtu kwa shughuli za maendeleo ya wananchi (*Public Interests*) kama ujenzi wa barabara, skuli, uchimbaji wa kisima n.k. Serikali inalazimika kulipia gharama kwa malaki na mamilioni kwa ardhi hizo bila ya kujali kwamba ardhi hiyo imepatikana vipi.

Mhe. Spika, kwa marekebisho haya Serikali itaweza kulipa fidia tofauti kwa wale ambao wamepata ardhi kutoka kwa Serikali (Waziri) na wale waliopata kwa njia nyengine kama kununua. Kwa msingi huu, wale walionunua ardhi kwa bei ghali watafidiwa zaidi kuliko waliopata kwa bei rahisi kutoka kwa Serikali.

Mhe. Spika, hata hivyo Kamati inapendekeza kwamba, wakati wa kufanya tathmini na kupanga fidia basi badala ya kutumika fidia inayoridhisha itumike fidia inayoendana na soko la sasa.

Mhe. Spika, Kamati pia inaipongeza wizara kwa kuja na wazo la kuiondoa sehemu ya tatu ya mswada huu, ambapo kwa sasa wameona ni vyema sheria

hiyo ya usajili wa ardhi ifanyiwe marekebisho yote badala ya kuja na marekebisho ya kifungu kimoja kama kilivyokuwemo katika mswada huu.
Mhe. Spika**,** kutokana na muda naomba kuwasilisha baadhi tu ya mapendekezo hayo, lakini maelezo kwa urefu yanaonekana katika waraka wa maoni ya Kamati kama ulivyowasilishwa kwako.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, napenda nimalizie kwa kuishukuru sana Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yanayotuhusu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa, kwa niaba ya Wajumbe wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ambao napenda niwataje kama ifuatavyo:
Bila kujisahau Kamati hii inaongozwa na mimi mwenyewe:

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mjumbe
4. Mhe. Marina Joel Thomas Mjumbe
5. Mhe. Moh'd Haji Khalid Mjumbe
6. Mhe. Salma Moh'd Ali Mjumbe
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Mjumbe

Naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.
Lakini pia nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sitowashukuru Makatibu mahiri na makini wanaosaidiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu na kazi zetu za kila siku nao ni Ndg. Latifa Saleh Suleiman na Ndg. Saad Othman Saad kwa umakini wao wa kazi ambao umeiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa asubuhi ya leo kuweza kutia baraka na hasa sisi wengine tunakuwa masharifu. Kwa hivyo, mswada huu kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Waziri tutauchangia kwa ufasaha kabisa.

Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Makatibu wake na Wakurugenzi na Wataalamu wake kutuletea kitu hiki ambacho kitakwenda na wakati; ambao sasa hivi hali halisi ilivyo huku nyuma ilivyotokea tulikuwa na

migogoro mingi sana ya ardhi, na hasa kulikuwa kama kipengele ambacho cha kuwa wenzetu wengine walioondoka nchini wakaenda katika nchi nyengine. Lakini leo sasa w tutaweza na wao kwa mujibu wa sheria ilivyoeleza hapa ambapo tunataka tuipitishe kuwa na wao watawaza kupata ile ardhi kwa muhusika kama alivyosema kuwa ambaye anaweza kumrithi mtu ambaye aliyekuwepo hapa na akiwa na mali ya ardhi.

Mhe. Spika, mimi hilo sina tatizo nalo ninakubali sana. Lakini Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia sana katika mswada kuna jawabu ambazo nimeangalia katika marekebisho huku ambayo ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano kuna kitu ambacho muda ule wa kuhodhisha. Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri kama sikuvaa miwani basi naomba sana aje kunisaidia kwa lugha nzuri na ya ufasaha kabisa. Kwa sababu ni kipindi cha kumkodisha mtu miaka 99 kama nilivyofahamu mimi ni muda mrefu sana hauhalisi sasa hivi. Ningeomba sana anakuwa ananufaika yule mtu aliyekodishwa kwa muda ule na athari zake zinatokezea, baadae inakuwa serikali sasa kwa kuona manyago anayoyafanya yule mtu inashindwa serikali kuvunja mkataba kutokana na ile hali halisi.

Lakini tukiwa na muda mchache ambao una *cost* karibu miaka 50 mingi 60, kwa sababu 60 unaweza kufika hata mimi naweza kufika miaka 60 bado ningali hai. Kwa hiyo, ningeomba hapa tuangalie katika *time* hapa ya kuweza kurekebisha kipengele hiki.

Mhe. Spika, niweze kumuuliza Mhe. Waziri suala dogo hapa limenitanza sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri aweze kunipatia jibu la ufasaha kabisa. Katika marekebisho haya ya kifungu cha 4 ambacho chini kabisa ya kirumi (iii) anasema kuwa kupata ardhi kwa njia ya hiba au kwa mtu ambaye ana uhusiano wa damu.

Mimi nina mantiki nyengine na sitoweza kuieleza lakini yeye Mhe. Waziri ana wataalamu ndio maana wakampa *statement* hii ya kuweza kueleza humu. Ningeomba sana anisaidie lugha hii ya fasaha huo udugu wa damu wa aina gani ambao utakaoweza huyu mtu kumpa njia ya kupata ardhi kwa huyo mtu ambaye aliokuwa nao. Kidogo naomba tafsiri hapa inanikanganya Mhe. Spika, ningeomba anisaidie sana Mhe. Waziri ili kuweza na mimi kumpa nasaha zangu nzuri sana.

Lakini katika kifungu cha (b) anasema kwamba mwenye kuthibiti na maslahi ya Taasisi za Serikali, Kampuni, Mashirika ya Biashara na wenye hisa nyengine na ni wazanzibari na jumuiya.

Mhe. Spika, unajua hivi sasa kuna wengine wawekezaji wanakuwa wanaingia sana ubia na Wazanzibari wenyewe halisi hasa na kwenye kampuni wanakuwa wanapewa hisa ambayo ni kwa mujibu wa sheria hisa ile inakuwa kubwa sana. Sijui yeye mtu huyu linapotokea tatizo la kuanguka kibiashara au tatizo jengine lolote anamlinda vipi katika kumiliki ardhi hii ili wale ambao ni watu wa kuja tu. Ningeomba sana tatizo kama hili limetokezea Venta alikuweko kijana mmoja pale alihusishwa kwa kweli niseme na yule kijana pale hakutendewa haki.

Lakini serikali nasikia lile eneo limeshachukua limeshampa mtu ni sawa. Lakini alikuwa na yeye ashirikishwe kwa namna moja au nyengine ili kuleta neema ile pale aone na yeye ashirikishwe na yule mtu aliyepewa ili kupata kuendesha uzuri na kuondoa umasikini wake. Naomba sana hilo, na hilo tatizo lisije kutokea tena. Sisi tunapenda sana Serikali ikichukua jambo kwa uzuri kabisa ili kwa lengo la kuweka sawa, na lile eneo tunaomba haraka sana lifanyiwe kazi na ithibitishe ili kuweza kupata maendeleo zaidi.

Sasa naomba hapo likitokea neno kama hilo mtu kama huyo atasaidiwa vipi? Ningeomba sana Mhe. Waziri katika sheria yake hii ili aweze kunisaidia kupata upeo wa kuweza kuchangia vizuri.

Mhe. Spika, mara nyingi sana mimi hupenda kusema lakini kila mtu na matamshi yake. Mimi kutamka neno la aya Mhe. Spika, huona shida sana tu kwa sababu hili neno la aya linakuwa na tafsiri yake ambayo naifahamu mimi ikiwa kama ni sharifu. Kwa hiyo nawaomba sana wanasheria tutafutieni jina lililokuwa zuri hii neno aya, aya kushirikisha katika hivi vitu ambavyo baadae vitakuwa na athari na sisi vitakuwa vinatupa tabu. Mhe. Waziri wewe ulikuwa maalim naomba sana Mhe. Waziri wangu nipe hii tafsiri iliyokusudiwa hasa ya humu ndani ya vifungu hivi kuwa mimi nihalalishe kifungu hiki kwa neno la kuitwa "aya" naona tabu sana mimi Mheshimiwa ili kuweka sawa.

Lakini vile vile kuna kifungu cha (d) hati nyengine ya umiliki wa ardhi kulipia fidia yenye kurithisha au kuzingatia thamani ya ardhi pamoja na gharama za maendeleo yaliyofanywa katika ardhi hiyo. Mhe. Spika, hili nakubaliana nalo lakini linapoteza muda katika kuwalipa haki wale ambao wanachukuliwa maeneo yale.

Mhe. Spika, ningeomba sana kutanuka kwa migogoro ya ardhi katika kisiwa chetu ni moja hili. Kwa sababu kweli ardhi ni mali ya serikali nakubaliana nalo na wala sina tatizo. Lakini inapoona pale panapo maendeleo ambayo ya kudumu kabisa naomba sana Mhe. Spika, zile fidia ziwe haraka sana, zisichelewe kwa sababu leo utakuta wananchi katika maeneo ya ukanda wa Kiombamvua kwendea mbele juzi tu imepita barabara mpya nyumba zao

ukikaa nje unamuona mtu mpaka ndani, lakini mpaka leo hajalipwa fidia zake. Sasa na hili Mhe. Waziri sijui utatusaidia vipi kuweza kuhakikisha suala kama lile kabla Serikali kuchukua eneo lile halafu kuweza kusahihisha masuala hayo.

Kwa kumalizia Mhe. Waziri nikushukuru sana hilo lakini kuna mambo haya sasa hivi. Lakini kwanza nikupongeze sana katika hiyo *system* uliyoingia wewe katika wizara hiyo tumeona mambo mengi ambayo sasa hivi yanakuja mabadiliko. Umeona ubadhirifu mwingi sana unaofanyika katika wizara yako na wewe mwenyewe umeshuhudia, na hili nikushukuru sana tena nakupa nguvu hasa nakwambia Mheshimiwa usiogope wala usiyumbishwe sheria,sheria, tizama sheria ili uwasaidie wale waliokuwa wanyonge waliokuwa sheria inawakwaza. Mimi naomba sana hilo.

Jengine jitahidi sana haiwezekani kiwanja kimoja kikatoka katika *document* aina tatu kwa kiwanja kimoja na hilo nalo uliangalie, katika hiyo sheria ambayo umesema utakuja nayo huko mbele tunaomba sana uwe mkali sana kwa sababu ni moja katika kuleta mzozo mkubwa, hilo suala nakuomba sana Mhe. Waziri uweze kuridhia.

Mhe. Spika, kwa kweli nikiendelea nitakuja kutoa thamani ya mswada huu kwa sababu mswada huu chini ya usimamizi wake Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri, na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wake na watendaji walikaa kwa kina sana na kuweza kuthibitisha na kamati yetu hii kuweza kusahihisha baadhi ya mambo ambayo tuliyoyaona humu hili na sisi tunakubaliana sana.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono pamoja na wananchi wa Jimbo la Kitope kuhusu sheria hii ambayo itawasaidia sana wanyonge na itaendesha haki ambayo tunaipitisha hapa. Vyengine tukienda kinyume Mhe. Spika, itakuwa ni kosa letu sisi na Mwenyezi Mungu hatotuacha kutuhukumu.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati pamoja na Baraza lako kwa mashirikiano na utulivu na hekima ambao Baraza lako linatumia chini ya uongozi wako. Matumaini yangu vile vile chini ya uongozi wako na busara zako umetusaidia sana sisi Wawakilishi kupata nafasi ya kusonga mbele katika maendeleo yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli niipongeze Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati pamoja na Kamati nzima na uongozi mzima. Mimi ninaamini uongozi ambao unaongozwa na Mhe. Waziri mwalimu wetu mzee wetu Alhaj Ramadhan

Abdalla Shaaban pamoja na watendaji wake wote naanimi wizara ile sasa hivi imepata utulivu mkubwa sana katika hali yoyote ya jumla katika kuwashughulikia shida zao wananchi wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwa maana ya Zanzibar.

Mimi niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini naunga mkono haya yote ambayo yameelekezwa na yakaja mbele yetu.

Isipokuwa tu Mhe. Spika, jambo ambalo linalonishtua nataka nilizungumze suala la Ardhi. Mimi niombe wizara kupitia kwa Mhe. Waziri inanipa mashaka kidogo kwa Zanzibar na wizara inayohusika kwamba kwa ufahamu wangu mimi ingelikuwa kwanza tufanye tathmini ya hii ardhi yetu ya Zanzibar Unguja na Pemba kwa maana na visiwa vyetu vya Changuu na Mnemba Island.

Mhe. Spika, katika Baraza lako hivi karibuni la juzi nilizungumza mimi kuhusu kisiwa cha Fungu Mbaraka kwa Kizimkazi ambayo ni ardhi yetu ya Zanzibar na Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kusema kwamba Kisiwa cha Fungu Mbaraka kiko chini ya Ardhi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kauli ile jana tulipewa taarifa rasmi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba kisiwa cha Fungu Mbaraka sio mali ya Zanzibar ni mali ya ndugu zetu wa Tanganyika kwa maana ya Tanzania Bara rasmi tumeambiwa. Sasa Mhe. Spika, shaka inayonipa bila ya kufanya tathmini ya visiwa vyetu na visiwa vyetu na ardhi tutakuja kujikuta huko mbele tunazungumza ardhi, kisiwa lakini sio chetu. Sasa naomba wizara hii itakapokuja kwa kuwa suala hili wenzetu Bara wameshatoa agizo kwamba hiki ni chao na wakati kipo kwenye ardhi ya Zanzibar.

Sasa nimuombe Waziri hapa atakapokuja atusaidie tena kwa sababu Mhe. Spika, Baraza lako ni Baraza la kutunga Sheria sisi tumekuja huku kwa niaba ya wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba kama ni Wawakilishi katika Baraza lako.

Kwa hivyo, Serikali inatoa kauli ile rasmi lakini muda mfupi wenzetu Tanzania Bara wanatoa kauli kupitia Serikali ya Mapinduzi kwamba kisiwa kile ni chao. Kwa maana ile ardhi ni yao na tunavyojua sisi kwa ufahamu wetu kwa miaka zaidi ya mia ile ni mali ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Spika, mimi naona sasa huko tunakokwenda mbele kuna haja sasa wizara hii inayohusika ikatengeneza rasilimali rasmi visiwa vyetu hivi na ardhi yetu ili tusije huko mbele kila ardhi itakapokuwa inatajwa ikaja

tukaambiwa kuwa si yetu. Sasa Mhe. Spika, hilo linanipa mashaka makubwa na haya matamshi yametolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuambiwa sisi Wawakilishi sote tuliokuwepo humu ndani kwamba Fungu Mbaraka wenzetu Bara wanasema ni kisiwa chao kwa maana ya ardhi yao.

Sisi Zanzibar ramani yetu historia yetu na hiyo *inshaallah* mbele ya Mwenyezi Mungu tutasimama ni ardhi yetu. Kwa hiyo, ninachoomba mimi Mhe. Waziri atakapokuja hapa kufanya mjadala mzima wa ardhi atwambie tena hii ardhi na hichi kisiwa ni cha Tanganyika au cha Zanzibar ili tuwe huko mbele tunapokwenda tusije kugongana.

Kwa hivyo, ninachoomba tu kwamba suala hili lipate ufumbuzi kwa sababu limezungumzwa rikodi zipo na zitaendelea na taarifa hizo zilizotolewa jana mimi naomba hili suala lifanyike ili Wizara inayohusika ifanye tathmini upya kwa ardhi zetu na visiwa vyetu hivi kwa kuhofia kwamba huko tunapokwenda kutakuwa na mambo mengi. Ili watoto wetu, wajukuu wetu, virembwe vyetu waje kurithi jambo ambalo halitakuwa na mzozo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kusema machache katika marekebisho haya ya sheria za ardhi. Kama tunavyojua kwamba hivi sasa migogoro mingi imetawala katika sekta hii. Ni imani yangu kwamba kuja kwa sheria hii kutaondoa baadhi ya migogoro hiyo. Mhe. Spika, marekebisho haya yanawawezesha hata wasiokua raia wa nchi hii kuwa na wao watakuwa na fursa ya kumiliki ardhi.

Mimi nataka niende katika kifungu cha 4c. Kifungu hichi Mhe. Spika, kinasema Mzanzibari yeyote ambaye alikuwa ana sifa ya kuwa Mzanzibari na akapoteza sifa hizo atakuwa na haki zifuatazo.

Mhe. Spika, sifa hizi zimeorodheshwa hapa mimi nataka nizungumzie kidogo hii namba 2 kupata ardhi ambayo alikuwa akimiliki kihalali kabla ya kukosa sifa ya kuwa Mzanzibari.

Kifungu hichi mimi imani yangu kwamba kidogo kinahitaji maelekezo mengine, kwani hapa kinamfanya huyu atakayekuwa anamiliki ardhi apate hii sifa aipate tu hii ardhi, lakini baada ya kumiliki inawezekana pengine ardhi hii ikawa ipo tupu haijatumiwa au ardhi hii ikawa tayari imeshatumiwa.

Na jengine katika sifa tulizozieleza huku ni kwamba kuna haki ya kufidiwa yule ambaye ardhi yake imetumiwa. Sasa ningelitaka kujua tu kuna fidia yoyote ya yule mtu ambaye baada ya sheria hii itakuwa ardhi yake imechukuliwa atarejeshewa, lakini jee ikiwa ardhi hiyo imeshaendelezwa na zile fidia nazo ambazo zimo katika ile ardhi yake ikiwa imechukuliwa na

serikali au amemilikishwa mtu mwengine. Jee, vipi sheria hiyo itaruhusu na huyu mtu kupewa fidia zile ambazo zimo katika ile ardhi yake.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 3 kinachosema, "Kupata ardhi kwa njia ya hiba kwa mtu ambaye wana uhusiano wa damu". Huku kwenye tafsiri ya Kiingereza wamesema hiba ni *gift*. Sasa mimi nahisi ikiwa tunaweka hiba, labda Waarabu wangesema "hubbu", yaani upenzi.

Sasa kulikuwa kuna haja gani kwamba huyu mtu labda awe ana uhusiano wa damu? Kuna ulazima wowote. Ikiwa ni *gift* mimi nafikiria kama nimeamua kutoa ardhi yangu basi kusilazimishwe kwamba awe ni mtu ambaye atakuwa ni wa damu, tumpe tu kama mimi nimeamua *interest* yangu nimpe fulani ardhi yangu niliyonayo basi nimmilikishe tu, lakini tusiweke huu ulazima wa kuwa ni lazima awe ni mtu wa damu.
Lakini pia ikiwa hiyo haitowezekana basi hawa watu wa damu tungewa-*specify* tukawaeleza kwamba mtu huyu awe ni baba, mama, mjomba, shangazi, kuliko kuiweka tu mtu wa damu, anaweza siku nyengine huko tunakokwenda tukisema mtu wa damu inaweza ikaleta utata.

Lakini Mhe. Spika, niendelee kidogo katika kifungu cha 5 (2) (C)kinachosema kwamba, "Kwa kulipa fidia yenye kuridhisha ya ardhi pamoja na gharama za maendeleo yaliyofanywa katika ardhi hiyo".

Mhe. Spika, hivi sasa utaratibu nafikiria utararibu huo upo wa kulipia fidia lakini upande unaoridhika ni ule mmoja tu, upande ambao unaotoa fidia ndio unaoona kwamba fidia hii inatosheleza. Nafikiri hapa kwa kuiweka hivi haipo wazi kwa sababu wengine bado watakuwa wanaendelea kulalamika. Sasa tungetafuta utaratibu hili neno lenye kusema "kuridhisha" likawa na ongezeko jengine kwamba yule ambaye atakuwa anafidiwa na yeye basi awe ameridhika isiwe ni upande mmoja tu ambao utakuwa umeridhika, na huo ndio utaratibu uliopo hivi sasa. Sasa kuondosha hayo basi na huyu ambaye atakuwa amefidiwa na yeye aridhike ndio upatikane uhalali wa kutumia ardhi yake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie hapo. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah Subhana Wataallah kwa kutujaalia mara nyengine tena kukutana katika kikao hiki kuendelea na shughuli zetu za kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa visiwa hivi.

Nimuombe Mwenyezi Mungu atuongoze kwa hekima na busura tufanye yale ambayo tunayotarajiwa na wananchi na kusimamia misingi ya uadilifu katika chombo hiki ambacho ni ngome ya wananchi wa Zanzibar.

Pili Mhe.Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache kuhusiana na mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali za Ardhi na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na uongozi mzima wa wizara yake na watendaji wake, kwa kutuletea mswada huu ambao lengo lake ni kusawazisha baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yanakwaza utekelezaji wa masuala mbali mbali katika nchi yetu hasa suala lile la haki ya matumizi ya ardhi.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, kwa ujumla mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi; kwa hivyo maoni na michango mingi tulitoa kupitia Kamati yako na nashukuru na kumpongeza tena Mhe. Waziri kwa usikivu wake ambao ulipelekea kuelewana katika maeneo mengi.

Lakini moja tu Mhe. Spika, nimkumbushe Mhe. Waziri, nadhani ndio maana hivi kidogo imeleta matatizo katika michango iliyokuwa imeshatoka hadi sasa, tulimuomba kwamba yale marekebisho kutokana na jinsi yalivyofanyika basi ingependeza ule mswada ambao umeandikwa upya ungegaiwa kwa Wajumbe badala ya kuendelea kufanya marejeo kwa mswada ambao ule uliowasilishwa kwa kusomwa mara ya mwanzo katika kikao kilichopita. Nadhani ndio maana baadhi ya Wajumbe wanaendelea kuuchangia kama vile ulivyo badala ya kuzingatia yale marekebisho ambayo Mhe. Waziri aliyokuwa ameyasoma wakati anausoma mara ya pili hapa asubuhi hii.

Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwamba atajitahidi ayagawe ikiwa muda utaruhusu ili wakati wa kupitisha vifungu basi kusitokezee kugongana au kutofahamiana.

Sasa baada ya hayo Mhe. Spika, kuna mambo machache ningeomba niyazungumze yakiwa nje ya yale ambayo Kamati tayari imeshawasilisha mapendekezo yake ambayo yote ninathibitisha kwamba tuliyaamua kwa pamoja.

Mhe.Spika, katika maoni ya jumla ambayo tulimpa Mhe. Waziri nje ya mswada ule ni moja ninadhani limesahauliwa. Kwanza lilikuwa ni katika kifungu cha 2 cha sheria mama hii ya *Land Tenure Act* au sheria ya matumizi ya ardhi ya 1992.

Mhe. Spika, kifungu cha 2 cha sheria mama kinazungumzia tafsiri ya maneno mbali mbali ambayo yametumika katika sheria hii. Sasa tulizungumzia zaidi katika tafsiri ya neno, na kwa sababu sheria mama ipo katika Kiingereza, nitaisoma kama ilivyo kwa Kiingereza.

Tafsiri ya neno *natural land.* Mhe. Spika, ili ifahamike hoja yangu ningeomba tufanye marejeo katika kifungu cha 3 (1) cha sheria mama ambacho kinasema hivi na ninaomba kunukuu, *"All natural land within the Islands of Zanzibar, occupied or unoccupied, is hereby to declared to be public land and shall be deemed to have been so declared from 8th March 1964".*

Kifungu hiki kimetangaza ardhi yote ambayo imetajwa labda kwa Kiswahili ningesema ni ardhi *khaaliya*, *natural land* kwamba ni mali ya serikali, kikiegemeza msingi wake kutokana na tamko la tarehe 8 Machi, 1964 ambapo kama tunavyojua sote Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar katika kulitangazia taifa kwenye mkutano wake wa kwanza wa hadhara, aliitangaza hivyo kwamba ardhi yote ni mali ya serikali.

Sasa neno lililotumika la *natural land* katika kile kifungu cha 2 cha sheria mama nilichokitafsiri Mhe. Spika, kimetafsiriwa hivi *natural land means any land taken its natural state without man made improvements.*

Sasa katika mjadala wa Kamati na nadhani ndio maana limesahaulika tulimshauri Mhe. Waziri kwamba hii tafsiri ifanyiwe marekebisho madogo tu. Na hili Mhe. Spika, tulilipata baada ya kukutana na *stake holders*, wahusika mbali mbali ambao tuliwaalika kuja kutoa maoni katika Kamati. Palitoka hoja kwamba Zanzibar ina maeneo ya ardhi ambayo yamepatikana baada ya kazi ya kibinadamu ya kubadilisha eneo la bahari kulifanya eneo la ardhi.
Katika maeneo maarufu Mhe. Spika, ni pamoja na eneo lile la barabara tunaloita *Greek Road* iliyokuwa ikiigawa Mji Mkongwe asili na maeneo ya ng'ambu na ndio neno ng'ambu ilitokana na kwamba palikuwa na kivuko. Sasa ardhi ile kwa lugha ya kitaalamu ilikuwa *reclaimed*, ilijazwa katika pwani mbovu ilikuwa ikiitwa ikabadilishwa ikawa ni ardhi.

Na hivyo hivyo inatajwa maeneo kwa mfano ya Gulioni mkabala na eneo la Mpigaduri hivi sasa na pengine yapo na maeneo mengine ambayo mimi siyafahamu, lakini ninachotaka kusema hizi kwa lugha zilizotumika katika sheria ni *man made improvement*, yaani ni marekebisho yaliyofanywa na binadamu na sio *natural land*.

Sasa tulimwambia Mhe. Waziri kwamba ni vizuri katika tafsiri ya *natural land* kwamba akayaingiza yale kwa sababu ikibakia kama ilivyo sasa kwamba inasomeka *natural land means any land taken it's natural states without man*

made improvement, inaweza ikaja ikatafsiriwa vibaya ikaja ikayatoa maeneo yale. Kwa hivyo tulimuomba Mhe. Waziri hilo alitazame, nakumbuka tulikubaliana lakini bahati mbaya limesahaulika na hata katika maoni ya Kamati bahati mbaya naona sikuliona hapa, nadhani hapa hili limekuwa limesahaulika. Hilo moja Mhe. Spika.

Lakini la pili Mhe. Spika, ni hili ambalo amelizungumza Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Mhe. Mohammed Raza. Mhe. Mohammed Raza katika kuuchangia mswada huu kazungumzia kutaka kujua nilivyofahamu mimi au kujumuisha tafsiri hasa ya maeneo yote ya ardhi ambayo ni sehemu ya mamlaka ya Zanzibar. Na yeye amezungumzia makhsusi Kisiwa hiki cha Fungu Mbaraka ambacho kwa Kiingereza kinaitwa *Latham Island*.

Mhe. Spika, nadhani hoja ya maana kuzingatiwa na serikali sijui katika sheria hii au katika sheria nyenginezo, lakini katika sheria mama ya matumizi ya ardhi *Land Tenure Act* hakukutolewa tafsiri ya ardhi ya Zanzibar kwa ujumla wake, lakini inajulikana kwamba sheria zetu zinatafsiriwa kupitia moja ya sheria muhimu sana hapa ya *Interpretation of Laws Act*, sheria Na. 7 ya mwaka 1984.

Sasa Mhe. Spika, tukiisoma hapa katika sheria hii ya *Interpretation of laws Act No. 7* ya mwaka 1984, kwenye kifungu cha 4 ambacho kinazungumzia tafsiri ya maneno mbali mbali. Katika tafsiri hiyo Mhe. Spika, Zanzibar imetafsiriwa na inasema, *Zanzibar means the Island comprises Unguja and Pemba including their offshore islands, and when Zanzibar is used it is geographical sense means the territories formal comprises the People's Republic of Zanzibar*.

Nadhani katika Kiswahili vile vile imetafsiriwa kwamba Zanzibar maana yake ni visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyo katika bahari ya Zanzibar, na pale Zanzibar inapotumika kijiografia, maana yake ni yale maeneo ambayo kwa pamoja hapo zamani yalikuwa yakijulikana kuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Sasa Mhe.Spika, ukienda katika mtiririko wa historia wa Kikatiba katika nchi yetu, utakuta kwamba katika Katiba ya uhuru wa Zanzibar ya mwaka 1963, ilipotafsiriwa *the state of Zanzibar* imetaja kwa jina kwamba inajumuisha visiwa vya Unguja na Pemba na Kisiwa cha *Latham Island*, inataja hivyo mbali ya kwamba kuna ushahidi mwingi wa kihistoria ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwahi kututolea hapa ikionesha hivyo.

Kwa hivyo nilikuwa nadhani ni muhimu sana serikali kila inavyowezekana suala hili katika tafsiri likatajwa makhsusi hasa, kwa hivi sasa inaonekana

Tanganyika wana mpango wa kutaka kukipora kisiwa hiki na kukifanya kwamba ni sehemu yao, wakati ushahidi wote wa kihistoria unathibitisha vyenginevyo kwamba hiki ni mamlaka, ni sehemu ya milki ya Zanzibar.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba ni vizuri Mhe. Waziri hata ikiwa lipo katika nje ya mswada akija akatutolea ufafanuzi ili liendelee kuwekwa kwa usahihi kabisa nini msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo, sasa naomba nigusie masuala yangu mawili ya mwisho katika mswada ambayo ningependekeza haya kwenye siku zijazo Waziri ayazingatie katika sheria hii, ingawa hayamo katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza ninazungumzia kifungu cha 23 cha sheria mama. Hiki ningemuomba Mhe. Waziri kama tulivyomuomba katika Kamati na naomba niseme hapa ikae katika *record* kwamba hiki kuna haja ya kukitizama nacho katika marekebisho yatakayokuja baadae.

Mhe. Spika, kifungu cha 23 kimetoa madaraka kwa Waziri katika kutoa hiyo haki ya matumizi ya ardhi. Sasa katika michango tuliyoipata ambayo nadhani ni pahala pake kuwasilishwa hapa, tulipata hoja ni msingi sana kwamba huko nyuma katika marekebisho yaliwahi kufanyika yaliwahi kuondosha haki hii kutoka kwa Waziri ikapelekwa nadhani ilikuwa kwa Kamisheni ya Ardhi na Mazingira wakati huo.

Katika vipindi tofauti kumekuwa na mabadiliko baina ya kumpa aliyekuwa nadhani Mkurugenzi Mtendaji mpaka kuja kwa Katibu Mkuu, halafu hivi sasa imerudi kama ilivyokuwa awali kwa Waziri. Sasa hapa palikuwa na hoja Mhe. Spika, kwamba unapotoa haki ya kutoa haki ya matumizi ya ardhi kwa Waziri inaleta matatizo kwa watumiaji wengi kwa sababu anapotaka sasa kukata rufaa iwapo hakuridhika na maamuzi ya Waziri, ngazi inayobakia kiutawala inakuwa ni kwa Rais tu labda kwa kupitia kwa Makamu wa Pili wa Rais au Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mfumo wetu wa sasa.

Lakini kiilivyo kwa sababu aliyemteua Waziri ni Rais, kwa hivyo ngazi yake ya juu inaelekea kwa Rais moja kwa moja. Sasa wananchi walikuwa wanasema hii kidogo inaleta usumbufu, itakuwa tabu kwamba kila mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya mtu ambaye sheria imempa haki ya kutoa hiyo haki ya matumizi ya ardhi, kwamba asiporidhika moja kwa moja akate rufaa kwa Rais kabla ya kuchukua hatua nyengine za kisheria kwamba hili linaweza kupelekea kukawa na mlundikano ikiwa mambo yatakuwa ni mengi kama mambo yanavyoonekana hivi sasa kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi inaendelea kujitokeza kila siku. Kwa hivyo nilikuwa nasema hili nafikiri

serikali kwa ujumla Mhe. Waziri walitazame katika marekebisho ya siku zijazo.

Mhe. Spika, jengine ambalo litakuwa ni la mwisho na nataka kulitolea maoni nje ya mswada kwa kumuomba Mhe. Waziri pia siku zijazo alitazame ni kifungu cha 37 (1) cha sheria mama. Hiki Mhe. Spika, katika sheria kama ilivyokuwa imepitishwa mwaka 1992, kilikuwa kinazungumzia suala la ukodishwaji wa ardhi, kwa maana ya *lease* na kimetoa nafasi kwa kipindi ambacho kinaweza kufikia ukomo wa miaka 49.

Lakini baadae katika marekebisho ya sheria hii yaliyokuja kufanywa ikaondoshwa ikarejeshwa katika vipindi mbali mbali ambavyo vinafikia miaka 99. Sasa Mhe. Spika, uzoefu katika utekelezaji wa sheria hii umeonesha kuwa kuna malalamiko mengi sana ya wananchi, kwamba ukodishwaji wa ardhi kwa kipindi kirefu kama hiki unaweza usiwe na tija kwa wananchi.

Hoja iliyotumika ya kubadilisha na kupelekea miaka 99 ni kwamba mara nyingi wanaokodishwa wanatumia kwa shughuli za kibiashara na vyema na kama wanahitajika wapate muda wa kutosha wa kuweza kurejesha gharama zake na pia kupata faid, lakini Mhe. Spika, mimi nadhani hata tukitizama katika nchi za wenzetu, utaratibu unaotumika kwa sababu katika nchi nyengine huwa inawekwa miaka 11, 22 au 33. Sisi tukaja tukabadilisha tukasema 33, 66 au 99.

Sasa Mhe. Spika, mimi naamini kwamba biashara yoyote hata akipewa huo ukomo kwa maana ya kipindi *maximum* cha miaka 33, basi ana uwezo wa kurejesha gharama na pia kupata faida ya biashara yake. Na kama kuna haja ya nchi ikiona kwamba mradi ule una maslahi na nchi, na kuna haja ya kuendelea kumkodisha ile ardhi basi bila shaka kutakuwa na nafasi baada ya miaka 33 ikifika kuweza kufanya mapitio yale makubaliano au mkataba.
Lakini kumuwekea miaka 99 Mhe. Spika, wananchi wengi wana malalamiko kwamba hili linapelekea wale wote pengine walioshughulika na *transanction* ile au utaratibu ule wa kumkodisha watakuwa hawapo duniani, bila shaka nyaraka zipo lakini tunadhani kipindi hiki ni kirefu sana. Hivyo nilikuwa nataka kumuomba sana Mhe. Waziri na kupitia kwake kuiomba serikali kwamba katika marekebisho ambayo baadae watizame na zile kesi za mbele ni kuupitia upya tena kwamba jee kuna haja ya kuendelea na ukomo huo wa miaka 99 ambao ulirekebishwa kutoka hiyo miaka 49 ya awali iliyokuwemo katika sheria ile ya awali ya mwaka 1992.

Nadhani kuna haja serikali kuyatizama haya Mhe. Spika, kwa sababu haya ni malalamiko ambayo yanazungumzwa na wananchi wetu, yamezungumzwa na

washiriki mbali mbali ambao walikuja kutoa maoni mbele ya Kamati, nadhani ni muhimu kuyafikisha mbele ya chombo hiki ili serikali iyasikie na ione kwamba kuna haja ya kuyatizama kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu.
Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba nithibitishe tena maoni yaliyotolewa na Kamati niseme mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi ambao nawawakilisha naunga mkono hoja hii ya mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbali mbali za ardhi na mambo mengine yanayohusiana na hayo asilimia mia kwa mia.
Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana majadiliano yanaendelea. Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuzungumza machache kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu.
Mhe. Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi kabla sijaingia kwenye mchango wangu naomba niunge mkono marekebisho haya asilimia mia kwa mia, kwa sababu haya marekebisho yanaonekana kwamba yanaweza yakatusaidia sana wakwezi na wakulima ambao kwa miaka mingi sana ilikuwa hatumiliki ardhi. Sasa mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi napenda niipongeze serikali kwa kuweza kuuleta mswada huu.
Mhe. Spika, mimi nizungumzie hili aliloliacha Mhe. Ismail Jussa Ladhu la ardhi, hii ardhi khaaliya au *natural land*. Mhe. Spika, vyombo vyenye mamlaka ya kumilikisha ardhi vimekuwa ni tatizo sana. Kwa sababu sisi wakwezi na wakulima ambao tulikuwa hatumiliki ardhi mara baada ya kuzungumzia hii ardhi *khaaliya* kwamba ni mali ya serikali, tulikwenda katika maeneo haya ku-*establish* maisha yetu.

Kwa mfano Mhe. Spika, sisi katika Jimbo langu la Wawi kule tunategemea sana ardhi ya Makaani kwenye masuala ya kilimo, mifugo, kuanzisha viwanda vya kokoto pamoja na uchimbaji wa mawe. Hivi viwanda Mhe. Spika vinasaidia sana katika masuala ya kupata maisha yetu kule Vitongoji, Kibokoni, Uwandani na kadhalika katika Jimbo langu la Wawi.

Mhe. Spika, mamlaka zenye kumilikisha ardhi katika miaka ya karibuni imekuwa na tatizo, imekuwa ikiyatoa maeneo yale kwa wafanyabiashara ambao kwa kweli wameshindwa kuwaendeleza watu wa maeneo yale. Hili limekuwa ni tatizo kubwa lakini naamini kwamba sasa marekebisho haya yatatusaidia sana.

Mhe. Spika, kwa mfano mimi binafsi nimesoma, nimeoa na naendesha maisha yangu kupitia ardhi ile ya maweni. La kusikitisha ni kwamba hivi karibuni katika ardhi ya Makaani wamefidiwa watu wengi tu ardhi ile na kututaka sisi

wakulima wa pale, wafugaji, wavunjaji wa mawe, wenye viwanda vya kokoto vya pale tuondoke bila ya kupata msaada wowote. Hili ni tatizo Mhe. Spika, na mimi naomba kwamba hii mamlaka ambayo sheria ikishapita itamilikisha ardhi, basi iangalie sana wakaazi mwanzo wa pale na mahitaji yao.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna ugomvi mkubwa pale kwetu baina ya wafugaji, wachimbaji mawe, wabanjaji kokoto na baadhi ya wafanyabiashara pamoja na watu wa serikali ambao wamekwenda tu kukatiwa yale maeneo bila ya kuyaendeleza pale. Wanawataka wasichimbe yale mawe ambayo ndio maisha yao, wasifuge tena ambao ndio maisha yao, wanataka wasifanye tena shughuli za kimaisha pale ambapo wao yanakwenda pale, huku wao ikiwa ardhi ile wameshakatiwa, wameshapimiwa bila ya kuiendeleza.

Sasa Mhe. Spika, katika hili hii sheria, mabadiliko haya naomba sana kwenye maeneo kama yale yanayomilikiwa na sio kumilikiwa lakini wanayokaliwa na wakulima na wakwezi wa nchi hii tangu mwaka 1964 hadi hii leo, basi kwanza waangaliwe wale wanyonge ndipo ikiwa pana mfanyabiashara aje pale. Kwa sababu pale petu Mhe. Spika, hakuna karafuu, Mzee Karume alikata eka tatu tatu kwa wenye mashamba sehemu za Kusini, sisi ardhi yetu ni maweni tu. Kwa hivyo kule sisi hatukupata eka lakini tukaenda maweni kulima, kufuga, kuchimba kokoto, pamoja na mawe.

Sasa maeneo yale naomba sana wale ambao maana ukienda wanasema hawajapewa hati miliki, lakini wapo mbioni kutengenezewa, huku wakulima na wafugaji wakinyanyasika. Mimi nadhani Mhe. Spika, sheria hii itakapopita mamlaka yenye kumilikisha ardhi basi ihakikishe kwamba watu wa maeneo ya Kibokoni, kwa mfano kule jamaa kaenda anasema mimi nachukua hapa, kwa sababu mimi kama ndio kama chama tawala hapa, mimi ndio mwenye serikali hapa, lazima nichukue hii ardhi, akawaondosha watu. Lakini watu wakakazana na nashukuru kwamba watu wale baada ya kukazana sana wanaendelea kufanya shughuli zao katika maeneo ya Makoba na maeneo kadhaa ya eneo la Vitongoji.

Kwa hivyo naiomba serikali katika hili ukipita mswada huu ukatiwa saini na Mhe. Rais, basi kabla ya kuangalia lolote waangaliwe hawa wanyonge ambao tangu mwaka 1964 hadi leo hii wanaendelea na maisha yao pale.

Sasa Mhe. Spika, niende kwenye eneo jengine. Eneo jengine ni kwenye marekebisho haya ya kifungu cha 8 ambacho kimefuta hii (b) na (c) na kuweka (d) na (c). Sasa katika kifungu cha (c) hapa nashukuru kwamba hawa Mzanzibari yeyote ambaye ana sifa ya kuwa ni Mzanzibari na kupoteza sifa hizo atakuwa na haki za kuweza kurithi na kuweza kupata ardhi.

Sasa Mhe. Spika, mimi naona pana tatizo kidogo, Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba atuwekee sawa. Kuna chotara wa Kinyamwezi na Kipemba anaitwa Kurwa Shauri, alihamishwa hapa asikaribie Zanzibar, ndugu yangu Kurwa Shauri, alihamishwa na awamu moja ya uongozi wa Zanzibar, kwamba asikaribie hasa Zanzibar Kurwa Shauri na wana ardhi yao pale Kichungwani na wana ardhi yao Vitongoji.

Kwa hivyo, mtu kama Kurwa Shauri ataingiaje hapa kuja kupata ardhi wakati kuna *presidential statement* ya kwamba asikanyage ardhi ya Zanzibar. Je, watu wa namna hii Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba, itakuwaje watu wa namna hii kina Kurwa Shauri. Aidha, kuna wale wengine ambao walikuwa ni raia wa Kisultani katika miaka ya nyuma. Mara baada ya mapinduzi raia wa Kisultani wote akina Mzee Shamte Hamad, Al Shirazi na wenzao walikuwa ni raia wa serikali ya watu wa Zanzibar. Sasa watu kama hawa wakija kurudi wengine bado wanaogopa.

Je Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba wewe unasemaje katika hili? Waliondoka wale wengine watoto wa Muhamad Shamte bin Hamad Al Shirazi, waliondoka pale Chambani wakaenda katika sehemu nyengine, je hawa wakija kurithi mashamba yao ya Shamte Hamad pale, vipi hawatokuja kupata tatizo, sheria hii haitokuja kuwatia watu matatizoni baadae? Suala hili nataka uje kunipa ufafanuzi. Kwa sababu Mhe. Spika, huu mswada wenyewe sio mrefu na kwa sababu mswada wenyewe ni mzuri, basi naendelea kuungana na wapiga kura wangu kuunga mkono huu mswada, na uangalie usimilikishe tu ardhi kwa matajiri, halafu wakawaachia wale watu wa Vitongoji pale Umangani, Kibokoni, Uwandani, wakiwanyang'anya yale maeneo wanayochimba mawe basi sheria iwaangalie vizuri, na iwape kipaumbele katika suala hili, na mwisho Mhe. Abubakar atujulishe hapa kwamba akirudi kuwashauri pamoja na wale baadhi ya Kisultani walioondoka baada ya Mapinduzi, akina Mzee Muhamad Shamte hawatokuja kupata tatizo wakija kurithi mashamba yao? Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima wa afya na kuweza kutufikisha kwa mara nyengine tena ndani ya Baraza lako tukufu tukiwa na idadi ile ile tuliyoondokea katika kipindi kilichopita, ikiwa ni Rehema yake mwenyewe Allah.

Mhe. Spika, pia nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kusema machache sana ili tu kuongeza ubora na kutoa wasi wasi wa mswada uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, mimi niseme naunga mkono kwanza sheria hii ya mabadiliko, kwa namna ambayo serikali imeona haja ya kufanya jambo hili ambalo sasa hivi kwa ujumla wetu Tanzania nzima, suala la ardhi ni tatizo

kubwa na ni zito, linaleta tafrani ndani ya jamii na kupoteza hata maisha ya wenzetu. Kwa hivyo, niipongeze sana serikali pamoja na Mhe. Waziri kwa kuona umuhimu wa kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, nimesema nitakuwa na machache, nilikuwa nataka tu kupata ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kwa kifungu cha 4(b)(c)(i). Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 8 kwenye mswada huu, iko kifungu hicho hicho cha 4(c)(i), kwa idhini yako nikisome;

Kifungu cha 4(c)(i)

"Mzanzibari 'yoyote' ambapo ilipaswa iwe 'yeyote' 'ambaye' sio 'ambae' alikuwa ana sifa ya kuwa Mzanzibari na akapoteza sifa hizo atakuwa na haki zifuatazo. Sasa hiyo *norminal* namba moja ndipo ninapotaka kupata ufafanuzi. Haki zifuatazo,

1. Kurithi ardhi iliyokuwa inamilikiwa na mtu ambaye alikuwa ana haki ya kisheria kumrithi. Haki ya kisheria, hapa inazungumziwa mirathi ya dini. Nakusudia dini ya Kiislamu, haki hii ndio inayokudusiwa ama ni mirathi hii ya kidunia, mirathi ya kidunia Mhe. Spika, kuna namna tunashuhudia sasa hivi mwanamme anakwenda kuoa ndani ya ndoa hiyo akapata mali na ikafika muda Mwenyezi Mungu akamuhitaji huyu mume. Kwa upande wa dini ya Kiislamu anarithiwa na mke wake, lakini kuna upande mwengine wa mirathi inaambiwa kwamba kile alichokichuma wakati ule yule mke anaye na huyu mke anakuwa na haki ya mali ile, kwa maana ya sawa kwa sawa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba uje utuwekee sawa hili, kuhusu hiyo haki ya kisheria ni ya kisheria ipi hapa iliyokusudiwa.

Jengine Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliotangulia wengine wamelizungumzia kwa mapana yake, lakini kwa umuhimu unaostahiki nasema kwamba suala la ardhi ni suala nyeti sana, na serikali nasema naipongeza kwa kuleta mswada huu. Tunaamini utaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa haya yanayojiri.

Mhe. Spika, uzoefu wetu tatizo huwa sio sheria. Zanzibar kwanza kuna wanasheria Alhamdulillah waliobobea na wanafanya kazi vizuri. Tatizo linalotukuta ni utekelezaji wa sheria yenyewe. Mhe. Spika, utekelezaji wa sheria zetu ndio unaotupa matatizo.

Wenzetu Tanzania Bara hapo au Tanganyika yanatokea maafa makubwa sasa hivi kwa sababu ya tatizo la ardhi. Lakini Waswahili wanasema *ukimuona mwenzio ananyolewa, wewe tia maji*, lakini kuna ile pia watoto nyoka yuwaja, hapo karibu tu hapo. Nadhani sasa wakati umefika serikali imeona haja ya

kuleta sheria hii na wenzetu watendaji, watekelezaji wa sheria zetu na wao wabadilike ili kuepusha hayo ninayoyasema kwamba yasije yakatutokea hapa.

Mhe. Spika, kwanza niiombe serikali, mimi nadhani inafahamu umuhimu wa wananchi wake na kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii mamlaka ya nchi ni wananchi na wala sio serikali, wala sio chama fulani, wananchi ndio wenye mamlaka ya nchi yao, na nchi yao ni Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu hapa kataja kwamba tarehe 8 Machi, 1964 Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Sheikh Abeid Aman Karume aliitangaza ardhi kuwa ni mali ya serikali. Sheria hiyo ipo ikawekwa vizuri. Yeye kwa makusudi kabisa alifanya hivyo ili wenye mamlaka na nchi yao waweze kufaidika na ardhi yao hii. Kuna wale waliokuwa na ardhi kubwa na wengine hawana kabisa.

Mhe. Rais wa Kwanza alitengeneza utaratibu ili na wale wasiokuwa nayo na wao wawe nayo, kazi nzuri aliifanya Marehemu Rais wetu wa Kwanza. Matatizo yamekuja hapa katikati ya utekelezwaji wa hizi sheria ninazozisema. Kwa makusudi alizigawa zile eka tatu tatu, lakini alipozigawa eka zile aliyegaiwa hakuwa na ruhusa ya kuuza, kama hana pa kuishi basi aishi ndani ya ardhi ile aliyopewa aitumie kwa kuzalisha ili aweze kuishi. Ni imani yangu vurugu hili lililotokea hapa katikati la matumizi mabaya ya ardhi zile huenda sasa yakawa ni kikomo.

Mhe. Spika, tatizo linaanza wapi? Tatizo linaanza pale ambapo anafanya makosa mtendaji, hao wenzetu tunaowapa dhamana za kusimamia hili kutoka ngazi za chini hadi kule juu na tunashuhudia huyu ndiye mkosaji, lakini tunaoneana haya, tunastiriana pasipokuwa na ulazima, na tunaruhusu maovu yatendeke. Eka hizi tatu tatu hata wale ambao wenyewe sasa ni marehemu Masheha ni zao wao, wanauza wanavyotaka, wanagawa wanavyopenda alimradi ni vurugu. Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba ile dhana Mhe. Waziri ya Marehemu Rais wa Kwanza, sasa hivi itarudi pale alipokusudia yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, jengine ambalo kwa sasa hivi linatupasua vichwa vyetu, tukipata maswali tunashindwa kuyajibu kwa wananchi wetu ni suala zima la Kisiwa hiki maarufu cha Fungu Mbaraka. Serikali kwa sababu ni dhamana mpaka na mali za wananchi wake, Fungu Mbaraka ikiwa ni miongoni mwa mali za Wazanzibari wenzetu wanasema kisiwa ni chao, sisi tunasema ni chetu. Sisi tunasema ni chetu kihistoria tunayapata maelezo kwa wenzetu Kijiografia ni Kijiolojia. Fungu Mbaraka ni sehemu ya Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vidogo vidogo vilivyoizunguka Zanzibar. Hebu Mhe. Waziri kwa heshima kubwa na busara unayoaminika kwamba unayo na ni kweli unayo, hebu

waweke pazuri Wazanzibari kisiwa hiki cha Fungu Mbaraka ni mali ya Wazanzibari kama tunavyoamini au ni mali ya wenzetu wa Tanganyika, tuwekee wazi tufahamu hilo, na kwa nini wao waseme ni mali yao ilhali kwamba sio mali yao.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hili kwa sababu ninavyoamini mimi Asaa kwamba mirathi baada ya wazazi au mzazi kuondoka ulimwenguni basi ni haki ya watoto kama wapo, na kama hawapo basi kuna warathi waliotajwa Mwenyezi Mungu amewataja kwenye Qurani yake tukufu, wapi ni kina nani watarithi. Sasa hakuna aibu wala sio dhambi, wala hakuna sababu ya ugomvi changu kupewa mwenyewe au kukidai. Kwa hivyo, isije ikafikia mahali ikawa yule anayepigia kelele ya madai ilhali hakimuhusu sio chake, basi ikaonekana ndiye mwenye haki kwa sababu sisi tulio wenyewe tumenyamaza kimya hatusemi.

Mhe. Spika, mimi katika hili namuomba mzee wangu atakapokuja kutoa majibu ya jumla basi apate muda muafaka ili atuwekee vizuri hoja hii.

Mhe. Spika, la mwisho kwa leo. Tuna tatizo jengine, wazee wetu wengine hawakuwa na hati za umilikaji wa mashamba yao, hivi sasa kizazi pengine mpaka cha zaidi ya kumi na wao wanakwenda hivyo hivyo, ni ile kijijini inajulikana kuwa shamba hili lilikuwa ni la Mzee Bakari, shamba hili lilikuwa ni la Bi Time, watoto wake ndio warathi inakwenda hivyo kwa ushahidi huo, lakini kimaandiko hapana hayo maandiko. Kwa bahati mbaya mengine yamepotea, sasa ni utaratibu upi serikali itafanya ili watu kama hawa au Wazanzibari kama hawa waweze kupata umiliki wa mashamba yao bila ya kuwa na usumbufu, na kama tujuavyo kesho na keshokutwa waweze kutumia ardhi zao hizi kupata mahitaji ya kimsingi kuendesha maisha yao katika vyombo husika, haya yale maeneo ya vyombo vya kifedha. Leo bila ya kuwa na hati inayokubalika kwa kusema tu nakwenda wapi basi itakuwa haki hiyo ataweza kuikosa.

Mhe. Spika, kwa ujumla mswada ni mzuri, nia ya serikali ni nzuri, kwa hivyo nawaomba na watekelezaji wa sheria na wao waende sambamba na maudhui yaliyokusudiwa. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii ahsante.

Mhe.Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kusema maneno mawili matatu maana yake mswada wenyewe una karatasi mbili. Lakini sio kwamba una karatasi mbili tuudharau, una mambo mazito sana na kwa msingi huo ndio nikasema angalau niweze kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na marekebisho ya kifungu cha 56 cha sheria mama, nataka nianze hapa kwa sababu siku zote nilikuwa na mawazo kuhusiana na thamani ya ardhi na nilikuwa natamani siku moja serikali waweke utaratibu mpya wa kulipa fidia kwa ardhi, kwa sababu kama tunavyojua serikali yenyewe inagawa ardhi kwa wananchi kwa ajili ya majenzi, na kwa kawaida wanakuwa hawauzi isipokuwa wanamtolesha mtu ada ndogo labda ile *labour charge* ambayo watu wa ardhi wanakwenda kupima na kutayarisha nyaraka na mambo mengine, lakini ardhi walikuwa wanaekewa bure.

Mhe. Spika, kutokana na wakati ulivyo sasa hivi ardhi ina thamani kubwa, kwa sababu inawezekana mtu akapewa kiwanja na serikali kwa shilingi 200,000 au 300,000, maana yake kama kapewa bure isipokuwa analipia zile gharama za kutengeneza kile kiwanja mpaka kikawa. Lakini ile shilingi 200,000 sio thamani ya ile ardhi yenyewe, thamani ya ardhi ni kubwa sana na inaonekana ni kubwa pale ambapo yule aliyepewa mipango yake ikimuendea vibaya akashindwa kujenga akataka kuiuza basi hatakiuza kwa shilingi 200,000 atakiuza kwa pesa nyingi sana. Kwa hivyo, zile pesa atakazouzia na mnunuaji akaridhika kununua kwa pesa zile, pengine shilingi milioni 20 au 25, ile ndio thamani ya ardhi kwa wakati huu.

Mhe. Spika, sasa mimi nilikuwa napata tabu kwamba mtu kanunua ardhi kwa thamani hiyo, lakini leo serikali ikahitaji kuitumia ile ardhi kwa maendeleo ya wananchi na ikatokea bahati yule aliyenunua kwa thamani hiyo, hajafanya maendeleo yoyote kwenye ile ardhi, maana yake hajajenga, hajapanda wala hajafanya chochote, na serikali wakawa na ule msimamo kwamba wao wanalipia yale maendeleo yaliyofanywa juu ya ile ardhi, lakini ile ardhi binafsi hawalipii ni mali ya serikali. Mimi nasema hapa kuna aina fulani ya matatizo.

Kwa hivyo, nadhani mtu akilipwa fidia alipwe fidia kwa thamani ya ile ardhi, na pengine kile kilichoendelezwa pale juu ya ardhi ni kitu kidogo sana. Nashukuru sana kifungu hiki, kama nitakuwa nimekifahamu vizuri, ukisoma hicho kifungu cha 5 ambacho kinarekebisha kifungu cha 56 kumeongezwa aya pale ya (c) na (b) kwa kulipa fidia yenye kuridhisha, ambapo Kamati ilisema tusiandike yenye kuridhisha, lakini tuandike fidia yenye kulingana na soko kama hivi, niliona pahala imeandikwa kwenye ripoti ya Kamati. Mimi nakubaliana na marekebisho yale kwamba tuseme kama ni fidia itakayolingana na soko la sasa la ardhi, sasa hii kidogo itaridhisha watu Mhe. Spika, kwa sababu leo mtu ananunua ardhi yake kwa shilingi milioni 20 au 30 hajawahi kujenga, halafu serikali inapitisha barabara pale, wakitaka kumlipa fidia wanamuuliza umepanda nini hapa juu ya ardhi au umejenga nini, haa! Sijajenga kitu, wanasema basi ni bure. Sasa pesa za mtu zinapotea bure, lakini

pengine kwa vifungu hivi sasa mtu atarejeshewa kile chake alichokitoa kwa ajili ya kununua ile ardhi. Kwa hivyo, hapo mimi niipongeze serikali kwa suala hili.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo kwa kweli mimi nitaendelea kulilalamikia sana katika matumizi ya ardhi. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana serikali bado mpaka leo haijaweza kusimamia vizuri masuala ya majenzi ya nyumba. Tuna Sera ya Ardhi tuliipitisha hapa, lakini inaonekana bado usimamizi wake haujawa makini sana, kwa sababu mpaka leo Mhe. Spika, ndani ya nchi yetu, tena nchi ndogo kama hii majenzi holela yanaendelea. Mtu tu anaamua nina shamba langu Mwera sijui wapi huko, ameamua kulikata viwanja akauza mwenyewe, lakini bila ya kupata ushauri kutoka serikalini.

Kwa hivyo, mimi nadhani hii sheria ya matumizi ya ardhi ingeweka kifungu maalum. Mtu ardhi yake mwenyewe, lakini akiamua kuuza hasa kwa viwanja vya nyumba. Maana yake kama anaamua kumuuzia mtu afanye konde ni jambo jengine, lakini kama anaamua kukata viwanja kwa ajili ya majenzi basi kwanza asiruhusiwe kufanya hivyo mpaka awasiliane na serikali, serikali itoe wapimaji waende wakapime viwanja pale ili hicho kitakachojengwa hapo basi kiwe kinatoa huduma zote, kwa sababu wanamokaa watu panahitajika pafike barabara, umeme, maji na kadhalika ni mambo ambayo watu wanayahitaji kila siku, lakini mtu anakata viwanja watu wanajenga kama vile yale majumba ya kule Kojani. Samahani Mhe. Hassan Hamad Omar, hayumo.

Kule Kojani Mhe. Spika, ukifukuzwa kama ni mgeni huwezi kutoka kwenye ule mji, ukienda huku utagongana na ukuta, ukienda huku utagongana na ukuta. Kwa hivyo na sisi tusijenge kama vile, tujenge lakini turuhusu huduma zipite mule ndani ya mji ambamo binadamu anakaa mule. Kuna ugonjwa, mgonjwa anataka kuchukuliwa kwa gari na gari haipiti inabidi abebwe kwa machela, sio jambo zuri. Kwa hivyo, mpaka leo nasema katika suala hili bado serikali haijalisimamia vizuri, naomba sana Mhe. Waziri suala hili alichukue ili ikiwezekana sheria hasa itungwe mtu asiruhusiwe kugawa viwanja vya shamba lake mwenyewe mpaka kwanza azungumze na watu wa ardhi.

Jambo jengine Mhe. Spika, hata pale palipopimwa kwa sheria kabisa watu wakapewa viwanja na kila mtu akapewa namba ya kiwanja chake, akaoneshwa *beacon* zake, lakini matatizo yanatokea watu wanajaribu kuvunja sheria. Mtu zile *beacon* zilizowekwa na serikali anazing'oa halafu anaweka zake na mara nyingi kumekuwa na migogoro ya ardhi kwa sababu hiyo. Nataka nimwambie Mhe. Waziri hata kule mji mpya kule Tunguu, sasa hivi utaratibu huo unafanywa, mtu anaona lile butu lote la ardhi alilopewa halikumtosha anang'oa *beacon* ya mwenzake anasogeza. Kwa hivyo, nawaomba watu wa ardhi wawe wakali sana katika hilo, kwa sababu

watasababisha migogoro iliyokuwa haiishi kila siku na vinajulikana kwa sababu *beacon* ya serikali wale wataalamu wa ardhi wanakuwa mafundi kiasi ambacho hata uking'oa *beacon* wewe ukajenga nyumba pale katikati ya ukuta basi watakwambia *beacon* yetu imepita chini ya ukuta huu, wanapajua wenyewe. Kwa hivyo ni jambo la usimamizi tu.

Mhe. Spika, Sasa mimi nadhani kuondoa migogoro ya ardhi Mhe. Spika, basi ni muhimu serikali ikasimamia kwa karibu sana.

Jambo la mwisho kama nilivyosema kwamba mswada huu ni mdogo sana na wala hauna mambo mengi ya kusema. Mhe. Spika, bado naendelea kulalamika vile vile kwamba ardhi yetu Wazanzibari ni ndogo sana, na Wazanzibari wanahitaji ardhi hiyo kwa ajili ya makaazi na wakati huo huo wanahitaji ardhi hiyo kwa kilimo.

Sasa mpaka leo bado tunaendelea kufanya majenzi katika ardhi ambayo inatusaidia zaidi katika kilimo. Kwa mfano, kuna ukanda ule wa Makaani ambako kuna uwanda mkubwa kweli haufai kwa kilimo lakini bado hatujaupangia matumizi ya majenzi kule na kuiachia ardhi ya kilimo ifae kwa ajili ya kilimo.

Kutokana na hali hiyo, itafika siku Mhe. Spika kwamba Wazanzibari watashindwa pahala pa kupanda hata mboga sehemu zote itakuwa zimeshajengwa. Kwa hivyo, nadhani serikali iweke mkazo sana kuelekea kule ambako hayakui mazao ya kilimo na ardhi hiyo tunayo kubwa ya kutosha na tuiache ardhi ya kilimo ifae kwa ajili ya kilimo.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, mimi sina matatizo na mswada huu na nauunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau nikaweza kutumia kama dakika tano mpaka kumi juu ya mswada huu, ambao Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ametuwasilishia wenye kuzungumzia juu ya marekebisho mbali mbali yanayohusiana na ardhi.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kufikia kuleta mswada huu wa sheria, ambao umerekebisha baadhi ya vifungu vya sheria hizi zilizopita. Kwa kweli mswada huu unakusudia kurekebisha Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992 na Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam. 10 ya mwaka 1990.

Mhe. Spika, suala la kufanya marekebisho ya sheria ni muhimu, pale ambapo tunahisi baadhi ya vifungu haviendi sawa kulingana na wakati, kwa sababu

tukiangalia kwa mfano Mswada huu wa Sheria Nam. 12 wa mwaka 1992 una karibu miaka 11 hivi na huu wa Sheria ya Ardhi wa mwaka 1990 nao umezidi.

Kwa hivyo, ni muda mkubwa pengine vifungu hivi vya sheria vilikuwa viko sawa na vilikuwa vinaendana na wakati ule, lakini hivi sasa vimeonekana kwamba havihitajiki au vinahitaji kufanyiwa marekebisho kutokana na utaratibu na mabadiliko mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi huwa napendelea kusema kwamba wenzetu wanapotuletea miswada hii hasa inayohusu marekebisho ya mambo mbali mbali, basi wawe wanatuletea marekebisho ya zile sheria zilizopo na namna ya sheria nyengine zinavyosema, ili kutuwezesha sisi kuweza kufahamu kwa urahisi.

Kwa kweli jambo hili litawasaidia sana Waheshimiwa Mawaziri au serikali kwa jumla, ili kujua au kufahamu zaidi. Kwa mfano, kama unavyojua Mhe. Spika, kwamba bado tunayo nafasi ya kuifuatilia miswada hiyo lakini Wajumbe wako tunakuwa na shughuli nyingi tukishaipitisha sheria hapa maana yake ndio tumeshaipitisha.

Kwa maana hiyo, ni jukumu na wajibu wa Mhe. Waziri anayehusika kuturahisishia, ili tuone yale marekebisho yaliopo ama kuyafanyia masahihisho au kuyakubali na kuyaunga mkono kwa urahisi, lakini vyenginevyo tutakuwa tunakwenda giza na wala hatuoni ndani. Kutokana na hali hiyo, mara nyingi huwa ninapendelea hivyo na ninasema kwamba wawe wanatuletea *notice* zile ambazo zitatusaidia kutupa uelewa juu ya kile kinachoendelea.

Mhe. Spika, suala la ardhi ni jambo zito sana popote pale tena ni suala ambalo limekuwa na mizozo mikubwa na hii si kwa hapa kwetu tu Zanzibar, lakini karibu maeneo mengi au nchi nyingi. Matatizo haya yanakuwa mengi zaidi pale ambapo ama sheria zilizopo zina kasoro au udhaifu ama sheria zenyewe utekelezaji wake au vile vyombo vilivyopewa mamlaka ya kusimamia zile sheria basi hazifanyi wajibu wake ipasavyo. Kwa hivyo, katika eneo hili matatizo sasa yanakuwa makubwa zaidi.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika nimuombe sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia kwako, kwamba ajaribu kwa kadri ya uwezo wake kuhakikisha zile sheria zilizopo zinatekelezwa, ili kupunguza angalau matatizo katika maeneo ya ardhi.

Vile vile hata zile sheria ambazo zinapishana au vifungu ambavyo havikidhi mahitaji yaliopo, basi navyo vifanyiwe masahihisho. Kwa kweli mimi naamini kwamba kuna maeneo mengi mbali ya haya ambayo Mhe. Waziri ameyaona kwa ghafla, lakini kuna maeneo mengi yanayohusiana na masuala ya ardhi bado yanahitaji kufanyiwa marekebisho, kwa ajili ya kupunguza manung'uniko ambayo si ya lazima kwa wananchi.

Mhe. Spika, nadhani utakuwa unakumbuka wakati ule Rais wa Awamu ya Tatu wa Zanzibar Mzee wetu Mhe. Ali Hassan Mwinyi alipokuwa Rais wa Zanzibar, alijaribu kuanzisha utaratibu wa wananchi kwenda pale Afisi Kuu ya CCM kwa ajili ya kuonana naye na kupeleka malalamiko yao mbali mbali, lakini wananchi wengi waliofika pale zaidi ya asilimia 90 walikuwa wanawasilisha malalamiko ya ardhi katika muda wake wote.

Hali hii inaonesha kwamba matatizo ya ardhi yamekuwa makubwa mno, kwa wakati ule Mhe. Rais alikuwa anapata nafasi ya kuyasikiliza, lakini sijui kama alipata nafasi ya kuyasikiliza na kuyatatua kwa wakati ule, kwa sababu yalikuwa ni mengi, lakini pengine aliyoweza kuyatatua ameyatatua, na yale yaliyokuwa yamebakia alishindwa kuyatatua basi pengine bado yanaendelea kuwa ni matatizo na kila siku yanaendelea.

Mhe. Spika, si hivyo tu hata Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein amekuwa akipokea malalamiko mengi yanayohusu masuala ya ardhi na sote ni mashahidi, na wakati mwengine amekuwa na lugha anazitumia kwamba walioleta matatizo ya ardhi watayamaliza wenyewe, hizi ni *terms* ambazo amekuwa akizitumia. Kwa kweli hapa inaonesha ni aina gani ya uzito wa matatizo ya ardhi kwa hapa kwetu Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika suala la matatizo ya ardhi bado inaonekana ni tatizo sugu ambalo linahitaji kusimamiwa kwa umakini zaidi na watendaji hasa wanaohusika na masuala ya ardhi wana wajibu wa kuhakikisha sheria zile wanazisimamia ipasavyo.

Kwa maana hiyo, eneo hili ni eneo kubwa, yaani ni eneo ambalo lina vishawishi vikubwa sana vya rushwa. Mhe. Spika, katika eneo ambalo lina vishawishi vikubwa ni eneo la ardhi, kwa sababu ardhi ndio kila kitu. Kwa hiyo, wenzetu hawa wajitahidi pamoja na ubinadamu waliokuwa nao, basi wajitahidi kadri ya uwezo wao kuona kwamba vishawishi hivi vinakuwa pembeni, ili kuondosha matatizo haya.

Mhe. Spika, juu ya ukubwa wa matatizo ya ardhi hata Baraza lako tukufu limethubutu kuunda Kamati Teule kuhusiana na masuala ya ardhi, Kamati ambayo imeshachukua muda mkubwa na mpaka leo ripoti yao wameshindwa

kuiwasilisha hapa Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli hali hiyo, inaonesha kwamba suala la ardhi ni zito, kwamba kamati tumeiunda na imeshachukua muda mkubwa na hadi leo Kamati ile haijaweza kuwasilisha ripoti yake hapa, sasa sijui kuna nini.

Kwa maana hiyo, hili linaonesha kwamba suala la ardhi bado ni tatizo, kwa sababu hata Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wanashindwa kufanya zile shughuli ambazo tumewakabidhi.

Mhe. Spika, katika mswada wa Mhe. Waziri hapa kuna jambo ambalo amelizungumzia, ambapo nadhani wakati atakapokuja kufanya majumuisho naomba kupatiwa ufafanuzi kwa ruhusa yako, na naomba kidogo ninukuu kwenye eneo la Madhumuni na Sababu.

Sehemu ya Madhumuni na Sababu inaeleza hivi:-

> "Lengo la marekebisho haya ni kuweka tofauti ya fidia baina ya wale waliopewa haki ya matumizi kwa kununua, kurithi au hiba na wale ambao wamepata kutoka Serikalini, kwa wale ambao wamepewa haki hiyo na Serikali kwa kuwalipa ada ndogo tu, ambapo serikali itahitaji eneo husika kwa matumizi mengineyo, Serikali iweze kulichukua eneo hilo kwa kumpa eneo jengine mbadala pamoja na kumlipa fidia ya maendeleo yaliyofanyika au kumlipa fidia stahiki kwa ardhi hiyo pamoja na maendelezo yaliyofanyika".

Mhe. Spika, nahitaji ufafanuzi zaidi na kwa sababu ardhi yetu hii imegawika katika maeneo tofauti kwenye matumizi. Kwanza tumekubaliana kwamba ardhi ni mali ya serikali baada ya Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964; kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Jemedari wetu Mzee Abeid Amani Karume ilitangaza kwamba ardhi yote ni mali ya serikali.

Kwa maana hiyo, kuna ardhi ambazo zilikuwa ziko wazi hazimilikiwi na mtu, pia kulikuwa na maeneo ambayo tayari kuna wananchi wenyewe walikuwa wanamiliki ama walimilikishwa na Serikali ya Ukoloni kwa wakati ule au ni ardhi ambazo wamiliki wake walimiliki kutokana na urithi wa maeneo yale, yaani kulikuwa na aina nyingi za umiliki wa maeneo yale.

Kwa kweli wengi Mhe. Spika wale waliomilikishwa ama kwa kurithi kutokana na familia zao walikuwa hawana hati miliki, lakini ni wamiliki ambao katika familia zao au kwenye uzawa wao wameona tu maeneo yale ni

yao mengine yamepandwa miti na mengine hayajapandwa miti ni mapori na mengine yapo tu tambarare tu kama vile maeneo ya mawe na mengine, lakini wenyewe wananchi wa pale wanajua kwamba haya ni maeneo yetu ya ardhi ambayo tumerithi kutoka kwa wazee wetu.

Kwa hivyo, yote ni maeneo ya ardhi ambayo tunayo lakini serikali ikasema kwamba kuanzia leo ardhi ni mali ya serikali, na hii ni tofauti na nchi nyengine. Kwa mfano, Kenya ardhi si mali ya serikali na kila mtu mwenye pale ndio mali yake, isipokuwa sisi tumeweka ardhi ni mali ya serikali.

Sasa inawezekana Mhe. Spika, ikawa serikali inataka kufanya maendeleo katika eneo ambalo halina kitu ni eneo tupu ambalo bado halijamilikishwa na hiyo inakuwa hakuna matatizo.

Lakini pengine serikali inaweza kutaka kufanya maendeleo katika eneo ambalo linamilikiwa na wenyewe wananchi wa pale na wananchi wao hawana hati miliki isipokuwa eneo lao ni la urithi ambalo wanalitumia wao, ambapo wamelirithi kutoka kwa wazazi wao na wao wanao watoto wao wenye kulitegemea eneo lile, na pengine wameliendeleza kama vile wamepanda miti na mambo mengine.

Mhe. Spika, namna ya ufidiaji ambao Mhe. Waziri ameueleza hapa katika maeneo kama haya ukoje na anakusudia kufanya nini. Vile vile kuna maeneo ambayo serikali yenyewe imemmilikisha mwananchi katika eneo lile na mwananchi akaanza kulitumia eneo lile lakini amepewa na serikali.

Sasa hizi ada ndogo ndogo ambazo Mhe. Waziri anasema kwamba sheria hii inakusudia kuwalipa ada ndogo ndogo vipi, yaani ni eneo ambalo ameomba kwa serikali na amepewa na serikali, basi hiyo fidia anayoizungumzia hapa Mhe. Waziri ambayo ni fidia ndogo ndogo inakusudia nini? Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje atueleze lipi hasa linalokusudiwa.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu hapa ni kwamba umiliki ni umiliki ukishammilikisha mtu pengine ameshapanda miti na ameshajenga nyumba. Sasa unaposema kwamba eneo hili ada zake zitakuwa ndogo ndogo, mimi nadhani bado madhumuni ya sheria hii hayatakuwa mazuri kama ni hivyo, lakini pengine nimeelewa tofauti.

Katika hatua kama hizi ya masuala ya ardhi juu ya ardhi ya aina hiyo nayo kumekuwa na malalamiko. Kwa mfano, kuna mwananchi mmoja alikuja kunilalamikia ambapo alipewa ardhi muda mkubwa sana na serikali, na ardhi ile tayari ameshaiendeleza, yaani tayari ameshajenga ukuta wa kuiendeleza

kwa lengo lile ambalo amekusudiwa kupewa, lakini baada ya muda mkubwa serikali ikaja ikapima sehemu ya eneo lile kwa ajili ya maendeleo ya eneo lile.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha kwamba mbali ya lile eneo jengine ambalo limepimwa na serikali kwa ajili ya kuliendeleza na serikali sasa na lile eneo ambalo alipewa kabla hata ya uwekezaji ule nalo sasa anaambiwa aondoke hapa, kwa sababu serikali inataka kuendeleza.

Ah! Mhe. Spika, bado taratibu hizi za kiserikali juu ya wananchi wake zinaonekana zinaleta mashaka, kwamba yeye yupo pale kwa muda mrefu kabla ya hata huo uwekezaji wa serikali, na kwamba serikali imewekeza na ikaona eneo hili sasa limetosha, lakini bado serikali inahitaji kutoa *extension* ya eneo lile na kumtaka aondoke katika eneo lile.

Kwa kweli bado utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa wananchi pamoja na kwamba ardhi ni mali ya serikali, basi matatizo haya au haki hii kwa wananchi inakuwa haitumiki vizuri, kwa sababu hiyo serikali yenyewe ndio inayomiliki hao watu wenyewe. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na utaratibu mzuri wa kumridhisha hata yule mtu ambaye anataka kuondoka pale.

Kwa mfano, wapo wengine Mhe. Spika, wamechukuliwa maeneo yao hivyo hivyo kwa utaratibu huo huo kwamba mwananchi mwenyewe anataka kuliendeleza lile eneo, lakini kwa nguvu alizokuwa nazo mwananchi yule anataka kutanua eneo alilonalo. Kwa mfano, lile eneo ambalo anataka kulitanua lina miti tena ni eneo la watu wengi, lakini baada ya mashauriano walifika pahala hawakukubaliana kati ya yule mtu ambaye anayetaka kuliendeleza na wale wanaomiliki lile eneo hawakukubaliana kibei.

Lakini matokeo yake unakuta mtu yule alitumia mwenyewe utaratibu wake mwenyewe ikaenda ikatiwa thamani ile miti ambayo imo kwenye lile shamba, kwa hiyo ile miti sasa ikabidi walipwe fidia kulingana na bei za kiserikali ya ile miti na bado ikarudi dhana ile ile kwamba ardhi ni mali ya serikali. Kwa hivyo, sisi hatulipi ardhi tutalipa miti iliyokuwemo kwa bei zilizomo wakati ardhi ile ni ya muda mrefu, na lile ni eneo la kurithi na wananchi wenyewe wapo pamoja na wazazi wao wapo.

Mhe. Spika, kwa hiyo ile *term* ya ardhi ni mali ya serikali ilitumika vipi, isipokuwa ilitumika vibaya kwa wakati ule.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba amepewa dhamana kubwa juu ya suala la ardhi na atajua kwamba amepewa dhamana kubwa juu ya suala la ardhi pale Mwenyezi Mungu aliposema kwamba kutuambia wananchi

kuwa “ardhi na mbingu ni vyake”, kwa hivyo sisi wanadamu tusigombanie, ni vyake yeye Mwenyezi Mungu na hiyo ina tasfiri pana sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, jukumu hili tulilopewa la kusimamia ardhi tujue kwamba ardhi na mbingu mwenyewe ni Allah. Kwa hiyo, tutumie madaraka haya tuliyonayo kwa uadilifu na tuone kwamba tunawatendea haki hawa wananchi wetu ambao ndio tunaowategemea.

Kwa kweli sina mengi kama nilivyozungumza Mhe. Spika, isipokuwa mawazo au fikra ama mchango wangu ni huu juu ya mswada huu. Vile vile niipongeze Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuuchambua mswada huu mfupi na kutoa mapendekezo yao, mimi nakubaliana na mapendekezo haya yote na mawazo au fikra zao zote nakubaliana nazo na ninaziunga mkono.

Mhe. Spika, nakubaliana nazo naamini pengine wenzetu walipata ufafanuzi zaidi kuliko sisi hiyo *metres* pengine wameipata au wameiona na kuona kwamba wao kwa niaba yetu watoe mapendekezo haya. Kwa hivyo, sisi hatuna sababu ya kuyakataa mapendekezo haya ambapo wenzetu wameujadili kwa kina nakubaliana nayo, pia nimuombe Mhe. Waziri akubaliane nayo kwa sababu haya ni mapendekezo ya Kamati yetu ya Baraza na yanatokana na wananchi wenyewe na nguvu za wananchi wenyewe.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika na ninakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kujadili Mswada huu wa Sheria, ambao ndio ini au niseme moyo wa nchi.

Kwanza na mimi nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoona kwamba hivi sasa ipo haja ya baadhi ya sheria hizi kurekebishwa. Vile vile niwapongeze sana wanakamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ambao wametoa mapendekezo yao mazuri tena mwanana kifungu baada ya kifungu.

Mhe. Spika, mimi niiombe serikali kwa jumla kwamba tunapoleta marekebisho ya mswada Mhe. Spika, ni nyema ile miswada ya zamani basi tukaipata, kwa sababu unaposema nakusomea kifungu cha 5(2)(c) na (d) haidhuru tunatakiwa tufuatilie, lakini sasa nitakuwa sijui kifungu hichi kinaeleza nini, isipokuwa yale yanayosomeka humu ndio itabidi nifuate vile vile.

Kwa hivyo, Mhe. Spika niseme kwamba hivi sasa ardhi inashinda fedha, yaani fedha si lolote wala si chochote mbele ya ardhi. Kwa maana hiyo, niombe sana sheria hizi ambazo tumezileta kurekebishwa, basi ni vyema tukasimamia, tukazitekeleza pamoja na kuzifuatilia, kwa sababu kitu chochote ambacho unakibuni au unataka kukirekebisha kama hakuna usimamizi na utekelezaji pamoja na ufuatiliaji basi tutakuwa tunatia chumvi kwenye bahari.

Nikiendelea na mchango wangu naomba niende kwenye mapendekezo ya Kamati kifungu cha 5(2)(c) na (d) kuhusu maneno ya fidia yenye kuridhishwa yasomeke fidia kwa mujibu wa soko la sasa. Mhe. Spika, hapa naipongeza sana kamati, kwa sababu fidia hii itamfanya yule mlengwa kama amefikwa na tatizo lolote kwamba apishe katika maendeleo ya nchi au wananchi wana haja ya kitu basi utamfanya yule unayemfidia Mhe. Spika angalau afikishe lile lengo la kama ni nyumba au miti maana amepoteza nguvu zake siku nyingi na hii naipongeza sana. *(Makofi)*

Lakini nije kwenye mapendekezo ya jumla ambapo imeandikwa hapa kifungu cha 47(1) cha Sheria mama kinachohusu leseni ya miaka 99. Kwa kweli Kamati inahisi hiyo ni miaka mingi kwamba hata hao waliopewa, kwa maana hiyo niungane mkono kwamba miaka 99 kwa umri wetu wa sasa ni sawa na kumwambia nakupa hii nyumba au ardhi ama chochote kwa umri wetu wa sasa na tofauti na umri wa wazee wetu ambao hivi sasa wengine wameshapelekwa mbele ya haki.

Mhe. Spika, niunge mkono suala hili kwa kweli mtu unamwambia achukue kitu miaka 97 ni mingi mno Mhe. Spika.

Nikiondoka hapo kwenye mapendekezo ya Kamati sasa nije kwenye mchango wangu ambao nadhani na mimi nichangie. Mhe. Spika, kitu chochote kile kama hakina taaluma basi huwezi ukafanikiwa.

Kwa hivyo, niiombe wizara kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ni vyema wizara ikaandaa vipindi maalumu kwa upande wa redio na televisheni, kwa ajili ya kuelimishwa wananchi kuhusu utaratibu wa umilikaji wa ardhi na wakajijua. Kwa mfano, hivi karibuni tu tumesikia *bulldozer* limekwenda kuvunja nyumba za watu ambao wamejenga kwenye vyanzo vya maji.

Sasa naomba sana wizara hii itoe taaluma maalumu na iwe ni vipindi kwa siku na iainishwe hasa kwamba leo tarehe hii kutakuwa na taaluma ya kuhusu umilikaji wa ardhi na namna gani mtu anatakiwa atumie ardhi ile.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu hivi sasa kumeingia mtindo amesema mwenzangu Mhe. Abdalla Juma Abdalla, kwamba

kumeingia mtindo hivi sasa watu wanajijengea tu ovyo nyumba mlango huu umeelekea upande huu na nyengine mlango wake umeelekea upande mwengine, na hata njia yaani tunarudi karne ya nyuma hata mtu mgonjwa kama anaumwa basi achukuliwe kwenye gunia.

Kwa kweli mimi nashangaa Mhe. Spika, wakati hivi sasa tusielekee huko na wala tusijirudishe huko hivi sasa tuelekee na tutizame *vision* ya hivi sasa inasemaje, hilo moja ambalo nilisema nilizungumze.

Jengine Mhe. Spika, uvamizi wa ardhi umekuwa mkubwa namuonea huruma Mhe. Waziri, maana amerithi madhambi lakini Mwenyezi Mungu atamsaidia, kwa sababu amerithi madhambi makubwa sana ya uvamizi wa ardhi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ajitahidi inavyowezekana kwamba sasa zile sheria ambazo zinaoana na umilikaji wa ardhi, kwa sababu kuna Mahakama ya Ardhi pamoja na mambo mengine mengi kuhusu ardhi.

Kutokana na hali hiyo, basi nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, awakutanishe kwa ajili ya kupanga mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba ardhi sasa basi kuvamiwa na wala si kuvamiwa tu, isipokuwa mtu aangalie hapa je ni pahala pa kujenga au kilimo ama kwa ajili ya kufanya jambo gani hapa. Mhe. Spika, nimuunge mkono Mhe. Abdalla Juma Abdalla aliposema kwamba itafika wakati hata kile kisiki cha muhogo pa kukibandika kwenye nyumba basi huna sehemu hiyo. *(Makofi)*

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba haya nayo pia ayasimamie ipasavyo.

Lakini hee! Mhe. Spika, nadhani tusimpelekee madongo tu Mhe. Waziri na sisi wenyewe miongoni mwetu tunayo matatizo na wala sisemi watu wote Mhe. Spika, isipokuwa baina ya Waheshimiwa na Wananchi kwa jumla. Kwa kweli mtu hataki kufuata taratibu wala sheria na kama hutaki kufuata taratibu na sheria za nchi na wewe unapofikwa na lile janga basi usinung'unike na wala usipige kelele au usimuendee Mheshimiwa hapa nimeonewa ama nimefanywa nini, kwa sababu utamfanya na yule Mheshimiwa ambaye ni mtunga sheria na yeye akiuke sheria. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitoe wito Mhe. Spika, kwamba baadhi yetu sisi viongozi na wala sisemi Waheshimiwa Wawakilishi tu, isipokuwa ni baadhi ya viongozi wengi sisi ndio tuliosababisha tukavamia ardhi bila ya mpango, wala bila ya kudhani kwamba hali hii italeta vurugu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme kwamba kwa upande wa wananchi niwasihi wananchi kuwa si vizuri kugombana na utawala wao, hivyo ni wajibu wetu sote kufuata taratibu na sheria.

Jambo jengine niseme kuwa maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe na ukitaka kujenga kuweka vizuri kama kuna kitu hakipendezi basi lazima ubomoe. Kwa kweli hivi sasa karne tuliyonayo hatutabakia ile karne ya nyuma ni lazima tufuate karne ambayo wenzetu wanaifuata na sisi tutoke kule tulikokuwa twende kwahala ambapo ni kuzuri.

Kwa maana hiyo, nitoe wito kwa wananchi, vile vile niiombe Wizara kupitia kwako Mhe. Spika na hapa amezungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin kama kuna kitu ambacho kinataka kupita kwa ajili ya maendeleo ya nchi, basi ni vizuri mwenye ile ardhi na ninajua ardhi mwenyewe ni serikali, lakini yule ambaye amekaa miaka mingi, yaani tokea babu yake, akaja baba yake mpaka akazaliwa yeye basi apewe thamani na wala kusiwe na mivutano, na kukiwa na mivutano Mhe. Spika, basi ndio sasa hapo watu wanapoisema serikali kwa ubaya.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema wakae chini wakubaliane kama ni miti basi itiwe tathmini lakini isitiwe tathmini ya tokea mwaka 1760 isipokuwa itiwe tathmini ya miaka hii kama ilivyosema kuhusu habari ya ulipaji wa fidia kwa sehemu ile, kwa sababu hapo ndipo unapotokea utatanishi Mhe. Spika, wananchi wetu wanakuwa wakali kwa sababu hawakupewa haki zao.

Sasa leo niambie unamvunjia nyumba yake na wakati huo ilikuwa ni shilingi milioni tatu, lakini hivi sasa utaijenga nyumba ya milioni tatu kweli, huwezi kabisa. Kwa hivyo, usichukue fidia ya milioni tatu ya nyuma na ukamlipa mtu ambaye hivi sasa hata ukimpa zile shilingi milioni tatu au laki tatu hawezi kufanya chochote na mtu yule ana familia, watoto pamoja na wajukuu.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili alisimamie ipasavyo, ili mambo yetu yaende sambamba na matakwa ya wananchi.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, hapa kidogo maana kuna umilikaji wa ardhi. Kwa mfano, kuna zile eka tatu walizopewa wananchi, kuna mashamba ya karafuu. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba lile ambalo ni lake basi anijibu na ambalo si lake aniambie niende wapi.

Kwa kweli hivi sasa umeingia mtindo wa watu kurithi mambo ambayo si yao kabisa, isipokuwa akishakuona eneo limekaa basi ataanza kuweka kidude

kidogo cha kujionesha yeye yupo pale na halafu ukitimia mwezi kuna kibanda amekiezeka makuti mawili au matatu na ikitimia miezi mitatu au mitano basi unakiona chuma cha nyumba kimeteremshwa.

Mhe. Spika, nikija kwenye mambo haya niingie katika yale mambo ambayo nimeyasema hivi sasa kama yake basi anijibu na ikiwa si yake asinijibu, najua ipo wizara inayohusika, lakini kidogo hapa kuna utatanishi maana haya mambo ya ardhi wakati mwengine tunasema ardhi ni mali ya serikali, lakini kuna umilikaji wa mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba nijiulize kwamba haya mashamba ya mikarafuu yale ambayo hayana wenyewe haya yanamilikiwa na Wizara ya Kilimo, maana kuna ardhi mtu amepanda mkarafuu na hiyo ni ardhi, yanamilikiwa na wizara ya umilikaji wa ardhi au mashamba haya yanamilikiwa na nani, kwa hiyo ikiwa lake Mhe. Waziri namuomba kupitia kwako Mhe. Spika anijibu, na ikiwa si lake basi aniambie ili niweze kuuliza swali la nyongeza japo kipindi kinachokuja, ili tuondoshe huu utata uliopo hivi sasa. Suala hili limekuwa ni utata ambao watu hivi sasa wanavamia Mhe. Spika.

Baada ya kusema hayo, nimpongeze sana Mhe. Waziri na niseme naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tumefikia pahala pazuri na inafaa sasa tumpe muda Mhe. Waziri, ili jioni tufanye majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani muda unakaribia zimebakia dakika 15 hizi basi ni vyema twende tukapumzike, ili Mhe. Waziri aje afanye majumuisho jioni na Mhe. Hamza Hassan Juma nastaajabu lakini hakuomba muda wote na wala hakuna muda mwengine tena.

Kwa hivyo, naomba kuakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni, ambapo Mhe. Waziri atakuja kufanya majumuisho wakati huo.

(Saa 6:45 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na tukaweza kuendelea na kikao chetu

hichi jioni hii, naomba nikushukuru na wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Spika, na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wajumbe waliokuwa wakizungumza tokea asubuhi kuhusiana na hoja ya mswada huu ya marekebisho ya sheria za ardhi kuhusiana na umuhimu wake, kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuchukua hatua ya kuona haja ya kufanya marekebisho haya na kuyaleta mbele ya Baraza lako tukufu. Kusema kweli haya marekebisho yatatusaidia sana katika usimamizi wa sheria zetu za ardhi. Na bila shaka yatafungua mlango wa kuzingatia marekebisho zaidi huko mbele ambayo yataisaidia kufanya usimamizi wa sheria za ardhi kuwa rahisi zaidi.

La tatu Mhe. Spika, naomba na mimi nichangie kwa ufupi sana katika hoja hii na hasa katika lile eneo ambalo Mhe. Waziri aliniomba nitoe ufafanuzi kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu waliliuliza, naamini mengine yeye mwenyewe ni mweledi atayatolea ufafanuzi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, alichoniomba Mhe. Waziri na mimi mwenyewe naona ni vizuri kulitolea ufafanuzi zaidi kwa sababu limeulizwa hapa na ndio pahala pake ni suala la umiliki wa Kisiwa cha Latham ambalo limeulizwa na Mhe. Mohammed Raza na pia Mhe. Ismail Jussa na nadhani Mheshimiwa mwengine ni Mhe. Asaa Othman Hamad limekuwa limenipita.

Mhe. Spika, nadhani hili kwenye kikao chetu jana kwa ufupi tulilizungumza lakini nadhani kwa sababu ya kukosekana ule ufafanuzi Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na haki ya kuwa na wasiwasi, na kwa sababu hiyo tukasema labda uniruhusu nitumie muda kidogo nieleze msingi wa kwa nini Zanzibar tunaona kwamba na tunaamini kwamba hichi kisiwa ni cha Zanzibar na mwengine yeyote aliyekuwa na madai hatumkatazi kuwa na madai, lakini tunaamini kwamba hatokuwa na hoja ya kisheria ya kuthibitisha madai yake hayo. Kwanza Mhe. Spika, Kisiwa cha Latham kwa jina jengine Fungu Mbaraka, kwa jina jengine pia kinaitwa pia Fungu Kizimkazi.

Kabla ya mikataba baina ya Wajerumani na Waingereza ya mwaka 1866 na mikataba ya mwaka 1890 kuna ushahidi wa kutosha ambao haupo tu Zanzibar lakini upo katika nyaraka na kumbukumbu katika majumba ya nyaraka ya Ufaransa, *French National Archives* na pia katika Ofisi za Nyaraka za Uingereza yaani *British National Archives* na zinaanzia siku za nyuma kabisa. Na miongoni mwa mfano huo ni kwamba miongoni mwa nyaraka ambazo ziko katika *archives* ya Wafaransa kwa mfano, inaonesha kwamba tarehe 1/8/1844 Sultani wa Zanzibar aliwahi kutoa kibali kwa Bwana mmoja akiitwa Captain Cogan kwa ajili ya kuchimba na kutumia na kuuza samadi ya ndege ambayo ni nyingi sana katika kisiwa kile. Na mwaka 1851 akatoa pia kibali

kwa Bwana mmoja Muingereza akiitwa Lindsey kwa ajili ya kuchimba na kutumia ile samadi ya ndege na akampa *exclusivity* ya miaka miwili kuweza kuchimba na kutumia ile samadi kwa ajili ya kuuza.

Kwa hivyo ulipokuja mkataba wa mwaka 1866 kwa nini naeleza mikataba, nitakuja kueleza huko mbele kwa sababu hiyo ndio misingi ya baadhi ya hoja za wale wanaodai kwamba labda hiki kisiwa hakiko upande wa Zanzibar. Lakini mwaka 1866 kilichofanyika katika mkataba baina ya Waingereza na Wajerumani ni kutambua au kukubali kwamba Wajerumani wachukue ile sehemu ya Sultani wa Zanzibar iliyokuwa Tanganyika na kwamba yeye wanamuachia ukanda wa mashariki ya pwani na sehemu nyengine zilizobakia wanamuachia.

Na mwaka 1890 mkataba baina ya Wajerumani na Waingereza ambao maarufu unaitwa *Heligoland Treaty* hasa kifungu cha 11 cha mkataba ule ilikuwa ni kuwapa Wajerumani Kisiwa cha Mafia kutoka kwa Zanzibar kuwapa wao kwa sababu mpaka mwaka 1890 kabla ya mkataba Mafia ilikuwa ni sehemu ya Zanzibar, baada ya kuchukuliwa ile *territory* iliyokuwepo yaWatanganyika. Kwa hivyo mkataba ulitambua kuipa Mafia kuipeleka kwa Wajerumani na pia Wajerumani wakapewa Heligoland. Lakini kikubwa ni kwamba haya yalikuwa ni makubaliano baina ya Wajerumani na Waingereza, hayakuwa makubaliano baina ya Zanzibar, Ujerumani na Waingereza, wenyewe katika makubaliano yao walikuwa wanajibishana barua na zipo ambazo walikuwa wanasema kwamba kutokana na mikataba hii Muingereza anakubali kutumia *influence* yake kwa Sultani wa Zanzibar kumshawishi akubali hili na hili na hili.

Kwa hivyo suala hoja ya Latham kwamba ipo upande gani ipo kwa Wajerumani au kwa Zanzibar kwa mara ya mwanzo ilikuja mwaka 1898 mwezi wa Agosti. Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza waliiandikia Serikali ya Zanzibar *first minister* kumuuliza kwamba je, Latham iko Zanzibar au iko upande wa Tanganyika? Na baada ya wao kupata hoja kutoka kwa Kampuni moja ambayo ilikuwa na hamu ya kuchimba ile samadi ya ndege ili wajue jee wakaombe kibali kwa Wajerumani au waombe kibali Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya Serikali ya Zanzibar kupata hoja hiyo kutoka Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza ikajibu mnamo tarehe 15 Oktoba, 1898 kwamba suala hili linahitaji kuangalia vizuri ile mikataba ya mwaka 1866 na mwaka 1890. Lakini aliyeandika barua hii bwana *Arthur Hardinge* alisema kitu kimoja, kwamba mikataba hii ni kweli kwamba haiko wazi kuhusiana na umiliki wa Kisiwa hiki, lakini miaka yote kisiwa hiki kimekuwa upande wa Zanzibar.

Hoja ya pili aliyoieleza ni ile ambayo nimetangulia kuieleza kwamba mikataba hii ikumbukwe ni baina ya Wajerumani na Waingereza. Kwa hivyo kwa Kisiwa hiki kwamba hakikutajwa katika mikataba hiyo haina maana kwamba kimeondolewa Zanzibar.

Lakini na hoja ya tatu aliyosema ni kwamba kwa mikataba hii kunyamaza kimya kuhusiana na umiliki wa Kisiwa hiki kwa Zanzibar haina maana kwamba walipewa Wajerumani. Kwa hivyo hizo ni hoja tatu ambazo alizitoa. Lakini na pia akatoa rai ya kwamba kwa ajili ya kuondoa utatanishi, kisheria za kimataifa tunaweza tukasema basi Kisiwa hiki si cha mtu au ni ardhi iliyokuwa si ya mtu yaani *no man's land.* Kwa hivyo tunatoa rai kwamba Sultani aende akakidai kisiwa hiki kwa kufanya mambo mawili ambayo kwa sheria za kimataifa inakubalika kwamba kukifanya kiwe ni chake rasmi. Cha kwanza tunasema lazima kuwe na *physical ownership* yaani ukakikalie rasmi.

Mhe. Spika, rai ya pili aliyotoa ambayo inatakiwa katika sheria za kimataifa ni kwamba uwe na *administrative authority*, yaani ikiendeshe rasmi. Na kwa kufanya hivyo Sultani tarehe 17 Oktoba, 1898 akamuagiza rasmi Sir Lord Mathews kwamba aende akafanye kazi hiyo. Na aliyeagizwa akachukua hatua za haraka tarehe 18 akaondoka kwenda katika kile kisiwa na tarehe 19 alfajiri akakiweka alama rasmi na baadaye wakapiga na mizinga 21 kutangaza rasmi kwamba kisiwa kile ni mali ya Zanzibar. Na akaweka alama na wakajenga na nyumba na wakamchagua mtu maalum wa kukisimamia ili kutimiza mambo yote mawili ya kisheria yanayotakiwa.

Mhe. Spika, baada ya hatua hizo zilizochukuliwa hakukuwahi tena kutokea hoja ya kudai kisiwa hiki, hoja ilikuja mwaka 1910 na ilikuja baada ya Serikali ya Zanzibar kumuandikia Gavana wa Ujerumani Dar es Salaam kuna watu wenu wanatoka wanakwenda kuchukua samadi ya ndege bila ya ruhusa ya Serikali ya Zanzibar. Baada ya kuandikiwa hivyo na Wajerumani nao tarehe 23 Disemba, 1910 wakajibu wakasema sisi tunavyofanya hiki Kisiwa ni chetu.

Lakini Serikali ya Zanzibar mwaka 1911 tarehe 11Aprili ikaiandikia Serikali ya Ujerumani kujibu barua yao hii ya tarehe 23 Disemba, 1910 kuwaeleza yote haya kwamba hiki Kisiwa hakiwezi kuwa cha kwenu na hakuna msingi wa kuwa cha kwenu. Lakini na wakawakumbusha katika miongoni mwa ushahidi waliotumia, wakawakumbusha kwamba Serikali ya Ujerumani mbona leo mnageuka, maana mwaka 1899 mwezi Januari tuliwaandikia kutaka kuwakumbusha au kutaka kuwashauri kwamba katika eneo la Zanzibar tunataka kuweka minara ya kuongoza meli na tunataka kuweka minara hii Kigomasha kule Pemba, Chumbe kwa Zanzibar na pia katika Kisiwa cha Latham. Lakini na nyinyi Ujerumani mkatujibu mwezi wa Machi mwaka

1900 kwamba sisi hatuna tatizo lakini tunahisi kwamba muweke mnara Kigomasha na Chumbe. Kwanza muweke unapotakiwa ni Kigomasha, Chumbe si haraka unaweza kuwekwa baadae lakini Latham mkiweka unaweza uka-*confuse* na ule uliowekwa kwenye Kisiwa cha Mafia, kwa hivyo inaweza ikazipoteza meli. Anamkumbusha kwamba na sisi mwezi wa Mei mwaka 1900 tukawaeleza tena kutoa ufafanuzi kwa nini kuna haja ya kuweka mnara katika Kisiwa cha Latham, na mkatujibu katika mwezi wa Septemba mwaka 1900 kwamba tunaona bado hakuna haja kitaalamu na sisi tukakubali mbona hamku-*claim* kwamba Latham ni ya kwenu?

Mhe. Spika, baada barua hiyo ya tarehe 11 Aprili, 1911 hakuna kumbukumbu zozote zinazoonesha kwamba Serikali ya Tanganyika iliwahi kudai tena kisiwa hiki. Na katika barua hiyo ya tarehe 11 Aprili, 1911 ilitolewa rai kama nyinyi mna hamu mnaona hiki kisiwa kitawasaidia, njooni mkae na Serikali ya Zanzibar tuzungumze. Wakaambiwa yanazungumzika, kama yalivyozungumzika mkapewa Mafia, kama yalivyozungumzika na Serikali ya Uingereza mkapewa Heligoland. Kwa hivyo haikujibiwa wala hawakuja na baada ya hapo hakukuwahi tena kuletwa madai yoyote mpaka hii leo tunayosema.

Sasa mwaka 1959 hapa katikati kwanza kuna shughuli nyingi ambazo zilifanywa ikiwemo mpango wa Serikali ya Zanzibar kupanda miti katika kisiwa kile na ripoti zipo, taarifa zipo, ushahidi upo. Ziara mbali mbali ambazo zilifanywa na viongozi mbali mbali kati ya mwaka 1921 mpaka mwaka 1959 ripoti zipo, taarifa zipo. Lakini mwaka 1959 kupitia tangazo la kisheria namba 56 kisiwa kile kikatangazwa ni hifadhi ya ndege chini ya sheria ya hifadhi ya Ndege Zanzibar sura 124. Lakini kama hiyo haitoshi na kwa ajili ya kuondoa utatanishi katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1963 ibara ya 136 katika ufafanuzi wa dola ya Zanzibar ikaelezwa, yaani *State of Zanzibar* maana yake ni Unguja, Pemba na Latham.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaposema kwamba tuna ushahidi wa kutosha tuna uhakika wala hatuna wasiwasi katika hili kwa sababu tuna sababu za msingi za kisheria, za kiutawala, za kihistoria. Anayedai leo hoja yake kubwa anasema kwamba kwa sababu ya mikataba hiyo tuliyoitaja 1866 na 1890. Lakini kichekesho kikubwa zaidi anasema kwa sababu ya ramani ambayo imechorwa Tanganyika mwaka 1953, tena ramani hii imechorwa na Idara ya Umwagiliaji. Kwa hivyo mimi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika, watuamini tunaposema kwamba, sababu labda iwe kwa nguvu, kama mtaweza kupigana kwa nguvu hilo sina hakika, lakini kwa sheria tunapoambiwa kwamba tuna sababu za msingi, tuna misingi ya kisheria ya kwamba kisiwa hiki ni cha Zanzibar, ni kwa sababu tunazo si za kuzua wala

sio za kupanga. Wala hatujazileta leo baada ya kugawa vitalu vya mafuta hizi zipo zamani.

Sababu ya hoja hii kuletwa leo nadhani tutapokuwa na semina ile tarehe 19 Oktoba mwaka huu ambayo ni siku ya kutimiza miaka 115 tokea kisiwa kile kiwe chini ya mamlaka ya Zanzibar rasmi, siku ile pengine mtapata kujua sababu ya hoja hizi kuletwa sasa hivi. Lakini ukiachia hiyo sababu ziko wazi nadhani nimezieleza.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba tuipitishe hoja hii ili tumuwezesha Mhe. Waziri aende akafanye kazi ya kusimamia vizuri rasilimali yetu ya ardhi.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, Waheshimiwa Wajumbe mmefahamu kwamba mchango huu ni sehemu ya majumuisho ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kutuwezesha kukutana tena jioni hii katika jambo muhimu hili la kuendelea na kujadili hoja hii muhimu inayohusiana na mambo ya ardhi, jambo ambalo tuseme kwamba linaleta mustakbali mzima wa maisha ya mwanaadamu, kwani bila ya ardhi hakuna nchi, na bila ya ardhi hakuna kuishi.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuzungumza machache mno, mimi sitaki niseme mengi, nataka nizungumze kwa ufupi tu na hatimaye nimuachie Waziri ili aje akamilishe shughuli hizi kwa kutoa majumuisho na kupitishwa hoja hii kama vile inavyokusudiwa.

Mhe. Spika, ni kweli nithibitishe kwamba migogoro ya ardhi ipo na hususan imegawika katika hali mbali mbali. Aidha kuna migogoro ya ardhi inahusiana na wananchi ambao wananchi wetu wa Zanzibar wengi mno sasa hivi huwa wanavamia ardhi, aidha wengine niseme kwamba pasipokuelewa na wengine kwa kufanyiwa kwa makusudi ili wawe wanavamia ardhi hizo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwezi wa nane tumefanya ziara na Mhe. Waziri na tukaelekea katika maeneo ya Tunguu, lakini kwa kweli jambo la kusikitisha baada ya kufika Tunguu, tuliona watu wengi sana ambao wamevamia maeneo ya Tunguu ambayo ni maeneo ya serikali. Na maeneo hayo ndani ya wavamizi ambao waliovamia kuna baadhi ya watu ambao wamejihalalishia au wamejimilikishia maeneo yale na kutafuta wapimaji ambao si wapimaji wa serikali, wakayapima maeneo yale na hatimaye

kuwauzia wananchi. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Na ukiangalia katika kupima kwao huwezi kutofautisha jinsi ambavyo wanavyopima watu wetu wa Idara ya Ardhi na Usajili na vile wanavyopima wao. Kwa kweli haitofautiani kabisa. Kwa sababu ukiangalia hata *beacon*, *beacon* wanazoziweka wao unaweza ukafikiria labda ni *beacon* zetu ambazo zimewekwa na watu wetu wa Idara ya Ardhi na Upimaji. Sasa hili ni jambo la kusikitisha kabisa. Lakini vile vile watu hawa wamefikia pahala wanatoa hati, na hati zile wanazozitoa kama utawekewa hati yetu ya Wizara ya Ardhi na hati wanayotoa watu hawa basi huitafautishi kabisa.

Kwa hivyo hii hali ya uvamizi ni kweli ipo na sisi Wizara sasa hivi tuko makini katika kulifuatilia suala hili na uthibitisho wa kulifuatilia hili baada ya kuona hali inayoendelea maeneo ya Tunguu. Tumekaa Wizarani pale na tukajadiliana na Waziri wangu pamoja na watendaji wetu na tukachukua hatua zinazofaa za kisheria kwa kuvunja baadhi ya nyumba ambazo tayari ilikuwa zimeshaanza kujengwa katika maeneo ambayo yamevamiwa.

Kwa hivyo niwaombe sana wananchi waelewe kwamba ardhi kama ardhi basi wanaohusika na kutoa ardhi ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Idara yake ya Ardhi na Usajili si wengine wowote.

Mhe. Spika, chengine ninachotaka kukisema ni kwamba tulete masikitiko vile vile kwa wananchi wetu. Wananchi wengi huwa wanatuletea maombi ya kuomba ardhi kwa malengo tofauti. Aidha kuna wengine hutuletea maombi ya ardhi kwa malengo ya kupata viwanja kwa ajili ya kujenga nyumba zao za makaazi, lakini vile vile kuna watu wengine ambao hutuletea maombi ya kuomba ardhi kwa malengo ya ukulima. Lakini cha kusikitisha tayari mtu ambaye kaomba kwa ajili ya kulima basi unapompa eneo lile kwa wingi anaweza kufanya ni kuendeleza kilimo pengine kwa miaka miwili au mitatu, lakini inapozidi miaka ile...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Naibu Waziri anaendelea kutoa maelezo ikiwa nayo ni sehemu ya kumsaidia Mhe. Waziri katika majumuisho ya hoja hii, nawaomba tumsikilize.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Baada ya wananchi hao kuendelea na shughuli za kilimo katika kipindi cha miaka 2 au mitatu hatimaye eneo hilo la eka hukata viwanja na kuwauzia wananchi kwa ajili ya makaazi, jambo ambalo kwa kweli linatusikitisha sana. Kwa sababu tunapotoa hati na uthibitisho kwamba eneo la ukulima basi libaki katika mambo ya ukulima. Na eneo ambalo tunalotoa kwa ajili ya viwanja vya kujenga nyumba za makaazi libaki katika hali ambayo iliyokusudiwa. Hili

linatusikitisha sana, niwaombe sana wananchi tabia hii waiache na inairudisha nyuma serikali katika hatua nzima ya maendeleo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nizungumzie migogoro ya ardhi kama vile ilivyozungumzwa mwanzo kwamba kuna migogoro aina tofauti, lakini kuna migogoro ambayo hujitokeza ikisababishwa na sisi wenyewe viongozi kama alivyoeleza Mhe. Asha Bakari, kazungumzia kuna baadhi ya migogoro mengine inasababishwa na baadhi ya viongozi hilo ni kweli lipo. Na baada ya serikali kuliona hili Mhe. Rais wa Zanzibar kafanya semina ndani ya Kisiwa cha Pemba pamoja na Kisiwa hiki cha Unguja, lakini kule Pemba katika kufanya semina hiyo kawaita masheha, akawaita madiwani, akawaita Wakuu wa Mikoa na sisi wenyewe Waziri pamoja na Naibu Waziri tulikuwepo katika semina hiyo. Lakini ukiangalia bado migogoro ya ardhi ipo, hususan niseme katika Jimbo langu mimi mwenyewe la Nungwi ipo migogoro hiyo, kuna migogoro chungu nzima, wananchi wengine aidha wanakosa haki zao, wengine wananyan'ganywa tu makusudi lakini kwa kweli ipo katika hali tofauti na ukizingatia zaidi migogoro hii ni kweli inasababishwa na baadhi ya viongozi.

Niwaombe sana viongozi wa serikali ikiwemo pamoja na mimi mwenyewe na Wawakilishi wote hii tabia tuiache. Mwenye haki ya kutoa ardhi ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia idara yake. Sisi tunapenda tushirikiane na viongozi katika ufuatiliaji wa kutoa hizi ardhi aidha masheha, madiwani, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwa kututhibitishia tu kama kweli eneo hili liko hivi na hivi, lakini wao sio watoaji wa ardhi hiyo. Niwaombe sana viongozi wenzetu hili suala waliache mara moja kwa mustakabali mzima wa kuijengea maendeleo nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza mwanzo kwamba sitaki niseme mengi na naomba nimuachie mwenyewe Waziri aendelee na kujibu hoja hii na baada ya kusema hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru mara ya pili kwa kunipa tena fursa hii ya kusimama mbele ya Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu na kutoa ufafanuzi wa hapa na pale katika mijadala ambayo tunaipata humu ndani.

Mhe. Spika, mswada wangu umechangiwa na watu 12, naona kabla sijaanza kutoa ufafanuzi niwataje ili kuwatambua.

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa; Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
8. Mhe. Asaa Othman Said
9. Mhe. Salmin Awadh Salmin
10. Mhe. Asha Bakari Makame
11. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na
12. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Spika, amechomoza mtu wa 13 ambaye amechangia kwa maandishi Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, michango ni mizuri na kwa kweli itasaidia sana kuifanya sheria hii kuwa nzuri, ni mabadiliko machache kama walivyosema Wajumbe lakini mabadiliko muhimu kama walivyosema asubuhi, ya kuwezesha Ofisi yetu ya Mrajis kushughulikia vizuri suala zima la ardhi katika wakati huu wa kusajili ardhi.

Mhe. Spika, naanza na mapendekezo ya Kamati kama yalivyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwanza napenda kuishukuru Kamati kwa kupitia kwa kina mswada wa marekebisho mbali mbali ya sheria ya ardhi, kutoa mapendekezo yenye nia ya kuufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Kimsingi tumeyakubali maoni yote yaliyotolewa na Kamati na yanaingizwa kama ni marekebisho ya mswada huu.

Katika mswada huu Mhe. Spika, kulikuwa kuna Sehemu ya Tatu ambayo ilikuwa na kifungu cha marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Ardhi. Sehemu hiyo imependekezwa na Kamati itolewe na badala yake ifanyiwe marekebisho baadaye katika sheria nzima. Mapendekezo hayo yalielezwa na Mwenyekiti katika hotuba yake japo kuwa haionekani katika mapendekezo ya Kamati yaliyowasilishwa, wizara imekubaliana na mapendekezo hayo.

Nitaje kiufupi tu baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ambavyo vifungu vyake aidha vilichangiwa na Wajumbe au kuuliziwa maswali.

Katika kifungu cha tatu kinachohusu utolewaji wa haki ya matumizi ya ardhi kwa taasisi ambapo kamati ilionya kwamba suala hili linaweza kuleta migogoro ikiwa haitawekewa misingi madhubuti hasa kwa kampuni zinazoendesha biashara na hivyo kutaka liangaliwe kwa kina. Wizara

imepokea maoni hayo na hivyo inaingizwa katika marekebisho haya kuwa haki ya matumizi ya ardhi itatolewa kwa taasisi za serikali tu.

Wizara ilipokea na kuyakubali marekebisho yaliyopendekezwa ya kuwapatia ardhi wale waliopoteza sifa za Uzanzibari kwa njia ya ukodishwaji kwa masharti maalum tofauti na masharti ya wageni. Kwa kuanzia kifungu cha 46 (2) cha sheria mama kinachohusiana na masuala ya ukodishwaji. Mapendekezo haya pia yamepokelewa na wizara na yanawekwa katika marekebisho.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia wizara hii naanza mmoja mmoja ambaye wa kwanza ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mhe. Makame ameulizia juu ya suala la muda wa kukodishwa *lease* kwamba ni mrefu. Nimesema kwamba suala hili la mwaka 1999 tutalijadili wakati wa kuleta marekebisho ya sheria nzima ya ardhi ambayo hivi sasa iko katika matayarisho kwamba ifanyiwe marekebisho.

Jengine ameulizia juu ya suala la Hiba, hiba ni nini? Hiba ni *gift* kama alivyosema Mhe. Abdalla Juma Abdalla, ni zawadi ambayo mtu anaweza kuitoa kwa sehemu ya mali yake kumpa mtu, na anapofanya hivi ningewasihi Wajumbe wenzangu kwamba anayetaka kufanya hiba wakaangalia sheria ya urithi wa Kiislamu, wasije wakaitoa mali yote kuwa ni hiba, kuna asilimia fulani maalum inakubalika kama ni kutoa hiba kwa ajili ya mtu ambaye unataka apate hiba hiyo. Kwa hivyo, waliopewa hiba hii ndio tumewaingiza katika masuala ya mswada huu.

Vile vile tunasema kwamba mwenye udugu wa damu. Tunajua limekuja pendekezo moja hapa limesema kwamba isiwe kwamba ni udugu wa damu tu, madhali mtu mwenyewe anataka kutoa hiba kumpa mtu aachiliwe. Hilo vile vile Mhe. Spika, naliacha kwamba anayetaka kufanya hivyo akatizame sheria yetu ya Kiislamu kwa wale Waislamu ni wakati gani na nani anastahiki kupewa hiyo hiba ambayo unataka kuitoa.

Mhe. Spika, utaratibu huu unafanyika na watu wanapewa hiba hizi katika maeneo mbalimbali, lakini ningeshauri kwamba tuangalie vizuri sheria zetu za Dini ya Kiislamu katika kutoa hiba tusitoe tu moja kwa moja tukaitoa mali yote.

Halafu Mhe. Makame Mshimba amesema fidia zisichelewe. Hilo nalikubali na nitalifanyia kazi na kuona kwamba fidia hazichelewi. Halafu tuepuke tabia ya kutoa hati zaidi ya moja kwa kiwanja kimoja. Hiyo jitihada Mhe. Spika, tunajitahidi kuifanya sasa hivi, hatupendi kuona kwamba kiwanja kimoja tumewapa watu wawili kwa hati, na ikitokezea hivyo basi zote mbili

tunazifuta au tatu tunafuta na tunaanza kutoa upya sasa hivi kwa ajili ya maeneo hayo.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali ametoa pongezi kwa Wizara na amesema tufanye tathmini kwa ardhi yote ya Zanzibar pamoja na visiwa vyote vya Zanzibar kikiwemo Kisiwa cha Fungu Mbaraka ambacho amekizungumza kwa urefu. Mhe. Mwanasheria Mkuu muda mfupi uliopita amefafanua umiliki wa kisiwa hiki cha Fungu Mbaraka.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Moh'd Ali yeye aliulizia juu ya kuja kwa sheria hii na akaulizia juu ya suala la kifungu cha 4(c) ambacho kinasema, 'ardhi iliyoendelezwa italipwa'. Mhe. Spika, utaratibu wetu ni kwamba wanasheria wangu mara nyingi wananambia, tafsiri ya ardhi maana yake ni ardhi yoyote, ardhi khaaliya, ambayo ni ardhi tupu na ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar aliitangaza tarehe 8 Machi, 1964. Ni *natural land* kama ilivyotolewa ufafanuzi hapa na baadhi ya Wajumbe waliochangia hoja hii. Ardhi hiyo ni mali ya serikali pamoja na vilivyomo chini ya ardhi hiyo, pamoja na vilioko juu ambavyo havihamishiki, vyote ni mali ya serikali. Ukisema vilioko chini ya ardhi hiyo maana yake ndio unakuja kwenye mafuta, gesi, madini na mambo mengineyo ambayo yako chini yote yanakuwa ni mali ya serikali pamoja na milima, majabali ambayo mengine yanaweza kuwa yana vitu vya thamani nayo pia yanakuwa ni mali ya serikali. Kinachowekwa na mtu pale juu kwa kuendelezwa kama nyumba, mti na mambo mengineyo hiyo inakuwa ni mali yake yule mtu mwenyewe juu ya ardhi ile.

Kwa hivyo, hii ndivyo ilivyo na ndivyo tulivyokusudia ambapo Mhe. Abdalla Moh'd akumbuke iko hivyo. Yeye ndiye aliyependekeza vile vile kwamba isiwe ulazima wa mtu mwenye uhusiano wa damu tu ndio apewe hiba. Nasema hili Mhe. Spika, mimi hili siko *conversed* nalo kwa sababu lazima turudi kwenye sheria tutizame hiba inatolewa vipi siwezi kulizungumza mimi hapa.

Halafu aliulizia juu ya suala la fidia yenye kuridhisha ambalo anasema hili haliko wazi. Mhe. Spika, sisi tunapotizama ardhi na tukazungumzia fidia yenye kuridhisha tunatizama *location* ya ile ardhi, kuna tofauti ya kulipa fidia katika ardhi iliyoko mbele ya barabara katika eneo ambalo ni *market place* ambayo inaweza ikauzika kwa bei kubwa zaidi ile tunaitizama kwamba ni fidia ya kuridhisha kwa eneo lile. Halafu tunatizama eneo ambalo liko ndani kabisa ambako huko hakuna thamani sana kwa kufanya biashara na mambo mengineyo. Wakati mwengine vile vile inakuwa eneo la ufukwe ambalo mtu anaweza akalichukua na likawa na mradi wenye maana. Sasa hapo ndipo alipozungumzia fidia yenye kuridhisha kutegemea ardhi hii iko mahala gani, tabaan ardhi utakayoinunua Darajani leo ambapo pana soko ni tofauti na ardhi

utayoinunua Chumbuni ndani kule ambako hakuna soko. Kwa hivyo, hapo ndipo tunapima ardhi hiyo iko *location* gani na iko vipi, ndio tunapozungumzia thamani ya ardhi ya kuridhisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu namshukuru sana na yeye nilikuwa naye tangu kwenye Kamati huko. Namshukuru sana kwa pongezi zake alizotupa na alitoa pendekezo ambalo kusema kweli nalikumbuka sana na limekuwa likinipa shida kwa muda wote ninapofikiria mswada huu kwamba alisema uchapwe upya kwa kurahisisha upitishaji wakati tutapokuja kukaa kitako hapa. Nasikitika sana kwamba hili hatukuwahi kulitekeleza, tulitekeleza lakini sio ule waraka *official*, hatuwezi tukauleta hapa kwa sababu haujawa *official*. Waraka *official* lazima uje kwenye *house* na ukubalike na Katibu na usambazwe kwa Wajumbe wa Baraza hili. Ni wazo zuri kabisa na tutarekebisha katika masuala yanayoendelea.

Halafu amezungumzia juu ya masuala ya *reclaimed land* ardhi ambayo tofauti na hii ambayo tunayo *natural land* ardhi ambayo inafanywa kwa mikono ya watu. Mfano wa Saateni pale kwenye soko letu hapakuwa na ardhi lakini pamejazwa hivi sasa imekuwa ni ardhi tayari sasa. Darajani pale ambapo watoto wanafanya mikutano ya hadhara zamani na sasa hivi pana uwanja mkubwa na ilikuwa ni bahari, lakini sasa hivi pamejazwa ni ardhi, nayo pia ameshauri kwamba tuingize katika tafsiri ya ardhi ya Zanzibar nakubali ushauri wake huu Mhe. Spika.

Halafu Mhe. Jussa pia alizungumzia suala la Fungu Mbaraka ambalo limeshatolewa ufafanuzi na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa kweli nathubutu kusema kwamba namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu ufafanuzi alioutoa mimi ungenishinda kuutoa hapa, kwa sababu uchambuzi wa kina wenye tarehe na kila kitu tofauti saa ndio haikuwemo kwenye uchambuzi ule, lakini tarehe zote zimo na kila kitu. Kwa hivyo, inaonesha wazi kwamba Kisiwa cha Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar na inaonesha kwamba katika wakati mrefu hakukuwa na hayo. Pia amegusia kitu kule mwisho aliposema kwamba hili limekuja sasa hivi wakati ambapo gesi imekuwa ni suala ambalo linatafutwa hivi sasa na mafuta ndio limekuja, lakini huko nyuma halikuweko na tutaendelea kuishi kwa amani kama tulivyoishi siku za zamani hapa.

Mhe. Ismail Jussa amependekeza pia kifungu cha 47 nacho tutapoleta marekebisho mengine tukitizame ambacho kilirejeshwa katika marekebisho yaliyofanyika hapa kuweka mwaka 1999. Pendekezo zuri na nalikubali na nitalifanyia kazi kama alivyokwishatoa Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Saleh Nassor Juma amezungumzia juu ya suala la ardhi ya Makaani; ni ardhi ambayo wananchi wamekuwa wakiitumia kwa kuendesha maisha yao ardhi ile. Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Saleh Nassor kwamba tusipoangalia basi kutakuwa kuna wananchi hawana mahala pa kulima wala pa kufanyia ufugaji wala kufanya shughuli nyengine yoyote madhali hawana ardhi.

Juzi nilikuweko Pemba na nilikuwa nikisaini hati za ardhi. Kwa kweli nilizikataa hati zote zilizoletwa kuhusu ardhi za Makaani, nilizikataa na sikuzitia saini na nilisema haiwezekani ardhi hii tukaanza kuwapimia watu na kuigawa nayo vile vile wakati kuna wanyonge wanahitaji kuitumia ardhi hii katika matumizi yao ya kila siku, ile ibakie kuwa ni ardhi ya serikali na wananchi watumie kwa shughuli mbali mbali za mifugo na mambo mengineyo. Ardhi ambayo tunaigawa eka ni ardhi ya kilimo hiyo ndio tunawapa watu, na ardhi ambayo tunaiwekeza ni ardhi ambayo tunaamua makusudi kwamba eneo hili ni la uwekezaji, tumetayarisha *master plan* ya zamani na hivi sasa tunatengeneza *master plan* mpya ya kugawa matumizi ya ardhi ili yaendane na maisha ya watu wetu wote hapa na isiwe kwamba kila mahala anachukua mtu anapafanya mali yake. Nakubaliana naye sana Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 8 kilichozungumzia kwamba atakuwa na haki ya kumiliki ardhi yule aliyekuwa Mzanzibari, akazungumzia juu ya suala la Ndugu Kurwa. Mhe. Spika, suala hili linahitaji kutizamwa kisheria ambaye yeye alipigwa *PI* na ikabidi amerejeshwa Tabora na anasema ana ardhi yao kule. Lakini pia huyo ndugu Kurwa anaweza akaingia katika Kifungu cha X Mzanzibari au aliyekuwa Mzanzibari na nafikiri ataendelea kuwa Mzanzibari isipokuwa katiwa adabu fulani tu halafu bila shaka adabu ile itamalizika hakuna tatizo lolote.
Kwa hivyo, hii nasema siwezi kuitolea ufafanuzi hapa kwa sababu lazima nijue ile sheria ya *PI* inamalizika vipi na inakuwa vipi, hivyo siwezi kutolea ufafanuzi hapa.

Mhe. Asaa Othman Hamad amezungumzia kuhusu wazee waliokuwa hawana hati. Mhe. Spika, kwa sasa kuna utaratibu maalumu wa kuwatambua wamiliki wote wa haki ya matumizi ya ardhi kwa mikoa yote mitano ya Unguja na Pemba. Utaratibu huo unaendeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Finland chini ya Mradi wa *SMOLE,* na pia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia mradi wa MKURABITA. Kwa hiyo kwa kupitia mradi huu wananchi wote waliokuwa hawana hati lakini wakathibitishwa kuwa ni wamiliki halali wataweza kusajiliwa katika daftari la usajili, tunajua kwamba matatizo hayo yametokezea na watu ambao wanazo ardhi kweli na hawana hati na hivi sasa

ndio tukaanzisha hiki kitengo cha Usajili wa Ardhi ili kutatua matatizo haya ambayo tumekuwa nayo hapa.

Halafu pia amezungumzia juu ya eka kuuzwa. Mhe. Spika, ni kweli eka haina ruhusa ya kuuzwa lakini hili suala mtambuka linatuhusu katika maeneo mbali mbali, kuuza eka ni kosa kwa sababu eka unapewa kwa ajili ya matumizi na inabakia kwamba ile ni mali ya serikali. Katika ile hati ya eka pia imeelezwa kwamba ukiondoka mwenyewe nani anarithi na nani atafuatia kurithi baada ya huyo mwengine uliyemuachia urithi, kwa hivyo ile inakuwa haiuzwi inabakia *intact* vile vile. Hili tatizo lipo na kwa kweli kama kuna watu wanauza eka wanafanya kosa kubwa sana iliyobakia turudi kwenye sheria zetu za ardhi ili tutekeleze kama vile inavyotakiwa kutekeleza kwenye masuala ya eka. Mimi Mhe. Spika, kwa mtu yeyote anayekuja kwangu na akasema ameinunua ardhi ninapomhoji umepata vipi akanambia ilikuwa eka sitii saini hati hiyo, namwambia kabisa hii sitii saini kwa sababu najua eka haiuzwi na wameshatokea wawili watatu na nishawambia kwamba madhali ni eka mimi sitii saini ya kukumilikisha ardhi hiyo, hiyo ni ardhi ya serikali kama huitaki tafadhali irejeshe serikalini ili atafutwe mtu mwengine apewe heka hiyo badala ya wewe kwenda kuiuza eka hiyo.

Suala la Kisiwa cha Fungu Mbaraka limeshazungumzwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Lakini kuna kitu chengine ambacho nataka nikizungumzie hapa hapa nisije nikakisahau. Mhe. Spika, katika ardhi tunapowapa wananchi tuna hati namna mbili, kuna *provisional right of occupancy* yaani hati ya muda, na kuna *right of occupancy* tunampa mtu baada ya kuiendeleza ile ardhi. Pale ofisini kwangu faili nikilitizama tu najua kama hii ni *provisional* kwa sababu lina rangi yake maalum, *provisional* haiuzwi, mtu akipewa kiwanja Tunguu anapewa hati ya *provisional* wakati hajakijenga kile kiwanja, anatakiwa akiendeleze akishamaliza kujenga ndio anakuja tena ofisini kuchukua hati ya kudumu ya matumizi ya ardhi ile, ukiuza *provisional* tunachotakiwa kufanya tukunyang'anye na tuirejeshe serikalini ardhi ile kwa sababu umeiuza kabla hujaiendeleza. Hili ni kosa kwa mujibu wa sheria yetu, *provisional* haiuzwi, sasa watu waliouza wajitizame vizuri kuwa wamefanya makosa kuuza kiwanja ulichopewa na serikali, *provisional* haiuzwi. Hili naona niliseme hapa na tuelewane kwamba ukishakiendeleza kiwanja umejenga nyumba pale hapo tena unaruhusiwa kumuuzia mtu mwengine ambayo inaitwa *land transfer* unahaulisha kutoka kwako kumpa mtu mwengine.

Kwa hivyo, waliouza viwanja ambavyo hawakuviendeleza wajue kwamba wizara yangu inayo haki ya kuvirejesha serikalini na Mhe. Spika, nikivigundua navirejesha serikalini kwa sababu huwezi kuuza *provisional,* ile hati ya muda ya kupewa kile kiwanja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla amezungumzia thamani ya fidia ya ardhi ilivyokuwa mali wakati huu, ardhi hiyo ya kiwanja ikauzwa kwa thamani kubwa itabidi serikali ilipe kwa thamani ile haiyumkiniki sheria inakataza kuuza *provisional*. Kwa hivyo, Mheshimiwa kama ameuza kiwanja chake huyo aliyenunua yuko matatani kama tukimgundua tunaweza kumnyang'anya wakati wowote kwa mujibu wa sheria yetu, hicho kiwanja umepewa ujiendeleze wewe ujenge wewe, hapo katikati ujenzi umekushinda umeuza hilo tena suala jengine lakini ukiendeleze usifanye *transfer* kabla hujakiendeleza kiwanja hicho. Kwa hivyo, hicho Mhe. Abdalla Juma namjibu Mhe. Spika, kwamba si sheria kuuza *provisional certificate* katika utaratibu wetu. Serikali tunajitahidi kusimamia masuala haya na ni moja katika mgogoro mkubwa.

Hivi juzi nilikuwa nikitoa hati na nikayagundua makosa haya kwamba watu wanauza viwanja, anakuja mtu pale unamuuliza kiwanja umekipata vipi aa nimenunua, kwa nani? Kwa fulani. Nipe uhaulisho wako, hana uhaulisho, sasa ulikipata vipi hiyo hati siisaini mimi na sikuzisaini zimeondoka wamekwenda zao. Kwa sababu kiwanja unapewa muda wa miaka miwili, muda wa miaka miwili kiwanja ukiendeleze ikimalizika miaka miwili kiwanja hujakiendeleza tuna haki ya kukichukua sisi kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, wenzangu Waheshimiwa wenye viwanja ambao mmeweka kama ni vitega uchumi mpate mtu wa kumuuzia tutavirejesha serikalini hivyo.

Mhe. Spika, hilo zoezi linaendelea, wapige makofi lakini hilo zoezi linaendelea.

Halafu kwenye suala la kujenga nje ya mipaka ya *beacon* ambayo alizungumza Mhe. Abdalla Juma. Ni kweli tatizo hili lipo lakini mimi mwenyewe nishasema kwamba ukija ukileta lalamiko basi bila shaka watu wa upimaji wanaweza kuiondoa *beacon* hata kama umeitia ndani ya chumba chako, wakipima watakwambia *beacon* ilikuweko chumba hiki hapa ndipo ilipokuwepo umeing'oa wewe wanajua hilo, watu wa ardhi wakishaipata *beacon* moja tu watazigundua nyengine zote za eneo lote sio za kiwanja kile tu. Kwa hivyo kama unataka kufanya ghalati nafikiri ung'oe *beacon* za eneo zima lile la Tunguu lakini kama hujang'oa watagundua wao wapi *beacon* ilikuwepo pale.

Kwa hivyo, Mhe. Abdalla Juma pia amesema kwamba kuweka kifungu katika sheria mama kinachohusiana na ukataji wa viwanja kwa wananchi na ujenzi holela. Hili tunataka tulitekeleze Mhe. Spika, na naona hapa bora nitoe wito. Wananchi kwanza waondoe hofu wakubali kwamba maeneo yao yapimwe halafu wapewe wenyewe katika yale maeneo, lakini nyumba zipangwe sio

tuweke nyumba moja mlango Kaskazi, moja mlango Kusini, huyu dirisha lake liko chooni huyu wapi, hivyo sivyo hatuendelei, kama mnataka tuendelee basi nyumba zipangwe kwa *line* maalum ijulikane hapa nyumba, hapa skuli, hapa uwanja wa michezo, hapa nini na hiyo ndio kazi inayofanywa na Mipango Miji, lakini leo ukienda hata katika maeneo ya uwanda ukisema unapima watu wanakuja na mapanga kwa nini unapima katika eneo hili? Mhe. Spika, tutakawia kuiendeleza nchi hii kama tutaendelea na utaratibu huu. Mimi nawatoa hofu wakubali wananchi wawe wako Matemwe, wako Nungwi tupime tukisha tuwagaie viwanja wachukue viwanja wajenge na nyumba zipangike vizuri pale, hiyo ndio tutakuwa tumeipanga nchi yetu kuliko kila mtu kukimbilia kuuza.

Mheshimiwa mmoja alisema hapa kwamba watu wanaigeuza ardhi sasa hivi kuwa ni pesa yaani watapata pesa kwa kutumia ardhi na ndio chanzo cha migogoro mingi tunayoendelea nayo hivi sasa. Kwa hivyo, mimi nashauri Mhe. Spika, wananchi wakubali ardhi ipimwe ikiwa iko Matemwe, ikiwa iko Jambiani, ikiwa iko Paje wapimiwe maeneo yale ambayo ni ardhi ya serikali.

Halafu Mhe. Spika, tunashangaa vurugu zote hizi hazifanywi katika mashamba ya watu zinafanywa katika mashamba ambayo asili yake ni mali ya serikali au *community land* katika nyiwanda ndio vurugu hizi za mtu kwenda kupima akauza yeye, anaondoka yeye kule ndiye *land lord* anauza uwanda kiholela kabisa, Mheshimiwa hili linatia uchungu sana katika suala la ku- *administer* ardhi, linatupa matatizo makubwa sana. Nawaomba wenzangu tumekusudia kuleta maendeleo ya Januari, 1964 kuiendeleza nchi hii, pamoja na kuiendeleza tuipangeni hii nchi isiwe hivi ilivyo, tuipangeni vizuri miji yetu mtu akienda Jambiani anaukuta mji umepangika vizuri kabisa, akienda Paje umepangika vizuri, akienda Nungwi umepangika vizuri kabisa tufanye hivyo halafu watu wajenge kule katika maeneo yale vizuri. Naogopa Mhe. Spika, tusije tukageuka makumbusho duniani ya nyumba zilizokaa vibaya ikawa mzungu anataka kuona nyumba zilizokaa vibaya anakuja Zanzibar, akitaka kuona vurugu anakuja Zanzibar kama yale yanayotokea sasa hivi.

Mhe. Spika, kuna mambo yanatokea hapa katika nchi yetu sasa hivi yananishangaza kweli na mimi ningewasihi watu wanaohusika na masuala ya utalii wakalitizama sana. Atamchukua mtalii atampeleka katika soko la samaki anamfanya yule mtalii asiende kula samaki, huo ndio ukweli. Lakini anapomuona mtalii kazunguka kashughulika kupiga picha na nini anaona mtalii kapapenda hapa. Mimi naona tuhimizane kusafisha masoko yetu watalii wakija waone katika hali halisi kuliko kumchukua mtalii ukampeleka pahala ambapo kuna-*mess* na wewe unasema unatangaza utalii unampeleka mtalii mahala kwenye *mess* kabisa si vizuri kusema kweli.

Kwa hivyo, na hizi nyumba zetu ni vizuri tuzipange vizuri kabisa na ndio shabaha ya Mapinduzi ya Januari ya 1964, ndio maana Mzee Abeid Amani Karume akaanza kujenga majumba ya kuonesha mfano na Mzee Aboud Jumbe akaja akaendelea kujenga nyumba ndogo ndogo naye akaonesha mfano katika vijiji mbali mbali wananchi tu-*respond* kuelekea huko, tupimiwe viwanja vipangwe vizuri ili miji yetu iwe mizuri kabisa. Kwa hivyo, nakubaliana na Mhe. Abdalla Juma juu ya ujenzi holela ni suala ambalo tunalifanyia kazi vizuri hivi sasa. Suala hilo wizara imeliona na ni moja kati ya chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi, wizara tayari imeshatayarisha mfumo mpya kudhibiti ujenzi holela ambapo wakati wowote kuanzia sasa utaanza kutumika.

Mhe. Spika, hili suala la kwamba fidia ni ndogo, fidia tunazi-*revise* kila wakati kama tunavyo *revise* kodi zetu za ardhi. Lakini kuna ardhi ambazo zimekaa hazitumiki, kuna *speculators* wanachukua ardhi halafu wamezizungushia makuta ardhi zile hawazitumii zimekaa tu pale wala mwananchi mwengine hazitumii naye kaziweka anaranda Ulaya kutafuta mwekezaji aje amuuzie.

Mhe. Spika, ninayo orodha ya ardhi zisizopungua 270 ninazirejesha serikalini keshokutwa na tayari tumezigawa katika maeneo manne hivi.

Kuna ardhi ambayo mtu kaizuia tu lakini hana mradi nayo wala hakupewa kibali kachukua kwa nguvu zake katafuta watu wamejenga makuta hivi wamezungusha ile ardhi wamezuia tu wanatafuta watu waje wawauzie. Hiyo inarudi serikalini.

Kuna ardhi watu ambao wamepewa kutoka *ZIPA* waweke mradi muda wa kukaa na ardhi ile ni miezi 30, miezi 30 imepita sasa hivi ana mwaka wa 15 hajaweka mradi wowote hiyo inarudi serikalini na *ZIPA* keshashauri kama ardhi nane sasa hivi tayari zirejeshwe serikalini na vijana wangu tayari wananitayarishia hati niisaini ili zirejeshwe serikalini na ziko tayari zitarudi serikalini. Nimeshatoa kibali kwa hizo kwamba sasa hivi tayari zirudi serikalini maana wale wanachambua mradi muda wake na kila kitu, wale ndio wanaotoa vibali wakifuta mradi mimi nafuta ardhi ndio jambo lenyewe hilo.
Mhe. Spika, sifanyi hivi kwa kuwakomoa, tunafaya sheria zetu wenyewe tulizozitunga ndani ya Baraza hili hatumkomoi mtu wala hatutoki nje ya sheria, tunakwenda kwa mujibu wa sheria. Miezi 30 imewekwa kwa mradi ikifika miezi 30 hujaendeleza imeshapita sheria ipo utaratibu wa kuifuta tunaifuta ile ardhi tunairejesha serikalini.

Mhe. Spika, hii nchi tunataka tuiendeleze iwepo miradi ya uhakika inayotupatia mapato sio yawepo makuta hayatii mapato yoyote yamewekwa tu pale hiyo inakuwa si nzuri Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame amezungumzia juu ya suala la ujenzi holela nimeshalijibu suala lake nakubali suala hilo tutakuja kuzungumza pamoja. Halafu mtindo wa watu kurithi mali ambayo sio yao, nakubaliana naye utaratibu huu upo, ndio huu niliokwisha kuueleza mtu anakwenda kwenye uwanda anajipimia anaweka ukuta anasema ni mali yake. Hiyo ndio kurithi mali ambayo si yao. Na wengine wanaingia kwenye mashamba ambayo yamegaiwa eka eka ambapo mwenyewe keshafariki watoto hawana habari nayo, kwa hivyo imekaa pale anasema heka hii ni yangu anachukua. Hiyo vile vile ni kweli mali ambayo si yake anaichukua.

Halafu kuna mashamba ya mikarafuu napenda kumjibu Mhe. Asha Bakari Makame kwamba kwa sasa hivi mashamba yote ya mikarafuu ambayo hayana wenyewe yako chini ya Wizara ya Kilimo na wao wametengeneza utaratibu wa kuweza kuyakodisha na kuyashughulikia kwa ajili ya kulimia na mambo mengineyo.

Kisiwa cha Fungu Mbaraka kimeshazungumzwa kama vile alivyokitaja Mwanasheria Mkuu, Naibu wangu ameshatoa mchango mzuri namshukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumzia suala la umuliki wa vitalu vya gesi. Nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma nafikiri anasema watu wa siku hizi wanasayansi wanaweza wakapatizama mahala wakajua kama chini kuna gesi kabla hawajachimba wakaitaka ardhi ile kwa sababu wanajua kwamba pale chini pana gesi.

Sasa huyu atalipwa kwa thamani ya namna gani ile ya gesi au vipi? Nasema ardhi ni mali ya Serikali na kilioko chini ya ardhi ni mali ya serikali na kilichokuweko juu kisichohamishika ni mali ya serikali. Tutamlipa kwa ile tunavyotumia sisi utaratibu wa *location* mahala gani ardhi ipo kama ni pwani tunajua pwani kukoje, kama sokoni tunajua sokoni kukoje, kama ni wapi tutamlipa hivyo. Kilichopo kule ni mali yenu wananchi ni kama mafuta, iwe gesi, ni mali ya wananchi.

Mhe. Spika, nimejaribu kutoa ufafanuzi wa hapa na pale kwa sheria hii. Lakini nasema kwamba nadhani sasa imefika wakati ardhi ishughulikiwe kikweli kweli tusifanye masihara tena, tuondoshe tamaa tushughulikie ardhi ili faida ya ardhi iende kwa wananchi wote. Baada ya kwenda kwa mtu

mmoja mmoja hiyo tutakuwa tunavunja Katiba yetu ambayo inasema kwamba faida ya mali ya taifa iende kwa watu wote kwa kupitia serikali yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri tunakushukuru kwa ufafanuzi huo wa kina ambao umeutoa na hatimaye ukamalizia kutoa hoja.

Mhe.Waziri Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 2	Marekebisho ya Sheria ya Umilikaji Ardhi namba 12 ya mwaka 1992
Kifungu 3	Marekebisho ya kifungu cha pili pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha 8 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5	Marekebisho ya kifungu cha 56 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	Kusomwa pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya kutunga sheria imepitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya mwaka 2013 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na mswada huo katika kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada ya Sheria wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya mwaka 2013 ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Katibu ananambia kwamba shughuli zilizopangwa kwa ajili ya leo zimemalizika na hakuna shughuli nyengine kwa leo. Hii maana yake sasa tukapumzike.Lakini naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango ambayo mmeitoa haidhuru kuna Waheshimiwa wengine hawapo lakini baadaye wakataka kuchangia.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wakati mjadala ukiendelea Wajumbe wengi tuwepo ili iwasaidie Wajumbe wengine wasikie yanayozungumzwa, hii itaepusha ile kurejea rejea, lakini kama utakuwa hupo kwa muda mkubwa halafu baadaye utaingia unataka kuchangia tabaan utayosema itakuwa yameshazungumzwa na wengi.

Niseme haya kumwambia Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa sababu kimsingi mchango wake kwa mujibu wa maelezo aliyotoa Mhe. Waziri katika kutoa majumuisho kwa kweli ilikuwa haijachangiwa na Mjumbe yeyote. Kwa hiyo, nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa ambayo mmetoa kwa kuendesha shughuli zetu.

Baada ya hayo basi tusitishe shughuli zetu hapa, na kwa maana hiyo basi niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 10/10/2013. Saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 12:13 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 10/10/2013. Saa 3:00 asubuhi)